**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NANE**

**Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 2 Agosti, 2007**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mhe. Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha, 2007/2008.

**MHE AME PANDU AME – (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NCHI ZA NJE):**

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. ABUBAKARY KHAMIS BAKARY - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka fedha 2007/2008

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa kawaida huwa tunatambulisha wageni wetu wakati wa kipindi baada ya maswali. Lakini leo kwa huyu mmoja nimeona nitangulie mapema tu kumtambulisha kwa sababu ya umuhimu wake naye si mwingine ni Mheshimiwa Fredrick Tuluway Sumaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Sumaye, karibu sana katika ukumbi huu. Tunakukaribisha sana umehusika sana na kuwepo wa Ukumbi huu kwa sababu wewe ndiyo uliyeweka jiwe la msingi la jengo jipya la Bunge na pia umejichomoza kuwa ni Waziri Mkuu Mstaafu ambaye katika kipindi chako umekaa katika nafasi hiyo kwa miaka kumi mfululizo. (*Makofi*)

Tumefurahi zaidi kwamba kwa unyenyekevu kabisa ulikwenda darasani na umerudi na Shahada ya *Masters.* Tunakushukuru sana kwa mfano huo na tunakuombea mafanikio katika shughuli zako. Katibu Shughuli inayofuata.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 337

**Huduma ya Afya Siha**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI –(K.n.y. MHE. AGGREY D.J. MWANRI)** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu wananchi wa Wilaya Mpya ya Siha hususan waishio katika Vijiji vya Sanya Juu na Vijiji jirani wamekuwa wakipata huduma za Afya katika Zahanati ya Kanisa la Kilutheri Dayosisi ya Kaskazini(KKKT); na kwa kuwa mpaka sasa hakuna huduma ya aina hiyo inayotolewa na Serikali wala Halmashauri katika maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Zahanati hiyo ili kuimarisha huduma zake na hivyo kuleta manufaa kwa wananchi?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuzisaidia taasisi za aina hiyo kwa kuzipatia wafanyakazi na kuwalipa mishahara hasa ikizingatiwa kuwa huduma hizo zinatakiwa kutolewa na Serikali au Halmashauri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Sanya Juu kinachoendeshwa na Kanisa la Kiluthei Dayosisi ya Kaskazini kimesajiliwa kama Kituo cha Afya na siyo

Zahanati kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Kituo hicho cha Afya kinahudumia wananchi wapatao 14,000 kutoka vijiji vitatu vya Sanya Juu, Koboko na Nrao Kisangara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasaidia kuimarisha utoaji wa huduma katika Zahanati na Vituo vya kutolea huduma za Afya visivyomilikiwa na Serikali. Msaada huo upo katika ngazi mbalimbali ikiwemo mafunzo kwa watumishi, upelekaji wa vifaa na wataalam wa kutoa huduma mbalimbali. Aidha Serikali inatoa fedha za ruzuku na za mfuko wa pamoja wa afya *(Council Health Basket Grant)* ili kuboresha huduma zitolewazo katika hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati za Serikali na taasisi mbalimbali *(voluntary Agencies)* ikiwemo mashirika ya dini. Vituo vya Afya, Zahanati za Serikali na zisizo za Serikali kwa pamoja hutengewa asilimia 15-20 ya Fedha za mfuko wa pamoja wa afya.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Hai kwa mwaka wa fedha 2005/2006 na 2006/2007 ilikisaidia Kituo cha Afya cha Sanya Juu kwa kupeleka madawa na vifaa vyenye thamani ya shilingi 10,195,420/=. Vilevile Halmashauri imefanya ukarabati sehemu ya ushauri nasaha na kupima virusi vya UKIMWI kwa hiari katika mpango wa kuzuia maambukizi ya virusi vya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. (*Prevention of mother to child transmision of the HIV).*

Kituo cha Afya cha Siha kilipewa vifaa na madawa kwa ajili ya huduma za mama na mtoto. Katika mwaka huu wa fedha 2007/2008 Serikali imepanga kukarabati Kituo hicho cha Afya Sanya Juu kwa shilingi 3,597,982.50. na shilingi 5,373,830/- zimetengwa kwa ajili ya kununua vifaa vya tiba.

(b) Serikali inatambua umuhimu wa kusadia Taasisi mbalimbali zinazotoa huduma za Afya zikiwemo Hospitali Teule za Wilaya, vituo vya afya na zahanati. Miongoni mwa miasaada ambayto Serikali inatoa ni pamoja na kupeleka watumishi, madawa, mafunzo na vifaa vya tiba.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyofafanuliwa na Wizara ya Afya alipowasilisha hoja yake hapa Bungeni katika Mkutano huu, watumishi wa Sekta ya Afya wanaajiliwa moja kwa moja kutoka vyuoni pindi wanapohitimu mafunzo. Kwa utaratibu huu angalau tatizo la watumishi litapungua. Kuhusu suala la kulipa mishahara watumishi; Serikali inatoa fedha za mishahara ya watumishi wote na fedha za matumizi ya kawaida (*OC*) kwa hospitali teule zote. Aidha inatoa ruzuku ya vitanda yaani bed grands kwa *DDH* zote hapa nchini. Katika mazingira ambapo hakuna kabisa hospitali au kituo cha afya; Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii hutoa kibali kwa zahanati iliyopo kuweza kulaza wagonjwa walau kwa siku moja na hivyo kustahili kupatiwa ruzuku ya vitanda na mishahara ya watumishi. Watumishi katika zahanati na vituo vya afya vinavyomilikiwa na taasisi binafsi wataendelea kulipwa na taasisi zao.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Siha ni mpya na kimsingi inastahili kuwa na Hospitali yake ya Wilaya. Je, Serikali inaishauri vipi Halmashauri mpya ya Siha sasa ili iweze kujiandaa na kuweza kufanikiwa kupata Hospitali yake ya Wilaya?

La pili, kumekuwa na mlipuko mkuwa wa Watendaji hasa wahudumu, Madaktari na Manesi kutoka katika Taasisi za dini kutaka kuhamishia ajira zao Serikalini na hii imeathiri sana Hospitali nyingi za Taasisi za dini ikiwemo hii ya Kilutheri, KKKT kule Siha pamoja na hospitali teule ya Muheza na hospitali nyingine teule. Serikali inasema nini kuhusu kuzuia mlipuko huu wa uhamishaji wa wafanyakazi kuhamia Serikali?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Hospitali ya Wilaya katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha. Wilaya hii ni mpya na sasa hivi iko kwenye mipango mbalimbali ya kuanzishwa kuanza majengo ya Halmashauri yenyewe pamoja na ya Mkuu wa Wilaya na kadhalika. Kwa hiyo, ninaishauri Halmashauri iweke katika mipango yake kwanza kutenga eneo husika na kuiweka katika Bajeti zao ndipo Serikali itakapoingilia baada ya kupita katika Vikao vinavyohusika.

Kuhusu wafanyakazi wa Taasisi mbalimbali za dini kuhama kutoka kwenye Taasisi hizo na kwenda katika Hospitali za Serikali. Kwanza ningependa tuishukuru Serikali kwa kuongeza mishahara katika sekta ya afya na kusaidia sana kwa kupata watumishi wengi pia Serikali inasaidia kutoa watumishi mbalimbali kwenda katika zahanati na vituo vya taasisi mbalimbali za dini. Kwa hiyo haibagui kwamba wapeleke kwenye vituo vya afya au zahanati za Serikali tu bali inawapeleka pia katika zahanati za binafsi ili kuongeza ufanisi kwa sababu zote zinatoa huduma za kijamii.

Na. 338

**Kukarabati Barabara za Jimbo la Njombe Magharibi**.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA – ( K.n.y. MHE. YONO S. KEVELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara zilizo nyingi katika Jimbo la Njombe Magharibi ni mbovu sana hazipitiki kabisa hadi kufikia kuwa njia za ng’ombe na kwa kuwa barabara hizo hazina madaraja kwa mfano barabara kati ya Kata ya Ilembula na Usuka kupitia Kanamalenga Barabara ya Wanging’ombe na Saja kupitia Ikulimambo na Luduga kupitia Kidugala.

Je, Serikali ina Mkakati dani wa kukarabati barabara hizo pamoja na madaraja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yono Stanley Kevela, Mbunge wa Njombe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba barabara za Jimbo la Njombe Magharibi hazitengenezwi hadi kufikia hatua ya kuwa njia za ng'ombe. Serikali kupitia vyanzo mbalimbali kama Mfuko wa Barabara, Mfuko wa Ruzuku wa Serikali za Mitaa (*LGCDG*) na Mfuko wa Kuendeleza Kilimo *DADPS* inajitahidi kuzifanyia matengenezo barabara za Jimbo la Njombe Magharibi kulingana na Bajeti sawa na Majimbo mengine katika Wilaya ya Njombe.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya awamu ya nne ina nia thabiti ya kuboresha miundombinu ya barabara katika Halmashauri zote nchini kulingana na urefu wa barabara (*network*) za Halmashauri husika. Kwa kutambua umuhimu huo ndiyo maana mwaka huu 2007/2008 Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 65 kwa ajili ya mfuko wa barabara. Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imetengewa kiasi cha shilingi milioni 565.43 ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita ambapo ilipata kiasi cha shilingi milioni 172.14 na wakati huo ikiwa na eneo kubwa zaidi kwa maana ya wilaya nzima ya Njombe tofauti na sasa ambapo fedha hizi ni kwa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe tu ukiondoa Halmashauri ya Mji wa Njombe ambapo nayo imetengewa kiasi cha shilingi milioni 346.73 kwa ajili ya matengenezo ya barabara kutokana na fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 matengenezo ya barabara katika Jimbo la Njombe Magharibi ni kama ifuatavyo:-

Barabara zenye urefu wa Km. 139.1 zitafanyiwa matengenezo ya kawaida kwa kiasi cha shilingi milioni 76.27, barabara zenye urefu wa km 30 zitafanyiwa matengenezo ya sehemu korofi kwa kiasi cha shilingi milioni 45, barabara zenye urefu wa km 9.5 zitafanyiwa matengenezo ya muda maalum kwa kiasi cha shilingi milioni 94.Kuhusu barabara alizozungumzia Mheshimiwa Mbunge, Serikali ina mikakati ifuatavyo:-

(i) Barabara kati ya Kata ya Ilembula na Kata ya Usuka kupitia Kanamalenga. Serikali kupitia mfuko wa ruzuku kwa Serikali za Mitaa inaikarabati barabara hiyo yenye urefu wa Km. 15 na kazi imekwishaanza. Kuhusu daraja lenye sehemu ya juu ya kupitia magari iliyojengwa kwa mbao *wooden deck* linalopitika muda wote, Serikali imeliwekea mikakati ya kulibadili na kuliwekea deki ya zege *(Concrete deck)* ambayo ni ya kudumu kwa muda mrefu zaidi kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

(ii) Kuhusu barabara za Wanging'ombe na Saja Serikali imeziwekea mkakati wa kuzikarabati barabara hizo ni katika mwaka wa fedha 2007/2008. Barabara hizo ni Idofi-Saja km. 12 na Ufwala –Uhenga Km 12.

(iii) Serikali kupitia Bajeti ya mwaka 2007/2008 inategemea kukarabati sehemu korofi katika barabara ya Imalinyi –Kidugala km 11, Estate No. 5 Kidugala –Kigoma Km 40.

(iv) Mheshimiwa Spika, barabara ambazo zimewekewa mikakati ya kukarabatiwa katika kipindi cha mwaka 2007/2008 ambazo zinaunganisha Kata ya Saja na Wanging'ombe ni Katenga – Uhenga Km 14.8, Igomba – Isimike Km 14 na Saja –

Ikulimambo Km.20. Kuhusu barabara za Imalinyi na Luduga kupita Kidugala Serikali imeweka mikakati ya kuzitengeneza barabara zote kwa kipindi cha mwaka 2008/2009. Barabara hizo ni Kidugala – Luduga km. 15 na Imalinyi – Masage km.18.7. Madaraja ya kuunganisha Kata ya Wanging'ombe –Saja Serikali imeweka mikakati ya kuyajenga katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/2009. ili kuyafanya yawe ya kudumu.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, swali moja la nyongeza. Kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri huyu kwa jinsi anavyojibu vizuri maswali ya Wabunge na kwa jinsi anavyojibu kwa undani kama ulivyomwona katika swali hili. Kwa kuwa sasa Wilaya ya Njombe imegawanyika katika Sehemu mbili, eneo moja la Jimbo moja ni mji wa Njombe, na Majimbo yale mawili Magharibi na Kaskazini hayo ndiyo Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambako kama alivyosema ameongeza fedha. Kwa kuwa hiyo mikakati mizuri na kazi tuliyokuwa tunaifanya wakati ule kabla ya mgawanyo huu. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba lile ombi dogo moja tu kwamba aunganishe Lupembe na Taweta kwake kule ndiyo wakati mwafaka sasa wa kuleta Wilaya nzima kama Mheshimiwa Waziri aliyosema?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, Ombi lake tumelipokea katika Wizara ya Miundombinu na tumewaelekeza Mameneja wa Mikoa ya Morogoro na Iringa ili wafanye mapitio ya barabara hii inayotoka Taweta, Lupembe mpaka Madeke. Tukishapata taarifa hiyo ndiyo tutaona ni nini sasa tuweze kufanya katika barabara hiyo kama ni kuipandisha kuwa ya Mkoa. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo kubwa la barabara hizi za Njombe Magharibi ni kwamba zinatengenezwa kwa kiwango ambacho ni cha changarawe si cha lami na hivyo kupelekea kila mwaka katika Bajeti kutengewa fedha. Je, Serikali haioni wakati umefika sasa wa kutenga fedha zikatengenezwa barabara chache za Njombe Magharibi lakini kwa kiwango cha lami na hatimaye kumaliza tatizo hili la barabara?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya kawaida mimi ningeweza nikatoa kibali cha fedha hizo zote zilizotengwa kwa ajili Wilaya hii ya Njombe ambayo ukiondoa ile ya Mjini wazipangie waone kama zinaweza zikajenga lami na waamue lami hiyo ijengwe kwenye Jimbo lipi kati ya Majimbo hayo mawili. Maana yake ni nini? Ni kwamba uwezo wa Serikali kwa sasa ndiyo huo ambao tulionao. Shilingi milioni 500 kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika majengo yote mawili. Uwezo wa Serikali utakapokuwa na kutuwezesha kuwa na uwezo wa kujenga lami nchi kubwa kama hii katika maeneo ya vijijini basi tutafanya hivyo.

**SPIKA:** Ahsante sana kabla hatujaendelea ninataka kusema tu kwamba kwa kuwa Njombe ina Majimbo matatu pamoja na la Naibu Spika, pengine nalo lisiweze kusahauliwa. (*Makofi*)

Na. 339

## Mahitaji ya Umeme Wilayani Lushoto

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa karibu nusu ya Wilaya nzima ya Lushoto hasa katika Tarafa za Kaskazini ikiwemo na Tarafa za Mlola hazina umeme na kwa sababu hiyo, wananchi katika maeneo hayo hudumaa kimaendeleo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa uhakika wa kuwafikishia wananchi wa Mlola huduma ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Hassan Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuyapatia umeme maeneo yote nchini yenye mahitaji ya nishati hiyo kwa lengo la kuhamasisha maendeleo endelevu. Hata hivyo kutokana na maeneo kuwa mengi na upelekaji wa umeme katika maeneo hayo kuhitaji fedha nyingi inalazimu utekelezaji wa miradi ya kupeleka umeme katika maeneo hayo kufanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.Upelekaji wa umeme katika maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge utafanyika kwa awamu kupitia mpango wa usambazaji wa umeme nchini utakaotekelezwa chini ya Wakala wa Nishati Vijiji *(Rural Enegy Agency*). Kati ya kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara mwaka 2007/2008 ni uanzishwaji wa Wakala hiyo pamoja na mfuko wake *(Rural Enegy Fund);* na mwaka huu Wizara imepanga shilingi bilioni 10 kama kianzio.

**MHE. BALOZI ABDI HASSAN MSHANGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nipatia nafasi kuuliza swali la dogo tu la nyongeza. Tarafa ya Mlola yenye Kata nne inazungukwa na Kata zenye umeme au miradi ya umeme kwa mfano Kata ya Ngwelo inapakana na Kata ya Mlalo ambako kuna umeme umbali wa kama km 10, na Kata ya Malibwi ambayo ni ya tatu Wilayani Lushoto kwa idadi kubwa ya watu na Maendeleo makubwa inapakana na Kata ya Kwai ambako umeme umefika. Kata ya Makanya inapakana na Kata ya Mgwashi ambapo sasa hivi kuna mradi wa umeme katika Jimbo la Bumbuli.

Je, isingekuwa busara kuunganisha Kata hii ya Makanya na mradi ule Mbwashi kufikisha umeme huu wa Mlalo ukafika Ngwelo na Mlola na kufikisha umeme huu wa Kwai ukafika Malibwi kwa vile *distance* ni dogo na njia ya kupita umeme ni rahisi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli ni busara kwa jiografia jinsi ilivyo ya Jimbo lake, tunaona kwamba kuna busara na Serikali kama ilivyosema kwenye jibu la msingi tuna nia ya dhati. Nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutawaelekeza *TANESCO* waanze kufanya kazi za awali kwa maana ya upembuzi kujua gharama hasa zinazohitajika kwa ajili ya kufikisha umeme maeneo ya Mheshimiwa Mbunge. Baada ya hapo taratibu za kifedha zitaendelea.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la Wilaya ya Lushoto linafanana sana na tatizo la Wilaya ya Meatu; na kwa kuwa Serikali imeahidi kupanua mtandao wa umeme vijijini.

Je, Serikali itatimiza lini ahadi yake ya kupeleka umeme mji mdogo wa Mwandoya kupitia vijiji vya Isengwa, Mbalagane, Lubiga na Mwandoya yenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, Serikali tunaendelea kutekeleza ahadi za ufikishaji wa huduma mbalimbali katika maeneo ambayo Serikali ilishaahidi na bahati nzuri ni kwamba Mheshimiwa Mpina ni kati ya Waheshimiwa Wabunge ambao yeye na Ofisi yetu imekuwa ikifanya kazi kwa karibu sana maombi yake tunayafanyia kazi na tunaendelea kumwahidi kwamba tunayafanyia kazi na tutamtaarifu jinsi ambavyo upatikanaji wa fedha utakuwa unaendelea.

Na. 340

**Sera na Sheria ya Madini**

**MHE. BAKAR SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Sera na Sheria ya Madini nchini hazifanani:-

(a) Je, ni kiwango gani wananchi wanaoishi maeneo ya migodi wananufaika?

(b) Je, ni lini Serikali itafanya marekebisho sera na sheria ya madini ili wananchi wanaokataa maeneo ya migodi hiyo wapate kunufaika?

(c) Kama sera na sheria hiyo imerekebishwa ni manufaa gani ambayo wamepata watu waishio maeneo hayo baada ya marekebisho kufanyika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a), (b) na (c) naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 1997 Serikali ilitunga Sera ya Madini inayotoa dira na mwongozo wa Serikali katika kusimamia shughuli a madini hapa nchini. Sera hiyo inaelekeza kampuni za madini kushiriki katika shughuli za kijamii na kiuchumi kwa maeneo yaliyo jarani na migodi yao. Katika kutekeleza mwongozo wa Sera hiyo, Serikali ilitunga Sheria ya Madini ya mwaka 1998.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii Sera na Sheria ya madini zinaendana kwani Sheria ya madini ya mwaka 1998 ilitungwa ili kutekeleza sera ya Madini ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kampuni zinazomiliki migodi zimekuwa zikichangia katika huduma za Maendeleo ya jamii katika maeneo yanayozunguka migodi yao. Huduma zinazochangiwa na kampuni hizo ni pamoja na ujenzi wa shule, zahanati na miundombinu ya barabara na maji. Migodi hiyo pia hutoa ajira na kununua hudama na bidhaa mbalimbali kutoka kwa wananchi wa maeneo yanayozunguka migodi.

Hata hivyo Serikali inaendelea kuhimiza kampuni zinazomiliki migodi kuchangia zaidi ili wananchi wanaozunguka migodi wanufaike zaidi. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Sera na Sheria za madini zilizopo kwa sasa zinatoa fursa kwa wananchi walio karibu na migodi kunufaika na migodi hiyo. Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba Watanzania wananufaika zaidi na sekta ya madini, mwezi Februari, 2004 Serikali iliunda Tume ya Kudurusu Sera ya Madini na kutathmini zinazoikabili sekta ili kutoa mapendekezo yenye lengo la kuinua mchango wa sekta ya madini kwenye uchumi wa Taifa. Tume hiyo ilikamilisha kazi yake mwezi Desemba 2004 na kuwasilisha taarifa yake Serikalini. Serikali inaendelea na mchakato wa kuidurusu Sera ya Madini kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, wananchi walio jirani na migodi wananufaika na huduma za kijamii zinazochangiwa na migodi iliyo jirani na maeneo haya. Ukamilishaji wa marekebisho ya Sera ya Madini kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume yatawanufaisha zaidi wananchi walio karibu na migodi.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Je, Serikali itakubaliana na ushauri wa kuongeza mrahaba kutoka asilimia 3 na kufikia asilimia 5 na kwamba asilimia 2 ibakie kwenye Halmashauri za Wilaya zenye Migodi ili wananchi wapate kufaidika zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nifafanue kwa faida ya Bunge hili Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba, kwa sasa hivi mrahaba uliopo ni kwamba kwa madini yasiyokuwa ya vito (Almasi na madini mengine) mrahaba unatozwa ni asilimia 3. Lakini kwa madini mengine ni asilimia 5.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tunauzingatia, lakini niseme tu kwamba tunachofanya sasa hivi wakati tunaidurusu sera na sheria yake ni kuhakikisha kwamba tunakwenda mbele zaidi ya kuangalia mrahaba tu. Kuna mambo mengi ya kuzingatia, lakini kwa kweli tunaheshimu sana maoni yake. Kuhusu suala la

asilimia 2 kubaki kwenye Halmashauri ni mambo ambayo siwezi kuyatolea jibu sasa hivi la moja kwa moja kwa sababu mchakato wa kuidurusu sera una hatua zake na unawashirikisha wadau mbali mbali. Tunahitaji kujiridhisha kwa pamoja ili tufikie muafaka ambao una maslahi kwa watu wengi kwa maana ya Taifa zima. Lakini, tunazingatia maoni na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. DR. RAPHAEL M CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda nimwulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa toka mwaka 2004 bado tunajaribu kudurusu sheria au muswada mpya wa madini. Lakini ukiangalia kwamba *the Corporate Social Responsibility* ya Makampuni haya ni ya hiari. Sasa Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuweka utaratibu maalum kwamba kila mgodi uweze kuchangia walau asilimia fulani ya mapato yao katika maeneo ambayo migodi ilipo ili kuacha huu wajibu wa kwamba wanachangia kwa hiari shughuli mbali mbali za Maendeleo katika maeneo husika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niseme tu kwamba msingi wa kwa nini michango ya shughuli za Maendeleo ya jamii na huduma mbali mbali katika jamii zinazofanywa na makampuni ya migodi na hata wawekezaji wengine kuwa hiari ni kwamba hili ni suala ambalo kimsingi ni *conventional*, ni suala linalohusu nchi nyingi tuseme ni jambo ambalo limeishakuwa kama utamaduni, si jambo la kisheria wala si jambo la kanuni ambazo zimewekwa. Kwa hiyo, ni suala la hiari kwa sababu haiwalazimishi na michango yao wanayoifanya, nirudie tu kusema kwamba kimsingi si mbadala ya mipango na majukumu ya Serikali Kuu. Lakini tunafahamu kwamba Maendeleo yanafanywa kwa ushirika wa wadau mbali mbali wakiwemo wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kuweka utaratibu, kwa kweli tutakuwa tumekwenda mbele zaidi tofauti na nchi zingine. Tunafahamu hata nchi zingine ambako shughuli hizi zinaendelea kufanyika ambako wenzetu wana uzoefu zaidi. Jambo la uchangiaji halijawahi kuwa ni jambo la kisheria, lakini tunaheshimu maoni ya Mbunge kwamba pengine wakati umefika kwa jinsi ambavyo jamii na wadau katika nchi yetu wataona inafaa. Lakini kwa sasa hivi tukubali kwamba ni jambo ambalo linafanyika duniani kote. *Corporate Social Responsibility* ni jambo la hiari, lakini pia uhiari wake umeishakuwa kama ni utamaduni na mila kwa wawekezaji wengi.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante! Kwa kuwa suala la Kilindi haliko mbali sana na haya yaliyoulizwa, tofauti ni kwamba kule kwetu bado hakuna vibali vya uchimbaji, ni vya utafiti *(PL)*. Sasa, naomba kuuliza wale wananchi wananufaikaje na hawa wanaopewa *PL*, ukizingatia utafiti unafanyika na mpaka utakapomalizika na madini nina hakika yatakuwa yamekwisha. Sasa hawa wananchi kwa sababu wamehamishwa kwenye maeneo yao na wengine hata kwenye vijiji na wamekatazwa kuchimba. Je, wao wanastahili kunufaika nini? Mheshimiwa Spika, ahsante!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba kwanza, fursa ya kuweza jamii kufaidika katika maeneo husika inategemea pia na jinsi gani wananchi wenyewe wanafuata kwa sababu kimsingi si rahisi hawa

wawekezaji kuanza kuomba au mwekezaji yeyote, ninaposema wawekezaji simaanishi wawekezaji wa nje tu, hata wa ndani. Kwanza, lazima kuwe na ombi ambalo linafanywa na wananchi wanaoona kwamba kuna umuhimu ama wanadhani wanahitaji nguvu ya msaada kutoka kwa hao wawekezaji wanaowazunguka.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kwamba Kilindi vibali vinatoka, ofisi yetu inafahamu na kumbukumbu zipo. Lakini ninafahamu pia kuna maeneo mengine katika eneo la Mheshimiwa Mbunge ambayo bado maombi hayajatolewa vibali, lakini kuna sababu maalum, kuna taratibu bado tunazikamilisha hasa kwa wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nalihakikishia Bunge hili Tukufu na wananchi kwa ujumla kwamba wawekezaji tumeona na tumeshuhudia wote, tumekuwa tukisoma kwenye vyombo vya habari kwamba wamekuwa wanaendelea kushirikiana na wananchi kwa kweli. Sisi kama Serikali tunaendelea kulifuatilia hilo zoezi kwa makini na tunaendelea kuwahamasisha wazidi kushiriki. Kwa hiyo, nimwombe Mbunge awasiliane na wawekezaji walioko karibu yake. Lakini, kwa wale ambao wako kwenye hatua za awali za utafutaji wa madini, pengine si kusema kwamba tunajaribu kuwajengea mazingira ya kutoshiriki. Lakini tuseme kwamba wanapokuwa kwenye hatua za awali, inakuwa ngumu kwa sababu wanakuwa hawajaanza kupata faida. Kimsingi michango ya hiari inatokana na faida wanayoipata kutoka kwenye shughuli zile wanazozifanya.

Lakini unapoongelea kwenye hatua ya *Prospecting License*, unaongelea kwenye maana ya utafutaji wa awali. Kwa hiyo, inakuwa bado haujafikia kuanza kuzalisha kibiashara.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufafanuzi juu ya suala lile alilouliza Mheshimiwa Beatrice Shellukindo na kutoa rai kwa Watanzania wote na Wabunge waliopo kwenye Bunge hili wanaweza kutusaidia. *Prospecting License* haimruhusu mtu kuchimba madini kwa biashara, anayefanya hivyo anavunja sheria. Kwa hiyo, kama kuna mtu amepata *Prospecting License* na huku anachimba madini anayafanyia biashara, kama mkimgundua tunaomba mtusaidie mlipoti, tuna maofisa wetu huko katika Kanda wanaangalia hiyo, lakini kama mtu anafanya hivyo, anavunja sheria, inabidi kumnyang'anya hiyo *License* na kuifuta. *(Makofi)*

Na. 341

**Utabiri wa Hali ya Hewa**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI** aliuliza:

Kwa kuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini inafanya kazi ya kuufahamisha Umma wa Watanzania juu ya hali ya hewa; na kwa kuwa wakulima na wafugaji wanapaswa wafahamishwa juu ya hali ya hewa ilivyo, lakini makundi hayo hayajaelimishwa juu ya hali hiyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba makundi hayo yanaelimishwa?

(b) Je, ni sababu gani za msingi/kisayansi zinazoifanya Mamlaka hiyo ishindwe kufanya utabiri wa muda mrefu kama miezi 3 au zaidi ili Serikali na wananchi waweze kukabiliana na majanga mengi yanayosababishwa na hali ya mbaya ya hewa kama vile ukosefu wa mvua uletao ukame?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), napenda nitoe maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa imekuwa ikitoa taarifa zake kuwafahamisha wananchi na taasisi mbali mbali wakiwemo wakulima na wafugaji juu ya mwenendo wa hali ya hewa. Taarifa hizi zimekuwa zikitolewa katika vyombo vya habari kila msimu, kila mwezi, kila siku 10 na kila sherehe za Kitaifa ambazo Mamlaka hushiriki kama vile:- Nane Nane, Siku ya Hali ya Hewa Duniani na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-(a) Serikali kwa kutambua kuwa njia hizo hazikuweza kufanikisha uelimishaji na upashaji wa habari uliokusudiwa hasa kwa wakulima na wafugaji ambao walio wengi wako vijijini na wanaweza kutokuwa na redio, luninga, kutokuwa na uwezo wa kununua magazeti na kuhudhuria sherehe, hivyo imeweza kushirikisha ofisi za Kilimo na Mifugo Wilayani ambazo ziko karibu nao kupelekewa taarifa za hali ya hewa ili wafikishe kwa walengwa. Aidha, kuandaa warsha na kongamano zitakazofanyika katika ngazi za Wilaya na kushirikisha wakulima na wafugaji kutoka maeneo ya Wilaya hizo.

(b) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa hutoa utabiri wa hali ya hewa *(weather outlook)* kila msimu kabla ya kuanza msimu wa mvua husika kueleza hali itakavyokuwa kwa kipindi cha muda wa miezi mbele. Utabiri huo huboreshwa kadri hali inavyojitokeza. Usahihi wa utabiri unategemkea sana ubora wa vifaa, utaalam na mtandano wa vituo. Vifaa vinavyoweza kutoa utabiri wenye usahihi ni pamoja na rada ambazo Tanzania hatuna.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuiwezesha Mamlaka ya Hali ya Hewa kuwezeshwa kupata vifaa na mafunzo yatakayoboresha usahihi wa utabiri wa muda mrefu kadri fedha zitakavyokuwa zinapatikana. *(Makofi)*

**MHE. GOFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa nchi nyingi na hasa zilizoendelea zina uwezo wa kutabiri majanga makubwa yanayojitokeza kwa mfano; Tsunami na majanga ya Ukame na kwa maana hiyo kuwaweka wananchi wetu tayari katika kukabiliana na hali hiyo. Lakini pia kwa kuwa Serikali inasema tatizo ni uwezo wa kifedha lakini bado hili ni suala muhimu zaidi, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kujibana sasa na kuweza kununua vifaa vya kuiwezesha nchi kutabiri majanga kama hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili Sasa hivi kuna utaratibu wa kununua rada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa na kwamba kuna kiasi cha pesa ambacho kimetengwa kwa ajili ya madhumini hayo. Je, ununuzi sasa wa rada hiyo kwa ajili ya kazi hii muhimu utakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mamlaka yetu ya Hali ya Hewa haina vifaa kama ambavyo tungetegemea. Lakini kwa uwezo mdogo walionao na kwa vifaa mbavyo wanavyo, mimi nadhani wanajitahidi sana katika kusaidia kutabiri hali ya hewa na tumeona jinsi ambavyo kwa kipindi kirefu angalau wamekuwa wakipatia pamoja na kwamba kumekuwepo na matatizo ya hapa na pale. Lakini kama nilivyosema tunahitaji kuongeza uwezo na wazo lake hilo la kwamba Serikali sasa ifanye kila linalowezekana kujibana kuongeza fedha kwa ajili ya kuwapatia vifaa vinavyohitajika, hilo tumelizigatia sana na ndio maana katika sehemu ya pili ya swali lake hilo la kunua rada, Serikali toka mwaka jana ilitenga fedha kwa ajili ya kununua rada na mchakato wa kununua rada hiyo umeishafanyika, zabuni zilishatangazwa. Lakini kwa bahati mbaya kwa kweli kumekuwepo na uchelewefu katika mchakato mzima wa kukamilisha zabuni hiyo.

Hii imetokana na ukweli kwamba ilibidi kufuata taratibu za zabuni za kimataifa na vile vile kuwashirikisha wataalam wengine wa masuala ya anga na masuala ya usalama kama Jeshi la Wananchi, kama *TCAA* na vile vile *TICRA*. Nadhani baada ya mchakato huo kukamilika, rada hiyo itaagizwa.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa utabiri wa hali ya hewa haukuwa sahihi kabla ya mvua za Elnino ambapo wakulima wa kilimo cha juu walitakiwa walime mabondeni, lakini baadaye zikaja mvua za Elnino zikaharibu mazao na wakulima wale wakapata hasara nikiwemo mimi. Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuwalipa fidia wakulima kwa kosa ambalo siyo lao?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Serikali huwa haifidii majanga ambayo yanatokana na *act of God* kwa sababu siyo Serikali iliyopanga hivyo. Lakini Serikali inaweza kutoa huduma za dharura kwa maana ya kuwasaidia wananchi waliopata maafa ama kuwa hamisha, kuwajengea labda nyumba za dharura kama msaada katika kitengo chake cha maafa. Lakini, siyo kama fidia.

Na. 342

**Ubovu wa Barabara katika Mikoa**
**yenye Mazao ya Uhakika**

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA (K.n.y. MHE. ANNE K. MALECELA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipokuwa ikijibu Swali Na. 1278 tarehe 13/11/2006 lililohusu malengo ya Milenia, ilikiri wazi kuwa Mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mbeya, Iringa, Kigoma, Manyara, Kilimanjaro, Arusha na Wilaya za Kongwa na Mpwapwa zina uwezo mkubwa wa kuzalisha mpunga na mahindi na kuweza kutosheleza chakula nchini na hata kuuza nje ya nchi kama ardhi yote itatumika kikamilifu na hivyo kuondoa kabisa tatizo la njaa na kupunguza umaskini; na kwa kuwa Serikali ilibainisha wazi kuwa kuna tatizo kubwa ala ukosefu wa barabara za uhakika na zilizo bora za kusafirisha mazao hayo mjini kwenye masoko makubwa:-

Je, Serikali haioni ni vyema kuanzia sasa ikahakikisha kuwa inatenga kiwango kikubwa cha fedha za barabara kwa ajili ya Mikoa hiyo yenye mazao ya uhakika ili tulikomboe taifa letu katika aibu ya kuomba chakula kila siku?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara inakuabaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba kama ilivyo kwa Mikoa yote, barabara nyingi katika Mikoa yenye mazao ya uhakika bado ni mbovu.

Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS)* imekuwa ikitenga fedha katika Bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya barabara katika Mikoa mbali mbali nchini. Tatizo ni kwamba fedha zinazotengwa ni kidogo ukilinganisha na mahitaji halisi na hali hii inasababishwa na uwezo mdogo wa Serikali kiuchumi. Wizara yangu kwa kushirikiana na TAMISEMI itaendelea kuzifanyia matengenezo barabara hizi kadri Bajeti itakavyoruhusu ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na mazao katika Mikoa hiyo. Hata hivyo, ukiacha fedha za Maendeleo ya ujenzi wa barabara ambazo nyingi hutegemea wafadhili wa nje, Serikali kwa mwaka huu wa fedha 2007/2008 imechukua hatua za makusudi za kuongeza bajeti ya matengenezo ya barabara kutoka shilingi bilioni 67 mwaka jana hadi shilingi bilioni 153 mwaka huu kwa barabara za Kitaifa na za Mikoa na kutoka shilingi bilioni 25 hadi shilingi bilioni 65 kwa barabara zinazohudumiwa na Halmashauri. Hatua hii itasaidia sana katika kukarabati barabara katika maeneo mbali mbali hasa yenye shughuli za kilimo kama Mikoa iliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge.

Aidha, Wizara ya Miundombinu imeandaa Programu ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Uchukuzi *(Transport Sector Investment Program)* inayolenga kuendeleza miundombinu hasa kwenye maeneo yanayoweza kuchochea na kukuza uchumi kwa haraka. Ukizingatia uchumi wetu unategemea kilimo cha mazao ya chakula na biashara, Program hii imelenga Makao Makuu ya Mikoa yote yanaunganishwa kwa barabara za lami ifikapo mwaka 2015 na pia barabara za Mikoa kuimarishwa upesi na hivyo kuweza kupitika kwa urahisi wakati wote ili kuweza kusafirisha mazao, watu na bidhaa nyingine kwa urahisi zaidi. Serikali iko katika hatua ya kutafuta fedha kwa ajii ya kuanza utekelezaji wa Programu hii. Programu hii ni ya miaka kumi na itatekelezwa kwa awamu mbili za miaka mitano mitano kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mhehimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela kwa kujali huduma za wakulima katika Mikoa mingi tu ya nchi yetu bila kuangalia tu eneo analoliwakilisha. Baada ya kusema hayo, ninayo maswali mawii madogo ya nyongeza. Kwa kuwa barabara za kule Same zimejinyonga sana kama nyoka ambazo zinapanda kwenye hiyo milima ambako wakulima ndiko wanakozalisha mazao, zinafanana pia na barabara za Jimbo la Peramiho ambako wananchi wamekuwa wakizitengeneza kwa kutumia Msalagambo yaani umoja wao kwa kuzichimba kwa mikono. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuzisaidia Halmashauri zetu kuwa na mashine za kutengeneza barabara ili kuokoa barabara hizo katika kila kipindi kinachotakiwa na kuwasaidia wakulima hao kusafirisha mazao yao?

Mheshimiwa Spika, la pili; kwa kuwa katika utekelezaji wa programu mbali mbali za Serikali hapa nchini masuala yenye umuhimu wa pekee yamekuwa yakifanyiwa kazi kwa utaratibu maalum kama mpango wa MMES na mapango wa MMEM. Je, Serikali haioni kwamba inatakiwa kutengeneza pia mpango maalum wa mara moja wa kutengeneza barabara za vijijini kwa kiwango kizuri cha kutosha ili wakulima hao waweze kusafirisha mazao yao na kuyafikisha mahali panapotakiwa bila matatizo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu hayo maswali, napenda nimpongeze yeye Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na Mheshimiwa Anne Malecela kwa namna wanavyofuatilia masuala ya Maendeleo na Matengenezo ya barabara nchini pamoja na majimbo yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema kwamba barabara zinahitajika kuboreshwa hasa kwa ajili ya wakulima kwenye maeneo ya milima na hata kwenye mabonde; na kwa maana hiyo Serikali kwa kweli imekuwa ikijitahidi kutenga fedha zake. Lakini, nieleze tu kwamba katika mkakati wa Serikali sasa wa kuwawezesha wakulima na wananchi kujihusisha katika matengenezo ya barabara, Serikali imepania kuhakisha kwamba inaendeleza tekinolojia rahisi ya matengenezo ya barabara na tunacho Chuo kule Mbeya ambacho kinatoa tekinolojia hiyo na sisi katika mwaka huu wa fedha na miaka

inayofuata, tutajitahidi kuhakikisha kwamba wananchi wenyewe na hasa wakulima tunawasaidia kama anavyosema kwa kupata vifaa na mashine ambazo zitakuwa ndio tekinolojia sahihi ya kukarabati barabara ambazo zinaelekea mashambani na kwenye vijiji vyetu. Lakini na Serikali kwa maana ya Wizara ya Miundominu ikishirikiana na TAMISEMI, itawasaidia vile vile katika mkakati huo. Na mpango maalum aliouzungumza ni pamoja na hiyo kwamba ukiacha fedha ambazo zimetengwa hizi ambazo zinatakiwa kwa kweli zielekezwe kwenye barabara mpaka hizi za vijijini, lakini hii tekinolojia rahisi au sahihi ambayo inawahusisha wananchi wenyewe, wakulima wenyewe, itaendelezwa kwa kasi mpya.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Katika swali la Mheshimwa Anne Kilango Malecela, Wilaya ya Kongwa imetajwa kama ni moja ya maeneo ya uzalishaji mkubwa wa mahindi na tunalo Soko la Kimataifa la Kibaigwa. Lakini, Soko lile la Kimataifa la Kibaigwa linaunganishwa na barabara mbovu ya kutoka Mkoa wa Manyara eneo la Dongo kupitia Njoge – Ngomayi – Manyata – Kibaigwa na ya kutoka Wilaya ya Mpwapwa kupitia Chamkoloma – Ndulugumi – Kibaigwa. Mkoa wa Dodoma umependekeza barabara hizi mbili zipandishwe hadhi ili zitoke kuwa barabara za Halmashauri kuwa barabara za Mkoa. Wizara inasema nini hadi sasa kwa ombi hili la Mkoa wa Dodoma?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ule mchakato ambao tumekuwa tukiusema wa kuangalia ama kupandisha au kushusha hadhi za barabara nchini, unaendelea na haujakamilika. Maombi yao ya kupandisha barabara hiyo inayotoka Manyara kwenda Kibaigwa na hiyo inayounganisha Kibaigwa kwenda Mpwapwa, yatazingatiwa katika mchakato huo ili kuona kwamba Je, Vigezo ambavyo vimeainishwa katika sheria mpya ambayo tumepitisha vinakidhiwa na barabara hizi kwa ajili ya kupandishwa ama la.

Na. 343

**Vifaa vya Kupimia Homa ya *RVF***

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kwa kuwa Homa ya Bonde la Ufa inaathiri wanyama na binadamu; na kwa kuwa wakati ugonjwa huo unaingia nchini hapakuwa na vifaa vya kutosha kupimia virusi vya ugonjwa huo na kusababisha Serikali kuingia gharama kubwa kupeleka vipimo nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kununua vifaa vya kupimia virusi vya ugonjwa huo?

(b) Je, mpaka sasa hali ya ugonjwa huo ikoje nchini kwetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA UTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Bura, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa wakati ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa unaingia nchini hatukuwa na vifaa vya kupimia virusi vya ugonjwa huko na hivyo kusababisha Serikali kuingia gharama ya kupeleka vipimo nje ya nchi. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako tukufu kwamba hivi sasa Wizara yangu ipo katika mchakato wa kujengea uwezo Maabara zake tatu ili ziwe na uwezo wa kufanya utambuzi wa awali wa magonjwa ikiwemo Virusi vya Homa ya Bonde la Ufa.

Maabara hizo ni pamoja na Maabara ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Maabara mpya ya kisasa iliyopo katika Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* na Maabara ya Hospitali ya Mkoa wa Arusha ya *Mount* Meru. Vifaa vinavyohitajika vimekwishaainishwa na Maabara hizo zitapatiwa fedha kupitia Mfuko wa Fedha wa Umoja wa Mataifa wa Dharura *(UN Central Emergency Relief Funds)*.

(b)Mheshimiwa Spika, tangu mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa *(RVF)* ulipoanza tarehe 31 Januari hadi jana tarehe 1 Agosti, 2007 jumla ya wagonjwa waliothibitika ilikuwa ni 309 na vifo 144. Mikoa iliyoathirika na ugonjwa huo ni kama ifuatavyo:- Arusha wagonjwa 12 na vifo 3, Dodoma wagonjwa 172 na vifo 93, Iringa wagonjwa 6 na vifo 2, Manyara wagonjwa 6 na vifo 4, Morogoro wagonjwa 54 na vifo 13, Mwanza wagonjwa 5 na vifo 4, Pwani wagonjwa 6 na vifo 2, Singida wagonjwa 47 na vifo 22, Tanga mgonjwa 1 na kifo 1. Mgonjwa wa mwisho alifariki tarehe 17 Julai, 2007 katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma. Kwa sasa hakuna mgonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa aliyeripotiwa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshinmiwa Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Serikali imekubaliana nami kwamba imetumia pesa nyingi kwa kupeleka vipimo katika nchi jirani na kwa kuw kupeleka vipimo huchukua muda mrefu, siyo siku moja wala siku mbili na ndio iliyosababisha wagonjwa wengi kufa hasa katika Mkoa wetu wa Dodoma. Je, Serikali italieleza Bunge hili kwamba mchakato huo utachukua muda gani kukamilika katika Hospitali hizo tatu zilizoteuliwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Je, kuna aina ngapi za virusi vya Homa za Bonde la Ufa, kwa sababu wagonjwa waliougua katika Mkoa wa Dodoma waliugua tofauti na Mikoa mingine. Wagonjwa waliougua katika Mkoa wa Dodoma walikuwa wanapoteza fahamu na kuchanganyikiwa akili. Sasa Waziri atueleze kwamba kuna aina ngapi za virusi vya Homa ya Bonde la ufa ili wananchi waweke tahadhari mapema pindi wanapoona dalili kama hizi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MUUNGANO (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA UTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Spika, vifaa ambavyo tunazungumzia ambavyo vitawekwa katika Maabara tatu nilizozitaja havitachukua muda mrefu kutoka sasa kwa sababu fedha tayari zipo. Kama nilivyosema awali, *United Nations Emergrncy Fund* tayari imeishatoa fedha hizo kwa ajii ya kuleta vifaa pamoja na Shirika la Kimarekani la *CDC* na lenyewe linasaidia *NIMR* ili vifaa hivyo viwekwe haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, nakubaliana na Mheshimiwa Bura kwamba virusi vinaweza vikawa na *strain* tofauti na sitoweza kuwaambia sasa hivi kwamba hii *strain* ya hapa ilikuwa ni *strain* gani kwa sababu vipimo vilivyofanyika ni vya kupima *anti-body*, kuthibitisha tu kwamba ni Homa ya Bonde la Ufa na hatukuangalia kwamba ni virusi vya aina gani. Na ni kweli kwamba mara nyingi ugonjwa huu hujitokeza kwa watu kutokwa na damu sehemu mbali mbali *(Discriminated Intravascular Coagulation (DIC)*. Lakini kwa wagonjwa wa hapa Dodoma ni kweli kwamba walipata matatizo ya mfumo wa fahamu.

Kwa hiyo, inawezekana kwamba *strain* hiyo ilikuwa tofauti, lakini hatutoweza kusema ni aina gani kwa sababu vipimo vilivyofanyika vilipima tu *anti-body* ya kuthibitisha kwamba ni virusi hivyo bila kujua ni *strain* gani. Lakini, bila shaka kwa sababu maabara zetu zinaboreshwa, katika siku za zinazofuata, suala hili linaweza likapatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea kwa sababu tulichukua muda kidogo katika kutambulisha mgeni mashuhuri na pia kuwasilisha taarifa za Kamati. Kwa hiyo, bado tunaendelea. Ila nisema tu kwa wale walioshangaa jinsi Mheshimiwa Waziri, Dr. Mwinyi alivyokuwa anajibu swali, wakumbuke kwamba huyu ni Daktari kamili. (*Makofi*)

Kwa hiyo, bado tunaendelea. Ila niseme tu kwa wale walioshangaa jinsi Dr. Mwinyi alivyokuwa Mheshimiwa Waziri anajibu swali wakumbuke kwamba huyu ni *Professional Medical Officer* (*Makofi*)

Na. 344

**Vyuo vya Maendeleo Nchini.**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia ilipokuwa ikijibu swali langu Na. 59 tarehe 5/2/2007 katika Mkutano wake wa Sita wa Bunge, lililohusu Chuo cha Maendeleo Msingi, ilikiri kuwa, Wizara hiyo inapewa fedha kidogo kila mwaka na kwa kuwa ilikiri pia kuwa, vyote vyote viko kwenye hali mbaya hali inayosababisha waendelee kutengeneza pikipiki za zamani na kununua baiskeli kwa ajili ya wakuu wa vyuo na watumishi wengine.

(a) Kwa kuwa hivi sasa Serikali inavitengeneza na kuvipanua vyuo vya ufundi *VETA*. Je, kwa nini vyuo vya Maendeleo ya wananchi visichukuliwe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya ufundi kwa kuwa ina uwezo na shughuli wanazofanya karibu zinafanana?

(b) Kwa kuwa vyuo vya Maendeleo ni vingi nchini. Je, Serikali haioni kwamba, kwa kuvikabidhi vyuo hivyo kwa Wizara ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi itakuwa imepeleka mambo ya ufundi, Maendeleo, Kilimo na shughuli nyingine za jamii karibu zaidi na wananchi?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inavyo vyuo vya Maendeleo ya wananchi vipatavyo 58 katika Wilaya mbalimbali hapa nchini. Vyuo hivi vilianzishwa kitaifa mwaka 1975 katika Wizara ya Elimu na Utamaduni, wakati huo Elimu ya Watu Wazima ikiwa katika awamu yake ya tatu, na hivyo wahitimu wake wakiwa wamefuta ujinga na wanajua kusoma na kuandika. Kwa namna hiyo madhumuni ya kuanzishwa kwa vyuo hivi yalikuwa ni kuwapatia maarifa na stadi za kazi wananchi waliofuta ujinga wa kusoma, kuandika na kuhesabu ili kuwawezesha kutatua matatizo yanayokabiliwa kwenye mazingira yao ili kujijengea uwezo wa kujitegemea.

Mheshimiwa Spika, vyuo hivi vilianzishwa kwa kurithi majengo na miundombinu ya taasisi mbalimbali zikiwemo vituo vya mafunzo ya ushirika vya mwaka 1964, vituo vya mafunzo ya maendeleo ya vijijini vya mwaka 1962 na shule za kati *(middle schools)* za miaka ya 1950. Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilihamishiwa katika Wizara yangu mwaka 1990 kutoka Wizara ya Elimu na Utamaduni, madhumuni bado yalikuwa ni kuwahudumia wananchi walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara yangu inapewa fedha kidogo kwenye Bajeti yake ya kila mwaka. Hata hivyo kwa fedha hiyo kidogo tunayoipata, tunaendelea kuviboresha vyuo hivi hatua kwa hatua, kwa kuvifanyia ukarabati wa majengo na kuboresha na kuongeza mahitaji muhimu ya mafunzo.

Mheshimiwa Spika, ufumbuzi wa matatizo yaliyopo kwenye Myuo vya Maendeleo ya Wananchi ni kuviwezesha vyuo hivi, kwa kuongeza fedha kwenye Bajeti ya Wizara yangu. Suala la kuvihamishia vyuo hivi kwenda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi linazungumzika, bila ya kuathiri madhumuni ya kuanzishwa kwa vyuo hivi ya kuwapatia maarifa na stadi za kazi wananchi waliofuta ujinga wa kusoma.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kuwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilianzishwa na Serikali kwa madhumuni niliyoyataja hapo juu. Vyuo hivi vinatoa mafunzo yenye mitaala tofauti na vile vya ufundi stadi- *VETA* na vile vile makusudi ya walengwa wa vyuo hivi yanatofautiana. Vyuo hivi (*FDC*) hutoa mafunzo kwa makundi mbalimbali ya wananchi walioko vijijini bila masharti kama yaliyopo *VETA (informal training)*. Masharti yaliyopo *VETA* ni kama vile sifa za elimu ya kuingilia chuoni. Hivyo maandalizi ya kina yanahitajika wakati tukifikiria kuvipeleka Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwenda *VETA* ili kutoa fursa ya kupata mafunzo kwa wananchi wenye viwango vidogo vya elimu, pamoja na uwezo mdogo wa kuchangia gharama za mafunzo yanayotolewa.

(b) Mheshimiwa Spika, lengo kuu la vyuo hivi ni kuwapatia mafunzo mbalimbali ya stadi za maisha ya wananchi walioko vijijini kama Mheshimiwa Mbunge alivyoeleza katika swali lake. Na hivyo kwa makusudi Serikali ilivianzisha vyuo hivyo kwenye maeneo ya vijiji wanakoishi wananchi wengi. Tangu mwaka 1990 hadi sasa Wizara yangu inaendelea kutoa mafunzo ya aina mbalimbali ya stadi za kazi zikiwemo za ufundi, kilimo, ufugaji, ujasiriamali na shughuli zingine kwa wananchi walioko vijijini kwa kutumia rasilimali walizonazo ili wajiletee maendeleo ya endelevu. Aidha, kutokana na maboresho ya elimu nchini katika mpango wa *education sector development programe* ambapo umeleta mafanikio makubwa katika elimu ya msingi na sekondari sasa mpango huo unaelekezwa kwenye elimu ya wananchi na elimu ya ufundi *(Vocational and folk education).* Ni vema vyuo hivi viimarishwe.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Bajeti ya Wizara yake ni ndogo na kwa kuwa Wizara ya Elimu na Ufundi sasa hivi inatengenewa Bajeti kubwa.

(a) Je, Serikali haioni kwamba kupeleka vyuo hivi vya Maendeleo wakati ambapo *VETA* bado inataka kujitanua na kwenda vijijini itakuwa imepunguza mzigo wa upande wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto?

(b) Kwa kuwa ukweli ulioko vyuo hivi vina wanafunzi wachache sana na wananchi wengi hawapeleki wanafunzi wao na maafisa wengi wa Serikali wanazunguka kwenda kutembelea hivi kwa kutumia fedha nyingi. Je, hawaoni kwamba kuliko hawa kuzunguka *VETA* ingefanya kazi bora zaidi yao?

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba kupeleka vyuo hivi *VETA* itapunguzia mzigo Serikali. Ni kweli lakini mpaka sasa tunazungumzia suala hilo mimi na Wizara yangu na Wizara ya Elimu lakini kubwa ni kwamba hata vikipelekwa ni lazima yale ya madhumuni ambayo yalianzishiwa vyuo hivi ni kutoa elimu kwa wale ambao hata hawakupata elimu iweze kuendelea kwa sababu nia kubwa ni kwamba kutoa elimu ya watu ambao siyo *informal* tofauti na *VETA* ambapo *VETA* lazima wawe na kiwango cha elimu na pia ada yake *VETA* ni kubwa. Lakini kwa vyuo hivi vya *FDCs* tunajitahidi kutoa elimu lakini kwa ada ndogo.

Kuhusu swali lake alilozungumzia kwamba ni mzigo mkubwa kwa Serikali ni kweli na pia wanafunzi sio wengi ni kweli hali ya vyuo hivi ni mbaya na haivutii wananchi kupeleka vijana wao katika vyuo hivi na ndiyo tunasema lakini *VETA* tutazungumza nao kuhusu elimu lakini kubwa ni kwamba bado jamii inahitaji kuwa na vyuo hivi. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha swali moja lililobaki la Wizara ya Kilimo, tutaliweka kwenye orodha ya siku nyingine.

Sasa ni matangazo tutaanza na wageni. Mheshimiwa Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Dr. Ibrahim Msabaha anao wageni wafuatao nitawaomba wasimame, kwanza ni Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki ambao ni Waheshimiwa Dr. Didas Massaburi, Mheshimiwa Dr. Said Ghalib Bilali, Mheshimiwa Janet Deo Mmari, Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kabourou, Mheshimiwa Dr. George F. Nangali, Mheshimiwa Dr. Fotnatus Masha, Mheshimiwa S. Kate Kamba, Mheshimiwa S. Nasor na Mheshimiwa Abdallah Ali Hassan Mwinyi. Karibuni sana Waheshimiwa tunafurahi sana kuwaona hili ndio jimbo lenu la Uchaguzi. Kwa hiyo, ni vizuri muwe mnakuja kutusalimia. Karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wengine wa Mheshimiwa Waziri ni kama ifuatavyo: Profesa Samuel Wangwe, aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Shirikisho. Karibu sana na hongera sana kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kuendesha Bodi ya Kibaha. Pia mgeni mwingine ni Ndugu yetu Omar Bendera aliyekuwa Katibu wa Kamati ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki. Karibu sana Mheshimiwa Bendera. (*Makofi*)

Wapo pia kwa kumwunga mkono kama mnavyofahamu Waziri ndio Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini, kwa hiyo kuna Madiwani wanane(8) kutoka Kibaha Vijijini. Naomba Waheshimiwa Madiwani msimame. Nafasi imekosekana wako kwenye *press gallery.* Unajua Kibaha ni karibu sana na Dar es Salaam. Kwa hiyo, watu hawakuzubaa. Waheshimiwa Madiwani walipoona nafasi zimejaa waliweza kuchupa na kuweza na kuingia kwenye *Press Gallery.* Nawapongeza sana Waheshimiwa. Wangekuwa ni wale wa vijijini hovyo hovyo kama ahaa nisitaje. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi wa vyuo vikuu vinne nchini wanaofanya mazoezi Wizarani pale naomba wanafunzi wa vile vyuo vikuu sijui nao wamekosa nafasi. Ahaa wako huku, tena wamekaa miongoni mwa maafisa na ndiyo inastahili. Ndio mazoezi yenyewe nyie mmepatia kabisa. Mtamsaidia Waziri kujibu maswali hapo. Karibuni sana.

Mheshimiwa Mohammed Seif Khatib, Waziri wa Habari na Utamaduni na Michezo ana wageni wake ambao nitawataja tu kwa majina hakusema hawa ni nani yaani wanamhusu nini pengine ni wapiga kura. Ndugu Mzee Rajab Vuai, Ndugu Said Hussein Haji, Ndugu Juma Ramadhan B. Moso, Makame Abdallah Issa na Ndugu Amour Mohamed Chumu, wale pale karibuni sana.

Mheshimiwa Charles Keenja, Mbunge wa Ubungo ametembelewa na wageni ambao wapo kwenye *gallery* ni wenyeviti wote wa CCM wa Kata za Jimbo la Ubungo wakiwemo wanawake wawili na wanaume 8 na msaidizi wa Mbunge. Wale pale wa kutoka Ubungo karibuni sana. Lakini Mheshimiwa Mbunge naona ni watatu siyo wawili ambayo inaongeza uwiano kuwa mzuri zaidi kwa hiyo hongera sana. (*Makofi*)

Kuna jamii ya wafugaji saba kutoka Wilaya ya Kilindi wakiongozwa na Laigwanani Mwarabu, Laigwanani lakini ana jina anaitwa Mwarabu ni wageni wa Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, kweli hawa naona hata Mheshimiwa Waziri Mkuu anapiga makofi kwa bidii sana ingawa ni wageni wa kutoka Kilindi. Hii ndiyo inaonyesha nchi yetu ilivyo nzuri. Mchanganyiko wetu ni mzuri tu si rahisi duniani ukapata mchanganyiko huu wamasai wako Kilindi na wameishi pale mpaka wanachaguliwa kuongoza. (*Makofi*)

Tunao wanafunzi 30 kutoka shule ya Sekondari ya Kikuyu nadhani wale wengine walikuja jana sasa wanakuja kwa awamu. Naomba wanafunzi wa Sekondari ya Kikuyu pamoja na walimu msimame pale mlipo. Ahsante sana karibuni. Wapo pia wanafunzi 42 kutoka shule ya msingi Kizota wasimame pamoja na Walimu wale wa Kizota. Ahsante sana karibuni sana. Wapo wanafunzi 12 na wageni saba kutoka *DC Jubilee High School Dodoma* pamoja na walimu pengine wamekosa nafasi. Ahsante.

Mheshimiwa Kyendesya, Mbunge wa Viti maalum Mbeya, anao wageni watatu ambao ni Bashiru Madaru, Mwenyekiti wa Vijana CCM Mbeya yule pale, Ndugu Saad Kusilawe, Katibu wa Vijana Mbeya na Barnaba Esau, Katibu wa Vijana Mkoa wa Mwanza. Kwa wale wenzetu mnaogombea *NEC* hawa ni watu muhimu sana. Lakini labda nina hakika mmekwisha waona hawa. (*Makofi*)

Mikutano, Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, anaomba wajumbe wote wa Kamati hiyo ya hesabu za Serikali wakutane saa tano Asubuhi ya leo chumba Na. 231 jengo la utawala.

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anasema kutakuwa na kikao cha pamoja cha Kamati nne zifuatazo:- Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Kamati ya Huduma za Jamii, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Ulinzi na Usalama na Kikao hicho pia kitawahusisha wajumbe wate wa Umoja wa Wabunge Wanawake na kitafanyika saa saba na nusu mchana leo katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Kwa hiyo, katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa saba na nusu hadi saa kumi na nusu. Inaonekana ni kikao kirefu na cha muhimu. Kwa hiyo, Kamati hizo nne za Maendeleo ya Jamii, Huduma za Jamii, Katiba, Sheria na Utawala, Ulinzi na Usalama na Wajumbe wote wa *TWPG* (Umoja wa Wabunge wanawake) saa saba na nusu Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa William Lukuvi anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo hii saa nane mchana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano atazindua mradi wa tunajali wa huduma kwa watu wenye virusi vya Ukimwi katika viwanja vya Mwalimu Nyerere *(Nyerere Square)* Mjini pale. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge tujitokeze kwa wingi katika tukio hili ambapo wananchi wamealikwa kwa wingi na tuweze tukasikilize mradi huu wa kuwahudumia walioathirika ambao ni muhimu sana katika jamii yetu. Kwa hiyo, ni saa nane pale Viwanja vya Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Job Ndugai, Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, anahitaji wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo saa saba mchana ukumbi namba 432. Mheshimiwa Abdallah Kigoda Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anaomba wajumbe wote wa kamati ya Fedha na Uchumi wakutane saa saba mchana katika ukumbi 219 ghorofa ya pili jengo la Utawala. Napenda kukumbusha tu jana jioni alitangaza Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mkutano mfupi lakini muhimu sana leo wa Kamati ya Uongozi ya Bunge *(Steering Committee)* saa saba kule ofisini kwangu, katika ukumbi wa Mikutano Wenyeviti wote. Sasa naona Wenyeviti wengi wametangaza mikutano. Kwa hiyo, naomba sana wawaachie makamu Wenyeviti waanze sisi tutakapomaliza ndiyo waende kule hatukai muda mrefu. Kwa hiyo, *Steering Committee* saa saba kamili mchana ukumbi wa Spika.

Baada ya hapo Waheshimiwa Wabunge, namwomba sasa Mwenyekiti Job Ndugai, kwa kuwa nina wageni aje hapa ili aweze kuendeleza na shughuli zilizosalia kwa leo.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2007/2008
### Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai mimi na familia yangu na kwa kuniruzuku rehema mbalimbali hadi kufika siku hii ya leo.

Aidha, namshukuru Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani aliyokuwa nayo kwangu kwa kunikabidhi dhamana ya kuiongoza Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki inayosimamia ushiriki wa Watanzania katika mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naomba pia uniruhusu kuwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Uchaguzi la Kibaha Vijijini kwa kuniwezesha kufika hapa nilipo na kwa uvumilivu wao pale wanapokosa kuniona kutokana na majukumu ya kitaifa. Nawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi hii kuwapongeza Watanzania wote walioteuliwa katika mashirika ya Kimataifa; nikianza na Mheshimiwa Dr. Asha-Rose Migiro aliyeteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa; Dkt. William Shija kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Mabunge ya Umoja wa Madola na Balozi Liberatta Mulamula, kwa kuteuliwa kuwa Mtendaji Mkuu wa kwanza wa Sekretariati ya Maziwa Makuu. Aidha, uniruhusu pia nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kujiunga na Bunge la Afrika Mashariki wakijumuisha Mheshimiwa Dr. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dr. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Janeth Deo Mmari, Mheshimiwa Dr. Aman Walid Kabourou, Mhe. Dr. George Francis Nangale, Mheshimiwa Dr. Fortunatus Lwanyatika Masha, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba, Mheshimiwa Sebtuu Nassor na Mheshimiwa Abdallah Ally Hassan Mwinyi. Nampongeza pia Mbunge mpya wa Jimbo la Tunduru Mhe. Mtutura Abdalalah Mtutura.

Aidha, nawapongeza Mhe. Bernard Membe, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mhe. Dkt. Batilda Salha Burian, kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Masuala ya Bunge, Mhe. Gaudence Kayombo, kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji. Hali kadhalika nampongeza Mheshimiwa William Ngeleja, kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Nishati na Madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuungana na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wenzangu walionitangulia kutoa salamu za rambirambi kutokana na kifo cha Mhe.Juma Jamaldin Akukweti, aliyekuwa Mbunge na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Mhe. Amina Chifupa Mpakanjia aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum CCM Vijana. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote hao mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salaam za pongezi na rambirambi naomba sasa nimshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa hotuba yake aliyoitoa yenye taarifa muhimu kuhusu hali ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya Serikali kwa mwaka 2006/2007 na mwelekeo wa Serikali katika mwaka wa fedha 2007/2008. Aidha, namshukuru Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakhia Meghji kwa hotuba zao zilizonisaidia sana kuweka mwelekeo wa shughuli za Wizara yangu na kuboresha maudhui ya hotuba yangu hii. Vilevile, napenda kuwapongeza Mawaziri wote walionitangulia kuwasilisha hoja za Wizara zao katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje chini ya Mwenyekiti wake Mashuhuri, Mheshimiwa Anna Abdalah,

Mbunge wa Viti Maalum CCM, kwa busara, ushauri, maoni na maelekezo yaliyowezesha kuboresha Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2007/2008. Aidha, hoja zao zenye busara walizozitoa katika Semina iliyoandaliwa na Wizara yangu mwezi Machi, 2007, ziliongeza chachu ya kuboresha ufanisi katika ufanikishaji wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Majukumu ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jukumu kuu la Wizara yangu ni kuhakikisha Tanzania inanufaika kikamilifu kutokana na ushiriki wake katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya za kikanda ni sehemu ya Sera yetu ya Mambo ya Nchi za Nje na Mkakati wa Serikali kuimarisha ushirikiano mwema na majirani zetu na mauzo ya bidhaa nchi za nje. Katika kufanikisha jukumu hilo Serikali iliunda Wizara maalum ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ajili ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (*Treaty*) na Itifaki zake (*Protocols*) pamoja na Programu mbalimbali za Ushirikiano.

Aidha, Wizara inasimamia na kuratibu ushiriki wa wadau mbalimbali katika taasisi za umma na za binafsi pamoja na wananchi wote wa Tanzania katika kutumia fursa za masoko na uwekezaji zilizomo katika nyanja zote za Ushirikiano kwenye Jumuiya. Kwa hiyo utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulizingatia sana azma hii ya kitaifa ya kukuza na kuimarisha mauzo nje na vilevile kudumisha ushirikiano wa Kiuchumi na Kijamii katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo Mkakati ya Wizara *(Strategic Objectives)* Malengo Mkakati ya Wizara ambayo yameainishwa katika Mpango Mkakati wa Wizara *(Ministerial Strategic Plan 2007 – 2010)* ukiwa ndio mwongozo wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara, yanajumuisha yafuatayo:-

(i) Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kama mojawapo ya Kanda za ushirikiano na Taasisi za kimataifa ambazo Tanzania ni muasisi wake;

(ii) Kuratibu na kuwezesha ushiriki wa wadau hususan sekta binafsi na wananchi kwa ujumla ili Taifa linufaike;

(iii) Kufanikisha majukumu yake kwa kuzingatia usimamizi bora wa matumizi ya fedha na uwajibikaji kwa mali ya umma kwa ujumla;

(iv) Kujenga uwezo wa utendaji kazi katika Wizara na rasilimali watu kwa kuongeza ujuzi na vitendea kazi kwa lengo la kuongeza tija katika utoaji wa huduma; na

(v) Kushiriki kikamilifu katika kuchangia jitihada za kitaifa za kupambana na majanga ya kitaifa na dunia nzima hususan kupunguza maambukizi ya UKIMWI na kutoa huduma bora kwa walioathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera na mikakati ya Wizara katika kutimiza malengo ya ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara yangu inaongozwa na Sera na Mikakati ifuatayo:-

(i) Kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Umoja wa Forodha unakuwa chachu na nguzo muhimu katika kujenga uwezo na imani ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kuelekea kwenye ushirikiano mpana na wa kina zaidi katika siku za usoni;

(ii) Ujumuishaji wa wadau wote wa taasisi za umma na za binafsi katika ubainishaji na utekelezaji wa programu za ushirikiano;

(iii) Matumizi kamilifu ya fursa za soko kubwa la watu takriban milioni 120 zilizojitokeza katika Programu za Ushirikiano kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kukuza na kuendeleza mauzo ya ndani ya Afrika Mashariki na ya nje;

(iv) Kuhimiza utekelezaji wa matakwa ya Aya ya 112 ya Sheria ya Usimamizi wa Masuala ya Forodha ya mwaka 2004 ya Jumuiya na marekebisho yake. Aya hiyo inazitaka Nchi Wanachama kama kundi moja kukamilisha mikataba ya ushirikiano baina ya Jumuiya na kanda nyingine za kiuchumi hususan *SADC* na *COMESA* ifikapo Desemba, 2008. Hatua hii inakusudia kuhuisha ushiriki wa Nchi Wanachama katika

(vi) Uimarishaji wa uwezo wa Wizara kiutendaji.

Utekelezaji wa Programu zilizopangwa, Katika Mwaka 2006/2007, kutokana na Malengo Mkakati ya Wizara pamoja na Sera na Mikakati niliyoitaja, Wizara imeendelea kuchukua na kutekeleza hatua mbalimbali za kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya, kuratibu na kuwezesha wananchi na sekta binafsi katika mchakato huu.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kushauriana na kushirikisha wadau wote katika majadiliano ya kikanda, kutoa elimu kuhusu Jumuiya na kutangaza fursa za masoko zilizojitokeza na changamoto zake, kurahisisha taratibu za forodha kwa kuzitafsiri katika lugha ya Kiswahili, kutoa mafunzo pamoja na kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa vikwazo vya kibiashara.

Aidha, Wizara ilifanikisha kuwepo kwa Mkakati wa Kikanda wa Kuimarisha Sekta Binafsi. Utekelezaji wa hatua hizo uliambatana na uhimizaji wa matumizi bora ya rasilimali zilizopo kwa kuzingatia sheria na taratibu za fedha na manunuzi pamoja na uboreshaji wa tija katika utekelezaji wa kazi mbalimbali. Aidha, Wizara iliendelea kujenga uwezo wake wa utendaji kama itakavyoelezwa hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2006/2007 masuala muhimu yaliyojitokeza ni pamoja na kukamilika kwa Mchakato wa kupata maoni ya wananchi kuhusu hoja ya kuharakisha uundaji wa Shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki; upanuzi wa Jumuiya kwa kuziingiza nchi za Rwanda na Burundi; kuimarisha Mahakama ya Jumuiya na Uwezo wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki; kukamilisha maandalizi ya Mkakati wa Tatu wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2006 –

2010; kuendelea na Utekelezaji wa Umoja wa Forodha; kuanza Maandalizi ya Majadiliano ya Soko la Pamoja na Kuimarisha Uwezo wa Wizara Kiutendaji. Aidha, Viongozi Wakuu wa Jumuiya katika kipindi hicho walifanya maamuzi kadhaa yanayohitaji utekelezaji au ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji wa Maoni ya Wananchi Kuhusu Kuharakisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki, Kifungu cha 5(2) cha Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kimeainisha hatua za mtangamano *(Integration Process)* za Afrika Mashariki. Hatua ya mwanzo ya Mtangamano wa Afrika Mashariki ni Umoja wa Forodha, ikifuatiwa na Soko la Pamoja, Sarafu Moja na hatimaye Shirikisho la Kisiasa. Utekelezaji wa Umoja wa Forodha unahusu masuala yafuatayo ya msingi:-

(a) Kuondoa vikwazo vya kibiashara baina ya Nchi Wanachama hususan kuondoa Ushuru wa Forodha;

(b) Kuweka wigo wa pamoja wa Ushuru wa Forodha kwa bidhaa zitokazo nje ya Jumuiya *(Common External Tariff)* ; na

(c) Kutunga na kutekeleza sheria moja ya forodha *(Common Customs Law).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Umoja wa Forodha ulianza mwaka 2005 na una kipindi cha mpito cha miaka mitano. Kwa hiyo, ifikapo mwaka 2010, Jumuiya ya Afrika Mashariki itakuwa ni Umoja wa Forodha uliokamili kwa sababu bidhaa zitokazo miongoni mwa wanachama hazitatozwa Ushuru waForodha, wigo na sheria ya pamoja ya forodha itakuwa imeimarika. Kwa maana hiyo, ushindani wa kibiashara katika soko la ndani utaongezeka. Kwa hiyo, kati ya sasa na muda huo utakapofika ni budi wazalishaji na wafanyabiashara wetu waongeze bidii katika kuongeza tija ili waweze kukabiliana na ushindani utakaojitokeza na wakati huo huo kutumia kikamilifu fursa za soko la Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Forodha unahusu ushirikiano katika nyanja za kiuchumi pekee hususan biashara. Soko la Pamoja linaongeza wigo wa ushirikiano kwa kujumuisha masuala ya kiuchumi na kijamii mathalani ulegezaji wa masharti yahusuyo ajira, mitaji, utoaji huduma na uhamiaji miongoni mwa nchi wanachama *(free movement of labour, capital, services, right of establishment and residence).* Hatua ya Sarafu Moja huimarisha ushirikiano wa kiuchumi kwa kusisitiza uhuishaji wa sera za kodi na fedha miongoni mwa Nchi Wanachama. Hatua ya mwisho ambayo ni Shirikisho la Kisiasa, hulenga katika kuunda dola moja itakayosimamia masuala yote ya Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa. Kwa maana hiyo, utaifa wa Nchi Wanachama hutoweka na badala yake Serikali moja ya Shirikisho huundwa. Mheshimiwa Spika, nimetumia fursa hii kuelezea kwa ufupi hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili Waheshimiwa Wabunge waweze kuelewa maudhui ya zoezi la kukusanya maoni ya wananchi kuhusu hoja ya kuharakisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za mtangamano nilizozieleza zimeainishwa katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hata hivyo, Mkataba haujabainisha muda wa kufikia hatua zilizosalia za mtangamano, yaani Soko la Pamoja, Sarafu Moja

na hatimaye Shirikisho la Kisiasa. Ni kwa mantiki hiyo, Viongozi Wakuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wakijumuisha Marais wa Kenya, Uganda na Tanzania katika Mkutano wao Maalum uliofanyika tarehe 28-29 Agosti, 2004 Jijini Nairobi, Kenya, waliazimia kuangalia uwezekano wa kuharakisha hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kusudi hatua ya Shirikisho la Kisiasa iweze kufikiwa katika muda mfupi kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viongozi Wakuu wa Jumuiya waliunda Kamati ya Wajumbe wawili kutoka katika kila Nchi Mwanachama, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Amos Wako, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Kenya akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti Prof. Haidari Amani aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Uchumi na Masuala ya Jamii (*ESRF*). Katibu wa Kamati alikuwa Dr. Ezra Suruma kutoka Uganda. Kamati iliwasilisha Taarifa yake katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya uliofanyika tarehe 26 Novemba, 2004 Jijini Arusha. Taarifa ya Kamati hiyo ilipitiwa na kujadiliwa na wadau mbalimbali katika Nchi Wanachama. Uchambuzi wa Taarifa hiyo ulibainisha mapendekezo yaliyowasilishwa katika Mkutano wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya uliofanyika tarehe 29 na 30 Mei, 2005 Jijini Dar es Salaam. Mkutano huo uliagiza kuwa wananchi wapewe fursa ya kutoa maoni yao kuhusu hoja ya kuharakisha Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki. Mheshimiwa Spika, lengo la kushirikisha wananchi kikamilifu ni kuzingatia Kifungu cha 7 cha Mkataba wa Jumuiya kinachotaka wananchi washirikishwe *(People Centred)* katika mchakato wa kuamua Mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13 Septemba, 2006, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliteua Kamati ya Kitaifa iliyojumuisha Wajumbe 15 na Sekretarieti ya watu watatu. Wajumbe wa Kamati walitoka katika Sekta ya Umma na Binafsi wakiwemo Waheshimwa Wabunge na Wawakilishi, Wazee Mashuhuri, Taasisi za Wafanyabiashara na Makundi ya Kijamii. Mheshimiwa Rais, aliizindua rasmi Kamati ya Kitaifa tarehe 13 Oktoba, 2006 siku ambayo Kamati za Kitaifa za Uganda na Kenya pia zilizinduliwa. Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Watanzania toka nyanja mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa katika Kamati hii ulisaidia sana kuwahamasisha wananchi kutoa maoni yao bila woga na hivyo kuleta mjadala mpana na wenye tija kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wananchi walijitokeza kwa wingi kutoa maoni yao na napenda kutamka kuwa zoezi hili lilifanikiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilisimamia na kuratibu zoezi la ukusanyaji wa maoni ya wananchi kuhusu Shirikisho katika Mikoa na Wilaya zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zoezi hili lilifanyika kwa mfumo wa kugawanya Nchi nzima katika Kanda ili kuiwezesha Kamati kujigawa katika makundi kuiwezesha kufikia maeneo yote ya nchi yetu kwa wakati muafaka kulingana na ratiba iliyopangwa kwa zoezi hili. Nchi iligawanywa katika Kanda zifuatazo:-

(i) Kanda ya Mkoa wa Dar es Salaam;(ii)Kanda ya Ziwa (Mwanza, Kagera, Mara, Arusha na Manyara);

(iii) Kanda ya Magharibi (Kigoma, Tabora, Shinyanga, Singida na Dodoma);

(iv) Kanda ya Pwani (Mtwara, Lindi, Pwani, Tanga na Kilimanjaro);(v)Kanda ya Kusini (Ruvuma, Mbeya, Rukwa, Iringa na Morogoro); na(vi)Kanda ya Zanzibar (Unguja na Pemba).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Januari, 2007 Kamati ilipata maoni ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Aidha, Mwezi Aprili, 2007 Kamati ilikuwa na fursa ya kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa Bunge lako hapa Mjini Dodoma kwa lengo la kupata maoni yao.

Mwezi Mei, 2007 Kamati ilikutana na Viongozi wastaafu Tanzania Bara na Zanzibar. Kamati ilikamilisha zoezi hili na kuwasilisha Taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 13 Julai, 2007 Ikulu, Jijini Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, kazi ya Kamati haikuwa rahisi lakini wajumbe waliifanya kwa moyo na uvumilivu mkubwa. Kwa niaba ya Serikali napenda kuishukuru Kamati ya Kukusanya maoni iliyoongozwa na Mwenyekiti wake, Profesa Samweli Wangwe. Kamati imefanya Kazi nzuri na yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio katika kuendesha na kusimamia zoezi la kupata maoni ya wananchi kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki ni matokeo ya ushirikiano ambao Wizara iliupata kutoka kwa Viongozi wote ikijumuisha miongozo madhubuti kutoka kwa Mheshimiwa Rais mwenyewe na pia viongozi wengine wakiwemo Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri wenzangu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Watendaji, Wafanyakazi na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Viongozi wote hao kwa kufanikisha zoezi hili. Aidha, naomba kutoa shukurani za pekee kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya; Waheshimiwa Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi; Vyombo vya Habari na Wananchi kwa ujumla kwa kushiriki kikamilifu katika Mchakato huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia mbalimbali zilitumika kukusanya maoni ili kuwafikia wananchi wengi kadri iwezekanavyo. Njia zilizotumika kukusanya maoni ni pamoja na Mikutano ya hadhara, madodoso, magazeti, radio, televisheni, tovuti na barua. Jumla ya Wananchi 18,321 walitoa maoni katika zoezi hili kwa kutumia njia hizo kwa mtindo wa uwakilishi yaani *sampling*.

Mfumo huu uliwezesha kupata maoni ya wananchi toka mijini, vijijini na nje ya nchi na hivyo kupanua wigo wa kidemokrasia katika kutoa maoni. Kwa hiyo maoni yatokanayo na zoezi hili ni maoni ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Kamati ya Kitaifa ya Kukusanya Maoni ya Wananchi kuhusu kuharakisha Shirikisho imejumuisha maoni ya wananchi wa Tanzania Bara na Zanzibar. Kati ya wananchi waliotoa maoni asilimia 75.9 ya wananchi wanataka uundaji wa Shirikisho usiharakishwe na asilimia 20.8 wanataka uharakishwe wakati asilimia 3.3 hawataki Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walitoa sababu kadhaa kukataa hoja ya kuharakisha Shirikisho; kwanza ni sababu za kisiasa na pili ni sababu za kiuchumi na kijamii. Kwa upande wa kisiasa, wananchi wengi walihoji hali ya kisiasa ya Afrika Mashariki kwa misingi mitano mikuu ikijumuisha: elimu na ufahamu mdogo juu ya Jumuiya na Shirikisho; demokrasia na utawala bora; Muungano kati ya Tanganyika na Zanzibar; ulinzi na usalama na tofauti za kiitikadi. Wananchi walieleza kuwa hawajui faida na hasara za Shirikisho na hivyo wanahitaji muda kuelimishwa na kujiridhisha juu ya faida zake. Kuhusu Demokrasia na Utawala Bora, walieleza kuwa hali ya utawala wa Kikatiba na Kisheria Afrika Mashariki bado ni changa na hairidhishi.

Vile vile, walieleza kuwa hali ya ulinzi na usalama katika nchi jirani zinazoizunguka Tanzania upande wa Kaskazini na Magharibi bado ni tete sana. Suala la tofauti za kiitikadi lilijitokeza pia.

Kwa hiyo, wananchi walieleza kuwa si wakati muafaka kuharakisha kuunda Shirikisho katika mazingira haya. Kwa upande wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii wananchi wengi wanataka masuala matano yafuatayo yazingatiwe kikamilifu; tofauti ya maendeleo ya kiuchumi; uwezo wa ushindani kibiashara na katika soko la ajira; kujenga misingi imara ya kiuchumi pamoja na umiliki wa ardhi na maliasili nyingine.

Wananchi wengi wasiokubaliana na wazo la kuharakisha Shirikisho walieleza kuwa tofauti za kiuchumi zilizopo baina ya Nchi Wanachama zitasababisha nchi dhaifu kumezwa au kutofaidika na Shirikisho. Walieleza kuwa Tanzania haijajenga uwezo wa ushindani katika soko la bidhaa za viwandani na ajira; sekta binafsi ikiwa ni pamoja na ujasiriliamali bado ni changa sana na kwamba tofauti za milki za ardhi zitasababisha Watanzania kuporwa au kunyang'anywa ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, Watanzania walio wengi wanataka uanzishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki usiharakishwe kwa sababu wanaamini kwamba muda uliopo kati ya sasa hadi mwaka 2013 hautoshi kuondoa kero na hofu nilizozitaja awali.

Aidha, wananchi walio wengi wameshauri kuwa msisitizo zaidi uwekwe kwenye kuimarisha uchumi ambao matokeo yake ni kuweka misingi imara ya kuingia kwenye Shirikisho la Kisiasa. Wakati akipokea Taarifa ya Kamati, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliwahakikishia kuwa maoni ya wananchi yatazingatiwa.

Napenda kutumia fursa hii kurejea Tamko la Mheshimiwa Rais kuwa Serikali itaifanyia kazi Taarifa ya Kamati ya Profesa Wangwe na maoni ya wananchi yatazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la kukusanya maoni ya wananchi limetoa mafunzo mengi kwa Wizara yangu na kwa Taifa. Kwanza, zoezi hili limeonyesha kuwa wananchi wakishirikishwa kikamilifu ni chemchem nzuri ya mawazo na ushauri katika kuendeleza nchi yetu.

Pili, tumeweza kujua uwezo na udhaifu wetu katika ushirikiano wa kikanda na jinsi ya kujipanga kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia kwa makini hoja na dukuduku za wananchi, ikiwa ni pamoja na vikwazo vinavyowapelekea kushindwa kufaidika na fursa za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki itachukua hatua za makusudi kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi nyingine kuhakikisha kwamba yale yote yaliyo ndani ya uwezo wake yanapatiwa ufumbuzi thabiti. Kwa kuanzia, suala la kutoa elimu kuhusu Jumuiya kwa wananchi litapewa kipaumbele.

Sambamba na hilo, Wizara pia inaangalia uwezekano wa kuhakikisha kwamba nyaraka zote za maamuzi, mikataba, na machapisho mbalimbali yanayohusu ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki yanatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na kusambazwa hadi ngazi za vijiji ili wananchi walio wengi waweze kusoma na kuelewa fursa mbalimbali zilizopo. Kazi hii ni kubwa na ili kila Mtanzania aweze kufikiwa kiasi kikubwa cha rasilimali kinahitajika. Kwa hiyo, tutaitekeleza kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujiunga kwa Rwanda na Burundi katika Jumuiya, katika kipindi hiki cha mwaka mmoja, Jumuiya imeongezeka toka nchi tatu hadi tano baada ya nchi za Rwanda na Burundi kujiunga. Nchi za Rwanda na Burundi ziliwasilisha maombi ya kujiunga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1996. Wakati huo Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikuwa katika hatua za awali kabisa za kufufua Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwa hiyo nchi hizi ziliombwa kusubiri hadi hapo Jumuiya ya Afrika Mashariki itakapoanza kutekeleza Umoja wa Forodha. Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuanza kushughulikia maombi ya nchi za Rwanda na Burundi ulianza baada ya kuanza kutekeleza Umoja wa Forodha mwaka 2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi Wanachama ziliandaa vigezo maalum vya kutathmini maombi ya nchi zitakazotaka kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki vilivyooneshwa katika Jedwali Na. 1. Vigezo ambavyo sharti nchi muombaji ivifikie ili ikubaliwe kuwa mwanachama vimegawanywa katika sehemu kuu mbili; Sehemu ya kwanza ni vigezo vya kupima mambo yaliyoainishwa katika Mkataba wa Jumuiya na Itifaki zake.

Vigezo hivyo ni pamoja na nchi inayoomba kuridhia Mkataba wa Jumuiya na misingi yake hususan utekelezaji wa demokrasia, utawala bora, uwezo wa kutoa michango ya kuendeshea Jumuiya pamoja na kushirikiana na Nchi Wanachama katika kudumisha amani na ujirani mwema. Sehemu ya Pili ilikusudia kupima uwezo wa Rwanda na Burundi katika kutekeleza miradi na programu za maendeleo. Sehemu hii ilihusu kupima uwezo wa nchi hizo kushiriki kwa hali na mali katika maeneo ya sekta za ushirikiano mathalani kilimo, mazingira, elimu, utamaduni, masuala ya jinsia, afya, na sekta binafsi. Katika kupitisha vigezo vilivyotajwa, Vifungu muhimu vya Mkataba wa kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki vilizingatiwa hususan Kifungu Na.3 ambacho kinaainisha masharti ya kutimiza kwa nchi inayoomba kuwa mwanachama wa Jumuiya.

Aidha, vigezo vilizingatia Kifungu Na. 5 ambacho kinaainisha madhumuni ya Jumuiya pamoja na Kifungu Na. 6 ambacho kinatilia mkazo utawala bora ukijumuisha demokrasia, utawala wa sheria, na haki za binadamu pamoja na usawa wa jinsia. Majadiliano ya kina yalizinduliwa mwezi Julai, 2006 na kufanyika katika ngazi ya Wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri ili kuzingatia masuala ya nyanja zote za ushirikiano, yaani kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano katika ngazi ya Mawaziri kati ya Jumuiya na nchi za Rwanda na Burundi mwaka huu, 2007 yalisimamiwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri la Jumuiya Mhe. Eriya Kategaya wa Uganda. Aidha, nilipata fursa ya kuongoza ujumbe wa Afrika Mashariki katika majadiliano hayo. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Mawaziri wenzangu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa imani waliyokuwa nayo kwa Tanzania na kwangu binafsi kwa kunipa nafasi ya kuongoza ujumbe wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* katika majadiliano ya Rwanda na Burundi. Mheshimiwa Spika, msingi mkuu wa majadiliano ulikuwa ni kulinda maslahi ya pande zote zilizohusika katika mchakato huu hususan kuimarisha mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Nchi Wanachama waliziingiza nchi za Rwanda na Burundi katika Jumuiya baada ya kuridhika na utekelezaji wa vigezo vilivyowekwa na Jumuiya. Mkataba wa kujiunga *(Accession Treaty)* ulisainiwa katika Mkutano wa kilele wa Viongozi Wakuu wa Jumuiya uliofanyika Jijini Kampala, Uganda tarehe 18 Juni, 2007. Mkataba huo una vipengele mahsusi kuhusu Tanzania ikiwa ni pamoja na Kifungu Na. 4 kinachozitaka nchi za Rwanda na Burundi kupunguza ushuru wa forodha kwa asilimia 80 (80%) kwa bidhaa zetu ziingiapo katika nchi hizo na halikadhalika bidhaa zao ziingiapo Tanzania .

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania imekuwa na uhusiano wa kibiashara wa muda mrefu baina yake na nchi za Rwanda na Burundi. Kwa hiyo kujiunga kwa Rwanda na Burundi katika Jumuiya kutainufaisha Tanzania Kibiashara, kwa sababu kujiunga kwao kutaendeleza fursa za kibiashara kwa wafanyabiashara wetu. Rwanda na Burundi ni miongoni mwa nchi chache ambazo kwa kipindi kirefu Tanzania imekuwa ikiuza bidhaa nyingi zaidi ikilinganishwa na manunuzi. Kwa mfano, kati ya mwaka 1999 hadi 2006 Tanzania iliuza nchini Rwanda bidhaa za thamani ya Dola za Kimarekani 20 Milioni na manunuzi yalikuwa Dola za Kimarekani 1.2 Milioni.

Aidha, Tanzania iliuza nchini Burundi bidhaa za Dola za Kimarekani 46.6 Milioni na kununua bidhaa za thamani ya Dola za Kimarekani 0.8 Milioni. Jedwali Na. 2 linatoa mtiririko wa manunuzi na mauzo baina ya Tanzania na nchi za Rwanda na Burundi. Aidha, Jumuiya itanufaika kutokana na kupanuka kwa soko lake toka watu takribani 90 Milioni hadi 120 Milioni. Ukubwa huu wa soko utaipa Jumuiya sauti kubwa katika majadiliano ya Kimataifa.

Mhe shimiwa Mwenyekiti, Mkakati wa tatu wa Maendeleo wa Jumuiya (2006-2010) Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinatambua kwamba lengo kuu la Ushirikiano ni kuunganisha juhudi za kupiga vita umaskini katika Nchi Wanachama. Mkakati wa Tatu wa Maendeleo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wa 2006 - 2010 umeainisha maeneo ya msingi katika kila sekta na jinsi yatakavyoshughulikiwa katika kupambana na umaskini. Baadhi ya maeneo hayo ni uendelezaji wa miundombinu, viwanda na kilimo. Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni ya Mkakati huu ni kusaidia *(complement)* mipango ya ndani ya maendeleo ambayo nchi moja moja peke yake isingeweza kutekeleza au utekelezaji wake ungechukua muda mrefu kutokana na ufinyu wa Bajeti. Kwa hiyo Mkakati huu unaziwezesha Nchi Wanachama kuweka nguvu zao pamoja na hivyo kufanikisha malengo kwa haraka zaidi. Kutokana na Mkakati huu tayari Tanzania imenufaika katika utekelezaji wa miradi ya ushirikiano hususan miundombinu ambayo nitaielezea kwa ufupi baadaye.

Uimarishaji wa Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sekretarieti ya Jumuiya imeimarishwa kwa kuongezewa Watumishi na vitendea kazi. Jumla ya Wataalam 38 wakiwemo Wataalam 13 kutoka Kenya, 12 kutoka Uganda na 13 kutoka Tanzania waliajiriwa katika mwaka 2006/2007. Aidha, idadi ya Wafanyakazi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa hivi sasa imefikia 142; wakijumuisha 34 kutoka Uganda, 41 kutoka Kenya na 67 kutoka Tanzania, kama mchanganuo unavyoonyesha katika Jedwali Na 3. Mfumo wa ajira katika Jumuiya unazingatia usawa kwa kadri iwezekanavyo katika kugawa nafasi zilizopo. Aidha, katika kada za kawaida za wafanyakazi, misingi ya ajira inafuata sheria na taratibu zilizopo nchini na ndiyo maana mtaona Watanzania ni wengi zaidi. Mheshimiwa Spika, napenda kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali itaendelea kuwa makini katika suala la ajira katika Jumuiya ili Watanzania wenye sifa wapate fursa sawa katika kupata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, maandalizi ya Ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yanaendelea vizuri. Serikali ya Tanzania ilitoa eneo la ekari kumi (10) kwa ajili ya ujenzi huo Jijini Arusha. Aidha, Serikali ya Ujerumani ilitoa kiasi cha fedha *'Euro'* milioni nane kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Jumuiya. Mkandarasi amekwishapatikana. Hatua zilizosalia ni ukamilishaji wa vipengele vyote vya michoro ya jengo ambapo maandalizi ya vifaa na ujenzi yanatarajiwa kuanza mwezi Machi 2008. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hatimaye imepata Bunge la Awamu ya pili. Spika wa Bunge hilo sasa ni Mheshimiwa Abdirahin Haithar Abdi kutoka Kenya. Naomba kutumia fursa hii kumpongeza Spika mpya kwa kuchaguliwa kuliongoza Bunge la Afrika Mashariki. Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Abdulrahman Kinana, Spika aliyemaliza muda wake kwa kazi nzuri na

kuiletea sifa Tanzania kwa uongozi wake makini. Bunge la Afrika Mashariki limeweka Kalenda ya Vikao na Miswada ya kuishughulikia katika mwaka 2007/2008. Miswada hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Muswada wa Usafirishaji katika Ziwa Victoria;

(ii) Muswada wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria;

(iii) Muswada kuhusu Kukasimisha Madaraka na Majukumu ya Wakuu wa Nchi Wanachama;

(iv) Muswada kuhusu Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Forodha katika Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(v) Muswada kuhusu Mapato na Matumizi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vi) Muswada wa kuhusu Nyongeza ya Mapato na Matumizi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(vii) Muswada kuhusu Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia ya Afrika Mashariki;

(viii) Muswada kuhusu Wakala wa Usalama na Usimamizi wa Anga Afrika Mashariki;

(ix) Muswada kuhusu Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki; na

(x) Muswada kuhusu Kamisheni ya Utafiti wa Afya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada hiyo inakusudia kuweka sheria na taratibu za kusimamia masuala ya ushirikiano yaliyomo katika Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na hivyo itasaidia katika kuimarisha mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mwezi Novemba, 2006 ulifanyika Mkutano Mkuu wa Kilele *(EAC Summit)* Jijini Arusha. Kati ya maamuzi ya msingi ya Mkutano huo ni Kuunda Upya Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuweka Kitengo cha Mahakama ya Awali na Kitengo cha Mahakama ya Rufaa. Muundo huu unakusudia kuimarisha utoaji wa haki katika Mahakama ya Jumuiya kikamilifu zaidi kuliko ilivyokuwa. Mfumo wa awali ulikuwa hautoi fursa ya kukata rufaa kwa upande wowote usioridhika na hukumu. Fursa hiyo sasa ipo. Kutokana na marekebisho haya, Mahakama ya Awali itakuwa na Majaji kumi (10) na ya Rufaa Majaji watano (5). Katika Mkutano wa kilele *(EAC Summit)* mwezi Juni 2007, Viongozi Wakuu wa Jumuiya walikubaliana kuwa katika kipindi cha mpito vitengo hivyo vya Mahakama ya Jumuiya vitakuwa na Majaji watano kila kimoja. Aidha, *'Summit'* iliamua kuweka utaratibu maalum wa Mafao kwa Majaji wa Jumuiya na kuwa utaratibu huo utatumika pia katika kuwalipa mafao Majaji Wastaafu akiwemo Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba wa Tanzania na Jaji Solomy Bossa wa Uganda. Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Jaji Warioba kwa kazi nzuri aliyoifanya katika Mahakama ya Afrika Mashariki na kuiletea Tanzania sifa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria *(Lake Victoria Basin Comisión),* Jumuiya ya Afrika Mashariki iliendelea na kazi za utekelezaji wa

kuhifadhi mazingira pamoja na kuboresha uchukuzi na usalama katika Ziwa Victoria. Mradi wa kuboresha uchukuzi na usalama katika Ziwa Victoria *(Lake Victoria Safety and Navigation Study)* umekamilika. Aidha, imeanzishwa Tume ya Bonde la Ziwa Victoria *(Lake Victoria Basin Commission)* yenye Makao Makuu mjini Kisumu, Kenya ambayo ilizinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Kenya Mheshimiwa Mwai Kibaki mwezi Juni, 2007. Nchi yetu iliwakilishwa na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume hiyo inasimamia mazingira na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika Ziwa Victoria kwa faida ya wakazi wapatao zaidi ya milioni thelathini (30) wanaoishi kandokando mwa ziwa hilo. Nchi ya Kenya imetoa hekta mbili na nusu kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya Tume hiyo mjini Kisumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kushuka kwa kina cha maji ya Ziwa Victoria, Viongozi Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mkutano wao uliofanyika Jijini Arusha mwezi Novemba, 2006, walielekeza Jumuiya ya Afrika Mashariki ifanye uchunguzi wa kina ili kubaini kiini cha tatizo hilo na kutoa mapendekezo ya hatua madhubuti zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na tatizo hilo. Kwa lengo hilo, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki imepanga kuitisha mkutano wa dharura wa Mawaziri wa Nchi Wanachama ili kujadili hali hiyo ambayo inatishia upatikanaji wa maji kwa matumizi ya binadamu, mifugo, viwanda, usafiri wa majini na uzalishaji wa umeme. Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa katika eneo hili na ambayo itainufaisha Tanzania inajumuisha Mradi wa Usalama na Uchukuzi katika Ziwa Victoria *(Lake Victoria Safety and Navigation Project)* pamoja na Mradi wa Kuendeleza Makazi ya Wananchi Waishio kandokando mwa Ziwa Victoria *(Lake Victoria Regional Water and Sanitation Initiative).* Mradi huu unatarajiwa kuhusisha miji 22 katika Nchi za Kenya, Uganda na Tanzania. Napenda kutumia nafasi hii kuwaomba na kuwahimiza wananchi na Taasisi zitumiazo Ziwa Victoria kuunga mkono juhudi hizi za kuendeleza na kutunza mazingira ya eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki za Kuanzisha Taasisi mpya, kuongezeka kwa shughuli za Jumuiya ni dalili njema za kukua kwake. Kwa maana hiyo kukua kwa Jumuiya kunaambatana na uanzishwaji wa Taasisi mpya zitakazosimamia majukumu mapya yatokanayo na ukuaji na maendeleo ya Jumuiya. Katika mwaka 2006/2007 Jumuiya ilianzisha Taasisi Nne (4) mpya. Kwa hiyo Itifaki mpya zilizopitishwa na kusainiwa mwezi Aprili, 2007 ni pamoja na:-

(i) Kamisheni ya Afrika Mashariki ya Sayansi na Teknolojia *(East African Science and Technology Commission (EASTECO):* Kamisheni hii itakapoanzishwa itaratibu na kusimamia utafiti na uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia katika Jumuiya. Kwa maana hiyo, ukuzaji na uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia utapata msukumo zaidi katika Nchi Wanachama ikiwemo Tanzania.

(ii) Kamisheni ya Afrika Mashariki ya Usalama wa Anga *(East African Civil Aviation Safety and Security Oversight Agency (CASSOA):* Kamisheni hii itaunganisha taasisi za

Nchi Wanachama katika kusimamia usafiri wa anga na usalama wake. Kwa hiyo, kuwepo kwake kutaimarisha juhudi zetu za kitaifa katika kukuza na kuendeleza usafiri wa anga.

(iii)Kamisheni ya Afrika Mashariki ya Utafiti wa Afya *(East African Health Research Commission (EAHRC):* kama zilivyo Kamisheni zingine za Jumuiya, Kamisheni hii pia lengo lake kuu ni kuimarisha mchakato wa utafiti katika sekta hii unaofanywa na taasisi mbalimbali za Nchi Wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Itifaki ya Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mojawapo ya itifaki iliyosainiwa mwezi Aprili, 2007. Juhudi za kuimarisha na kuendeleza lugha ya Kiswahili zimefikia hatua nzuri kutokana na kusainiwa kwa Itifaki ya Kamisheni ya Kiswahili. Kamisheni hiyo itakuwa mojawapo ya Taasisi katika Jumuiya kama zilivyo Kamisheni nyingine. Mojawapo ya lengo la kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ni kutambua na kuendeleza lugha ya Kiswahili kutokana na mahusiano ya karibu yaliyojengeka kwa muda mrefu kati ya wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Spika, hivi sasa Jumuiya ya Afrika Mashariki iko katika mchakato wa kupata Makao Makuu ya Kamisheni hii. Tanzania imeomba kuwa Makao Makuu ya Kamisheni hii yawe Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa itifaki ya Umoja wa Forodha, utekelezaji wa kuondoleana vikwazo vya kibiashara ulianza kutekelezwa tarehe 1 Januari 2005 baada ya Itifaki ya umoja wa Forodha kusainiwa mwaka 2004. Mpangilio wa kutekeleza vipengele vya ngazi zote za Itifaki hii unatarajiwa kukamilika mwaka 2010. Kwa ujumla licha ya matatizo ya hapa na pale, utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha unaendelea kama ulivyopangwa kwa mwaka 2006/2007. Pale matatizo yalipojitokeza, yamepatiwa ufumbuzi wa haraka na nchi wanachama kupitia majadiliano ya kuelewana katika vikao halali vya mfumo wa ngazi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga mazingira bora yenye ufanisi kwa ajili ya utekelezaji wa masuala ya Umoja wa Forodha, Nchi wanachama zinalenga kupunguza vipingamizi katika biashara zinazotokana na Vikwazo Visivyo Vya Ushuru *(Non Tariff Barriers).* Hii inatokana na matakwa ya Kifungu Na.13 cha Itifaki ya Umoja wa Forodha ambacho kinahimiza Nchi Wanachama kuondoleana vikwazo visivyo vya Ushuru kwa lengo la kuboresha mazingira ya kuendeleza biashara katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vikwazo Visivyokuwa vya Ushuru vimeendelea kuwapo katika Nchi za Jumuiya na kuwa kero kubwa kwa wafanyabiashara wengi. Baadhi ya maeneo yaliyobainishwa kuwa ni Vikwazo Visivyo vya Ushuru na yanayotafutiwa ufumbuzi yanaainishwa kama ifuatavyo:

(i) Taratibu na Nyaraka nyingi za Kiforodha;

(ii) Taratibu za uhamiaji zilizojaa ukiritimba;

(iii) Vikwazo katika nyanja ya ukaguzi;

(iv) Vikwazo vya barabarani;

(v) Kanuni na taratibu za biashara zisizofanana katika nchi Wanachama;

(vi) Wingi wa taasisi zinazohusika na uagizaji wa mizigo nje ya nchi; na

(vii) Taasisi nyingi zinazohusika na usajili wa leseni za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha mazingira ya kibiashara baina ya Nchi Wanachama, mfumo wa kukabiliana na aidha kuondoa au kupunguza Vikwazo Visivyokuwa vya Ushuru ni nguzo muhimu katika kukuza na kuendeleza mauzo ya bidhaa na huduma kati ya Nchi Wanachama wa Jumuiya. Nchi Wanachama zilipitisha mfumo wa kukabiliana na matatizo ya Vikwazo Visivyo vya Ushuru mwezi Agosti 2006. Kipengele muhimu katika mfumo huo ni kuwa na Kamati za Kitaifa katika kila Nchi Wanachama za kufuatilia vikwazo husika (*National Non Tariff Barriers Monitoring Committee)* ambazo zilizinduliwa mwezi Juni, 2007. Tukio hili lilifanyika kwa kushirikiana na *The East African Business Council (EABC).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la msingi la Umoja wa Forodha ni kulifanya eneo la Afrika Mashariki kuwa eneo moja la Kibiashara kwa bidhaa zinazozalishwa katika Nchi Wanachama na kukabiliana kwa pamoja katika ushindani wa kibiashara na bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya. Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Umoja wa Forodha umetoa fursa ya kukuza na kuendeleza uchumi wa Nchi Wanachama kwa kufungua mipaka ya nchi zetu kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Umoja wa Forodha uanzishwe, pamekuwepo na mafanikio makubwa kwa Jumuiya na kwa Tanzania. Mwenendo wa biashara katika Jumuiya unaonyesha kuwa biashara baina ya Nchi Wanachama imeongezeka. Jedwali Na.4A linaonyesha kuwa mauzo yetu katika Jumuiya yaliongezeka toka Dola za Kimarekani 95.4 Milioni mwaka 2004 hadi Dola 117.1 Milioni mwaka 2006, sawa na ongezeko la asilimia 23.4. Katika kipindi hicho hicho manunuzi yetu yaliongezeka toka Dola za Kimarekani 137.7 Milioni hadi Dola 174.4 Milioni kama ilivyoonyeshwa katika Jedwali Na. 4B.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria za kuboresha mazingira ya Biashara katika Jumuiya, Sheria ya Usimamizi wa Ushuru wa Forodha ya mwaka 2004 *(EAC Customs Management Act, 2004)* ni nguzo muhimu katika usimamiaji na ufuatiliaji wa karibu wa utekelezaji wa vipengele mbalimbali katika Itifaki ya Umoja wa Forodha. Katika kujenga mazingira muafaka ya ushindani ndani ya Afrika Mashariki, Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikubaliana kuwa na sera na sheria moja itakayosimamia ushindani miongoni mwa wafanyabiashara na watoa huduma katika Nchi Wanachama. Sheria hiyo ilipitishwa mwaka 2006 *(East African Community Competition Law).* Aidha, mwaka huo huo sheria ya Kusimamia Viwango, Ubora na Vipimo vya Bidhaa zitakazouzwa katika soko la Afrika Mashariki ilipitishwa *(The Standards, Quality Assurance, Metrology and Testing Act, 2006).* Inatarajiwa kwamba utekelezaji wa Umoja wa Forodha utakamilika ifikapo mwaka 2010 na baada ya hapo Soko la Pamoja la Afrika Mashariki *(East Africa Common Market)* litaanzishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maandalizi ya uanzishaji wa soko la pamoja *(Common Market)* maandalizi ya Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki yatahusu majadiliano ya pamoja na utekelezaji wa soko la pamoja. Maandalizi hayo yanafanyika kitaifa na kikanda. Kwenye ngazi ya Kitaifa, Wizara imekwishaainisha wadau watakaounda Timu ya Watalaam itakayohusika na majadiliano ya Soko la Pamoja. Timu hiyo ya Wataalam inaundwa na Wadau toka sekta zote zinazoguswa na masuala ya Soko la Pamoja. Timu ya Wataalam kwa kushirikiana na Wataalam Elekezi watakaoteuliwa na Wizara itaandaa mapendekezo ya msimamo wa kitaifa katika masuala yote ya majadiliano; itaainisha fursa na changamoto za Soko la Pamoja la Afrika Mashariki na kushiriki katika Majadiliano ngazi ya Wataalam. Katika ngazi ya Jumuiya, Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mkutano wake uliofanyika Jijini Arusha tarehe 4 Aprili, 2006, liliiagiza Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kufanya utafiti wa kina kuhusu Soko la Pamoja. Matokeo ya zoezi hili yaliwasilishwa kwa wadau Jijini Dar es Salaam tarehe 22 Juni, 2007. Mheshimiwa Spika, hatua zote hizi zinakusudia kuliwezesha Taifa na Nchi Wanachama kwa ujumla kujiandaa ili kushiriki kikamilifu katika majadiliano ya Soko la Pamoja. Ratiba inaonyesha kuwa majadiliano yamepangwa kuanza mwezi Septemba, 2007 na kukamilika mwezi Desemba, 2008. Baada ya hapo itafuata hatua ya kuweka sahihi Itifaki ya Soko la Pamoja na kuridhiwa na Bunge hili ili utekelezaji uanze mwezi Januari, 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi na programu zingine za Jumuiya, katika kipindi cha 2006/2007 Jumuiya iliendelea kutekeleza Miradi na Programu kadhaa katika Sekta ya Kilimo, Miundombinu, Nishati, Usalama na Usafiri wa Anga, Mtandao wa Mawasiliano na Ukuzaji wa Sekta Binafsi. Katika kipindi hiki, Nchi Wanachama ziliandaa Sera na Mkakati wa pamoja kwa ajili ya kuendeleza kilimo kwa lengo la kuwa na uhakika wa chakula cha kutosha kwa mahitaji ya ndani ya Jumuiya na kuuza nje ya Jumuiya. Aidha, Jumuiya iliendelea kutekeleza mradi wa barabara ya Arusha – Namanga – Athi River na Barabara ya Bagamoyo – Sadan – Tanga – Horohoro - Mombasa – Malindi. Barabara hizi zikikamilika zitaiunganisha Arusha na Nairobi na pia bandari ya Dar es salaam na Mombasa na hivyo kurahisisha usafiri na usafirishaji katika ukanda wa Mashariki na Kaskazini mwa Tanzania. Mheshimiwa Spika, ushirikiano katika usafiri wa anga uliimarika katika kipindi cha 2006/2007 kwa kuanzishwa chombo kimoja kitakachosimamia usalama wa usafiri wa anga katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Menejimenti ya chombo hicho inayoongozwa na Mtanzania imekwishateuliwa na kuanza kazi. Chombo hiki kitasaidia sana katika kujenga uwezo katika nyanja hii na kuweka mazingira bora ya kuvutia wawekezaji katika sekta ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki imejiwekea utaratibu wa kuendesha Maonyesho ya biashara kila mwaka kwa wafanyabiashara wadogo maarufu kama Jua Kali/NguvuKazi. Katika kipindi cha 2006/2007 Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Maonyesho hayo mwezi Desemba 2006 Jijini Dar es salaam. Maonyesho haya ni muhimu katika kukuza na kuendeleza sekta binafsi katika Jumuiya hususan katika kusaidia sekta isiyo rasmi kukua na hatimaye kuwa sekta rasmi. Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru wananchi wote walioshiriki na kufanikisha Maonyesho ya mwaka huu na natoa wito kwao kushiriki kikamilifu katika Maonyesho yajayo yatakayofanyika Nairobi, Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshaji mazingira ya utendaji kazi, mwaka 2006/2007 Wizara ilifanikiwa kujaza nafasi za ajira 26 za watumishi wa kada mbalimbali wakiwemo wachumi, wanasheria, na maafisa Biashara. Katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, Wizara ilinunua vifaa na vitendea kazi kwa Idara na vitengo vyake. Aidha, Wizara ilizindua Baraza la Wafanyakazi; lengo kubwa likiwa ni kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi na utawala bora kwa ujumla. Pia Wizara iliendesha mafunzo ya kupambana na rushwa na UKIMWI mahala pa kazi kwa lengo la kuboresha utendaji na kujenga uelewa wa watumishi.

Mheshimniwa Mwenyekiti, Mipango ya kazi za Wizara katika mwaka 2007/2008, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara za kisekta pamoja na wadau mbalimbali itaendelea na juhudi za kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mkataba wa Kuanzisha Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Itifaki zake. Aidha, Mkakati wa Tatu wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (2006-2010) utazingatiwa ili kuwawezesha Wananchi kushiriki kikamilifu katika kuzitumia fursa mbalimbali za kiuchumi kwa ufanisi na kwa manufaa yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeainisha maeneo ya kipaumbele ya utekelezaji kwa mwaka 2007/2008 kama ifuatavyo:-

(i) Kuratibu na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Mkataba wa Jumuiya na Itifaki zake pamoja na maamuzi mbalimbali ya vyombo vya Jumuiya ukiwemo Mkutano Mkuu wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya, Baraza la Mawaziri, Bunge na Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

(ii) Kushirikiana na wadau kutoa elimu na mafunzo kwa wananchi kuhusu fursa na changamoto zilizo katika Jumuiya;

(iii) Kuratibu na kusimamia kikamilifu maandalizi na majadiliano ya kuanzisha Soko la Pamoja;

(iv) Kufanya tathmini ya miradi na programu zilizo chini ya Jumuiya na kuandaa mapendekezo ya mikakati ya uboreshaji kwa manufaa ya nchi yetu na Jumuiya kwa ujumla;

(v) Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Forodha na kuhakikisha kuwa inakuwa chachu na nguzo ya maendeleo nchini;

(vi) Kujenga uwezo wa Wizara kwa kuajiri watumishi wenye taaluma zinazohitajika, sifa na uzoefu unaokidhi utekelezaji bora pamoja na kuendeleza taaluma zao na kuwawekea mazingira bora na vitendea kazi;

(vii) Kuingiza masuala mtambuka *(mainstreaming crosscutting issues)* katika mipango na mikakati ya Wizara hususan *HIV/AIDS,*Utawala bora, Mazingira na Jinsia;

(viii) Kuandaa na kuratibu mipango, programu na bajeti ya Wizara kulingana na mwongozo wa *MTEF,* MKUKUTA na Dira ya Taifa 2025; na

(ix) Kutayarisha na kusimamia matumizi ya fedha za Serikali kulingana na sheria na kanuni na taratibu za fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti shukrani, mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yametokana na Ushirikiano wa Serikali yetu, Taasisi za Umma na binafsi, Mashirika yasio ya Kiserikali, Wafanyabiashara pamoja na wananchi kwa ujumla. Wizara kama mratibu wa masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, inatambua kuwa mafanikio ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali yametokana na ushirikiano mzuri kati ya wadau wa sekta mbalimbali na Wizara. Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba nichukue fursa hii kuwashukuru wote waliohusika kwa njia moja ama nyingine kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Pia napenda kuwashukuru wananchi katika mikoa yote, Tanzania Bara na Zanzibar, kwa kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni yao kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki. Naomba kutoa shukrani za dhati kwa wote ambao wamenisaidia katika kusimamia kazi za Wizara. Kwanza kabisa napenda kumshukuru mke wangu, Zainab Ibuni. Kwa msaada anaonipatia katika kuhakikisha kwamba ninafanya kazi zangu vizuri. Pili, naomba nimshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Waziri mwanzilishi wa Wizara hii kwa kuweka misingi mizuri pale Wizarani. Tatu, naomba nimshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala kwa kunisaidia katika masuala mbalimbali hapa Bungeni na Wizarani na pia nimshukuru Mhesihmiwa Katibu Mkuu, Bwana Wilfred Nyachia, kwa msaada wake wa karibu anaonipa katika kusimamia majukumu ya Wizara. Napenda pia kuwashukuru Wakuu wa Idara na Vitengo, pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara. Aidha, napenda kumshukuru Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Balozi Juma Mwapachu, Sekretariati ya Jumuiya, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hususan Kamati ya Mambo ya Nje, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa Ushirikiano wao katika kufanikisha shughuli za Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya na ili kufanikisha shughuli mbalimbali za Wizara naomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya shilingi 8,007,280,000/= (bilioni nane, milioni saba na mia mbili themanini elfu) kwa ajili ya matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kwa mchanganuo ufuatao:-

Kwanza, Shilingi 5,422,014,000/- ukiwa ni Mchango wa Uanachama wa Nchi yetu kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki;

Pili, Shilingi 319,994,000/- kwa ajili ya Mishahara *(PE)* ya Watumishi wa Wizara; na

Tatu, Shilingi 2,265,272,000/- kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti naafiki.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yako. Kabla sijamwita Msemaji wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje niwaandae tu wachangiaji watakaofuata baada ya uwasilishaji wa Msemaji wa Kamati na Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ambao nimeona tuanze na Wajukuu wa Mheshimiwa Waziri, mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga na atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Rápale Chegeni. Naomba sasa nimwite Msemaji wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje. Anakuja Mheshimiwa Kasella-Bantu na yeye ni mjukuu pia. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. TEDDY LOUISE KASELLA-BANTU (k.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE):** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kila jambo na hasa leo kwa kutuweza sisi wote kuwa hai na wa afya njema, hivyo kuweza kutimiza majukumu yetu ipasavyo. Nasema *deogratius.* Pia napenda kuwashukuru familia yangu na hasa watoto wangu Kasella, Marina na Rosemary kwa kuwa karibu nami kila mara. Nawashukuru sana.Naomba sasa nitoe maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kamati yangu ndiyo inawasilisha maoni yake kwa mara ya kwanza katika Bunge hili la bajeti, kwa niaba ya Kamati na kwa niaba yangu mimi mwenyewe binafasi, na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa jimbo la Bukene, naomba kutoa salamu za rambirambi kwako binafsi, Bunge hili, wananchi wote wa mkoa wa Dar es Salaam, hususan Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi na Taifa kwa ujumla kwa kuondokewa na mpendwa wetu marehemu Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge.

Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia alikuwa mzalendo na mchapakazi na mauti yake imefika wakati taifa letu na hasa Bunge hili likimhitaji sana katika utekelezaji wa majukumu yake na katika ujenzi wa Taifa hili kwa ujumla. Naomba Mwenyezi Mungu azilaze Roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje kwa hekima na uzoefu wao kuhusiana na masuala mbali mbali katika nyanja za ushirikiano wa kikanda ambao umesaidia kujadili na kuchambua kwa kina masuala hayo pamoja na bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka fedha 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima naomba niwatambue kwa kuwataja majina Wajumbe wa Kamati hii ambao wote ni Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Anna M. Abdallah Mwenyekiti, Mheshimiwa Mussa A. Zungu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohamed R.Abdallah, Mjumbe, Mheshimiwa Ame P. Ame, Mjumbe, Mheshimiwa Abubakar K. Bakary, Mjumbe, Mheshimiwa Mohamed G. Dewji Mjumbe, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mjumbe, Mheshimiwa Balozi Khamis S. Kagasheki, Mjumbe, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mjumbe na ndiye anayesoma. *(Makofi)*

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Yono S.Kevella, Mjumbe, Mheshimiwa Khalifa S. Khalifa, Mjumbe, Mheshimiwa Hassan C. Kigwalilo, Mjumbe, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mjumbe, Mheshimiwa Ali A. Mohamed, Mjumbe, Mheshimiwa Balozi Abdi H.Mshangama, Mjumbe, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mbunge, Mheshimiwa, Mjumbe, Mheshimiwa Muhonga S. Ruhwanya, Mjumbe, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mjumbe, Mheshimiwa John M. Shibuda, Mjumbe, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mjumbe, Mheshimiwa Zainab M.Vulu, Mjumbe. *(Makofi)*,

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha Mbunge, Naibu waziri Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala, Mbunge Katibu Mkuu wa Wizara na Wataalam wengine kwa kuwasilisha mbele ya kamati mapendekezo ya Bajeti ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyoelezwa na Mheshimiwa Waziri, Wizara inaomba jumla ya fedha bilioni.8,405, 280,000/= kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na mishahara shilingi milioni 319,994,000/= michango ya nchi kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki shilingi bilioni 5,422,014,000/= na shilingi bilioni 2,585,272,000/= kwa ajili ya kuendeshea shughuli za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati:-

Moja, Serikali iendelee kutoa elimu kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwe na bajeti maalum kwa ajili ya hiyo. Bajeti hiyo iwe ya kudumu na mitaala yetu ijumuishe suala la Afrika Mashariki.

Mbili, Serikali iharakishe utoaji wa vitambulisho vya raia ili kuepuka kuwagawia ardhi na stahili zingine wageni pindi Shirikisho la Afrika Mashariki litakapoanza. Tatu, ili kuhimili ushindani ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki Kamati

inashauri urasimu katika bandari zetu uondolewe, aidha miundombinu iboreshwe ili kuimarisha shughuli za uchumi nchini.

Nne, Serikali ishiriki kikamilifu na kwa umakini katika miradi ya kulinda mazingira ya Ziwa Viktoria. Aidha makao makuu ya miradi hiyo yawe nchini Tanzania kwa kuwa sehemu kubwa Ziwa hilo iko nchini mwetu

Tano, Kamati inasikitishwa na kiwango kidogo cha bajeti, kilichotolewa kwa ajili ya Wizara hii. Bajeti hiyo ni Shilingi bilioni 8,007,280,000/= kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 5,422,014,000/= ni kwa ajili ya mchango wa Tanzania kwa Jumuiya. Hii ina maana kwamba bajeti halisi ya Wizara hii ajili ya shughuli zake zote ikiwa ni pamoja na mishahara ya watumishi wake kwa mwaka 2007/2008 ni shilingi bilioni 2,585,266,000/= tu.

Sita, Kiswahili ni moja ya lugha iliyokubalika kutumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki na kwamba walimu wanahitajika kwa ajili ya kufundisha lugha hii katika nchi za Rwanda, Burundi na kwingineko barani Afrika na duniani kwa ujumla. Kamati inashauri Serikali iwe na mkakati maalum wa kuandaa walimu kwa ajili ya kufundisha lugha ya Kiswahili ndani ya Afrika Mashariki na kwingineko duniani.

Saba, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ipo kwa ajili ya kulinda maslahi ya Tanzania ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha Wizara hii inaratibu maamuzi yanayofikiwa na vyombo mbalimbali ndani ya Jumuiya. Utekelezaji wa maamuzi haya unapaswa kufanywa na Wizara na Idara mbalimbali za serikali. Kamati inashauri Wizara na Idara za Serikali zifuatilie maamuzi haya na kuyatekeleza kikamilifu ili nchi yetu inufaike na kuwepo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Nane, Kwa kuwa kuna malalamiko mengi kuhusu utendaji usioridhisha katika bandari zetu hususan, bandari ya Dar es salaam, Kamati inashauri Wizara ya Miundombinu ichukue hatua za kuboresha utendaji wa kazi katika bandari hiyo ili wafanyabiashara wasihamishie shughuli zao katika bandari za nchi jirani na hivyo kuikosesha mapato Serikali yetu.Tisa, Serikali isimamie ipasavyo ujenzi wa barabara zilizoainishwa katika mtandao wa barabara za Afrika Mashariki zilizoko nchini mwetu ikiwemo barabara ya Dar es salaam kupitia Bagamoyo, Saadani, Pangani, Tanga mpaka Horohoro ambayo iko katika mpango wa utekelezaji kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Mheshimiwa Mwenyekiti hitimisho, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kuhusu mapendekezo ya Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2007/2008.

Kamati inampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuunda Tume ya kukusanya maoni ya Watanzania kuhusu uharakishwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki. Aidha tunampongeza Prof.

Samuel Wangwe kwa kuiongoza vizuri Tume hii mpaka ilipomaliza kazi yake kwa ukamilifu na kuwasilisha Taarifa yake kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba fedha zilizotengwa kwa ajili ya Wizara hii hazitoshi, hata hivyo Kamati inasisitiza kuwa kuweko na nidhamu ya hali ya juu katika kutumia fedha iliyotolewa. Mheshimiwa Mwenyekiti mwisho, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje kwa kuandaa Taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo,napenda kulishauri Bunge lako Tukufu likubali kujadili na hatimaye kupitisha mapendekezo ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika bajeti hiyo ambayo ni jumla ya shilingi bilioni 8,405,280,000/= .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti**,** naunga mkono hoja ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABUUBAKARY KHAMIS BAKARI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA USHIRIKIANO WA AFRIKA YA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa Bungeni tukiwa hai na wazima. Pili, naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuchangia kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 43(5)(b)(c) na 81(1) na kutoa maoni, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuhusiana na Wizara ya Afrika Mashariki, Wizara ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi zetu za Afrika Mashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi nichukue nafasi hii kutoa shukrani za pongezi za kipekee kwa viongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa uongozi wao madhubuti wenye kuifanya Kambi ifanye kazi yake kulingana na Kanuni zetu za Bunge. Bila kusahau, nitoe pia pongezi kwa wabunge wote wa Upinzani kwa ushirikano walionao, wakishirikiana na wale wote wanaoweka mbele maslahi ya nchi hii, kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kwa maslahi ya Taifa na Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na maafa na majanga mbalimbali ambayo yote ni miongoni mwa mitihani yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tuwaombee wenzetu wote waliokwishatangulia makazi mema peponi, na wale waliopatwa na maumivu waweze kupona haraka. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba yangu ya mwaka jana, nilielezea kwa kirefu historia ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika hotuba yangu hii nitapitia dondoo za msingi ili kujenga uwazi wa hoja yangu. Tutakumbuka kuwa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda zimekuwa katika ushirikiano toka zamani, takriban miaka 109 sasa. Ushirikiano huu ulianza tangu nchi hizi zikiwa chini ya utawala wa kikoloni, ingawa

Tanganyika ilichelewa kujiunga na shirikisho hilo kwa sababu wakati huo Tanganyika ilikuwa chini ya utawala wa Kijerumani wakati Kenya na Uganda zilikuwa chini ya himaya ya Waingereza. Hata baada ya uhuru nchi hizi ziliamua kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki hapo mwaka 1967, ingawa kwa kipindi hiki sasa Tanganyika na Zanzibar ziliingia kama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu zilizopelekea kuundwa kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki zilikuwa ni za kiuchumi, kisiasa, kijamii, kiusalama na kihistoria. Sababu hizi ndiyo misingi ya ushirikiano popote pale duniani ikizingatiwa kwamba katika dunia ya leo ushirikiano ni jambo la muhimu sana katika jitihada za maendeleo. Sisi tunaamini kuwa hili ni jambo la busara kwa maendeleo ya mataifa yetu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mmoja wetu anaelewa kuwa baada ya miaka 10 tu ya kuundwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya hiyo ilivunjika. Sababu za kuvunjika kwa Jumuiya hiyo zilikuwa haziepukiki. Nilitaja katika Hotuba yangu ya mwaka jana sababu hizo ambazo hadi leo hii zipo. Sababu hizi ni pamoja na:- kukosekana kwa nia za kweli kweli kwa nchi husika; kutofautiana kiuchumi kwa nchi wanachama; kutoshirikishwa ama ushirikishwaji mdogo wa raia juu ya uundwaji wa Jumuiya hiyo; kutokuweka utaratibu mzuri wa mgao wa mapato na hasara za Jumuiya hiyo kwa nchi husika; uroho wa madaraka wa baadhi ya Wakuu wa nchi hizo; itikadi tofauti za kisiasa (wakati Tanzania ilikuwa kwenye mfumo wa kijamaa, Kenya ilikuwa kwenye mfumo wa ubepari, na Uganda ilikuwa na mfumo wa kijeshi). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuvunjika Jumuiya hii, kasoro nyingine zilijitokeza yakiwemo malalamiko ya ulipaji kiinua mgongo usiokuwa na uwiano sawa kwa waliokuwa wafanyakazi wa jumuiya. Tanzania, kwa mfano, haijakamilisha malipo hayo hadi hivi sasa wakati Kenya na Uganda wameshawalipa wananchi wao wote

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar pia haikutendewa haki, malipo kutokana na iliyokuwa bodi ya sarafu ya Afrika Mashariki ambayo yalikuwa yalipwe kwa Zanzibar, hayakufikishwa Zanzibar, bali yalichukuliwa na Serikali ya Tanzania na eti kuingizwa katika uanzishwaji wa Benki Kuu ya Tanzania. Sina uhakikika kama ridhaa ya Serikali ya Zanzibar ilipatikana au hapana. Lakini vyovyote itavyokuwa, kuanzishwa huku kwa Benki kwa mitaji ya nchi mbili ni kielezo cha kuwa Benki hiyo ni ya pamoja, na ikiwa kuna nia njema, basi faida na hasara za Benki hiyo ni lazima zigawiwe kwa mlingano ule ule wa mitaji iliotolewa na Tanganyika kwa wakati huo na Zanzibar.

Mhshimiwa Spika, athari ya wazi iliyojitokeza punde baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ni kuibuka na kuendelea kwa uhasama wa kisiasa baina ya nchi za Arika Mashariki. Matokeo ya uhasama huo ni kufikia hatua ya vita vya maneno na kukejeliana baina ya Kenya na Tanzania na hata kupelekea kufungwa kwa mpaka baina ya nchi mbili hizi katika mwaka 1977. Pia kuibuka kwa vita baina ya Tanzania na Uganda mnamo mwaka 1978 ni moja ya athari hizo. Kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki hapo mwaka 1977 kamwe hakukumaanisha kuwa jumuiya haikuwa na umuhimu wowote. Kuthibitisha hili, baada ya miaka 14, hapo mwaka 1991, marais wa Kenya, Tanzania na Uganda waliona haja ya nchi zao kushirikiana hasa katika nyanja za uchumi ambapo

waliridhia kuanza kwa majadiliano mapya. Mkataba wa kuanzishwa tena Jumuiya ulitiwa saini Julai 2000, na kuzinduliwa rasmi Januari, 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar wakati huu iliwakilishwa kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sasa si mwanachama kamili kama ilivyokuwa kwa Jumuiya iliyokufa. Jambo hili sio geni, kwani kuna mifano mingi tu katika ulimwengu huu ambapo mahusiano ya namna kama hii yaliwahi kuundwa na baadae kuvunjika. Mifano ya Afrika ni muungano wa Senegal na Gambia na shirikisho la Ghana, Guinea na Mali. Muhimu hapa ni kuelewa sababu ambazo zilifanya mashirikiano hayo kuvunjika, na ni somo gani ambalo tunaweza kusoma kutokana na matukio hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zinazotolea juu ya sababu ya kuundwa upya kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kasi mpya ya kwenda katika Shirikisho ni kuongeza nguvu za kiuchumi na kupunguza migogoro ya mara kwa mara kwa nchi wanachama. Kwa upande wetu tunahisi kuwa kitu muhimu cha kuangaliwa ni taasisi za ushirikiano zilizojengwa na nchi wanachama, vipi zilifanya kazi, vipi zilisaidia wananchi wa nchi hizo, ni nini kilichotokea hadi kufikia mgawanyiko na ni nini cha kufanya ili tukianza na ushirikiano mpya basi hayo yaliyotokea nyuma yasije yakatokea tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha ni kwamba nchi zetu hazikusoma matatizo ambayo yalisababisha kuvunjika kwa Jumuiya hiyo ili kuondoa uwezekano wa kuvunjika tena Jumuiya hiyo hapo baadae. Kama vile haya hayatoshi, sasa tumewaingiza Rwanda na Burundi kwenye Jumuiya hii ikijulikana wazi kuwa hali ya utulivu katika nchi hizi bado haijatengemaa, maendeleo ya kiuchumi ya nchi hizi nayo ni tofauti na nchi za Tanzania, Kenya na Uganda.

Baya, zaidi ya yote haya ni kukosekana kwa ridhaa za wananchi katika maamuzi ya kuingiza nchi hizi katika Jumuiya likiwa ni moja na funzo muhimu la kushindwa Jumuiya iliyotangulia. Na nini hasa masharti yaliyowekwa kwa nchi jirani kutaka kujiunga na shirikisho kama vile Somalia, *DRC* na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa hali ya dunia hivi sasa ipo katika mwelekeo wa nchi zilizo majirani na; au kupakana kuunda Jumuiya za Kiuchumi kwa nchi hizo. Hoja zitolewazo ni kuwa kuongeza wanachama katika Jumuiya ni kuimarisha umoja. Lakini je hatuoni kuwa nchi zetu zina mitazamo tofauti ya kiuchumi, kimila, kisiasa, kiusalama na kwamba hii inaweza kutuongezea matatizo mbali mbali katika nchi zetu kuliko kufikia lile lengo letu tulilolikusudia? Kwanini hatukukaa kwanza na kutafakari kwa kina matatizo tuliyonayo? Haraka hizi ni za nini? Na kwa nini tufanye haraka kwa gharama za watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kushangaza ni kuwa wakati bado nchi zetu hizi zinakumbwa na matatizo mengi ya ndani, na mengine, yakiwemo matatizo yale yaliyosababisha kuvunjika kwa Jumuiya hii, wakuu wa nchi zetu wameamua kuingiza wanachama zaidi katika jumuiya hiyo. Je, isingelikuwa vyema kwanza tukatatua matatizo tuliyonayo sisi wenyewe kabla ya kujibebesha matatizo ya wengine? Sasa tunashabikia suala la kuunda Shirikisho la kisiasa haraka sana kama inavyowezekana. Ni kwa nini viongozi wetu hawafikirii kutatua matatizo ya ndani kwanza na kuboresha hali

ya kiuchumi kwa kila nchi kabla ya kufikiria kuingia katika Shirikisho? Je, tunaunganisha nguvu au tunaunganisha matatizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kuwa ushawishi huu wa kuungana ulileta na wakoloni kwa madhumuni mawili tu. Kwanza ni kupunguza gharama za uendeshaji katika makoloni yao, na pili ni kulinda maslahi ya walowezi hao. Kabisa haikuwa nia yao ya kutaka kumnufaisha mwananchi wa Afrika Mashariki. Lengo letu sasa ni kuwanufaisha watu wetu. Lakini kwa haraka hizi ndio kweli tutafikia lengo hilo la kumnufaisha mwananchi wetu au tutafikia lengo la kumkandamiza mwananchi wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zetu wanachama (Kenya, Uganda na Tanzania) zina matatizo mengi sana. Kenya, kuna matatizo ya kikabila, mfumo wa kisiasa wenye athari za ukabila, na mapigano ya kikabila. Uganda nayo halikadhalika si nchi shwari. Inaandamwa na jinamizi la *Lord Resistance Army (LRA*); pia mfumo wa kisiasa umetawaliwa na nguvu za kijeshi chini ya Amiri Jeshi Mkuu, mfumo ambao hata ile kanuni muhimu ya kuheshimu Katiba ya Nchi haiheshimiwi. Imefika hadi sasa Uganda wanapinda Katiba yao ili muda wa kuendelea kwenye madaraka uongezeke. Uganda bado kuna athari kubwa za mgawanyiko wa kikabila. Tanzania vilevile ina matatizo mengi. Suala la Muungano sasa limekuwa "mwiba ndani ya nyama." Malalamiko ya Kikatiba nayo yamekuwa ni mengi. Hali ya hewa ya kisiasa kuchafuka mara kwa mara huko Zanzibar na mpasuko wa kisiasa unaozidi kila uchao ndio inazidi kuidhoofisha Zanzibar, nalo ni miongoni mwa matiatizo makubwa ndani ya Tanzania ambayo ni lazima kupatiwa ufumbuzi kabla ya kujiingiza ndani ya matatizo mengine ya nchi za Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipongeze juhudi za mazungumzo yanayoendelea katika ya Chama cha Wananchi (CUF) na Chama cha Mapinduzi (CCM) juu ya matatizo ya kisiasa Zanzibar. Lakini pia sina budi kusema juhudi hizo zimekuwa zikizorota sana, na zisizokuwa za wazi kwa wananchi kuelewa ni nini hasa kinaendelea. Donda hili tulilonalo lisingefaa kabisa tukaliongezea na madonda mengine yaliyomo Kenya, Uganda, Rwanda, na Burundi na kuyauguza kwa pamoja. Tuchukue msemo wa zamani wa hekima wa kwamba "tutengeneze kwetu kwanza na baadae twende kwa wenzetu" vinginevyo, hali hii tete tunayoichezea inaweza hatimae ikatibua hali ya utulivu iliopo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi kabisa hali ya demokrasia katika nchi zetu za Afrika Mashariki bado ni mbovu . Ni bora na ni uamuzi wa busara kuwa kwanza nchi hizi zingeboresha walau siasa zao kabla kuingia katika Shirikisho ili tusije tukaangukia katika mfumo mbovu zaidi wa kisiasa na kuzidisha matatizo. Hatima ya haya ni kwa kuvunjika Shirikisho ambalo kwayo ni kipindi kidogo tu toka kuzaliwa upya. Hilo litakuwa pigo jingine kubwa la kisiasa kwa nchi wanachama pamoja na viongozi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuharakishwa Shirikisho la Afrika ya Mashariki? Nchi za Afrika ya Mashariki zipo katika harakati za kuunda shirikisho lao. Kuwa na umoja wa aina hii ni wazo zuri sana, na kwa mantiki hiyo lengo la kuunda Shirikisho la Afrika ya Mashariki ni jema na hivyo basi kambi yetu ya upinzani

tunalikubali, kwa kutumia maneno ya watani wetu mia juu ya mia. Suala ni je, tunalikubali vipi? Hapa pana makundi mawili. Kundi la kwanza tutaliita kundi la sasa hivi (*now*), hawa huitwa "*radicals*" na la pili ni kundi la hatua kwa hatua (*gradualism*). Msimamo wa Kambi yetu ni hatua kwa hatua, kwani haraka haraka haina baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba muda wa Tanzania kukubali kuunda Shirikisho haujafikia. Hii ni kutokana na ukweli kuwa hata huu utangamano tulionao sasa haujaleta matunda. Vilevile yapo matatizo mengi sana yanayopaswa kushughulikiwa kabla ya uamuzi huo. Madhumuni ya kusubiri ni kuhakikisha kuwa wakati nchi hizi zitakapoamua kufanya maamuzi hayo hatua muhimu za kutatua matatizo yetu ya kiuchumi na kisiasa ziwe zimeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya kuzingatiwa kwa makini sana kabla ya kuchukua maamuzi ya kuwa na Shirikisho ni pamoja na:-

(i) Tofauti za kiuchumi za nchi wanachama ambapo uchumi wa Kenya uko juu pamoja na maendeleo ya viwanda ukilinganisha na nchi zetu za Tanzania na Uganda. Tanzania haijafikia uwezo wa kushindana na Kenya katika sekta hii na hivyo basi ni hofu yetu kuwa Tanzania inaweza kugeuzwa soko la bidhaa za Kenya. Je, Tanzania imejiandaaje kuingia katika ushindani huu wa kibepari? Je, muda wa matayarisho (*grace period*) wa miaka 5 utatosheleza kwa Tanzania na Uganda kufikia hatua ya Kenya?

ii) Kenya na Uganda wana uhaba wa ardhi nzuri yenye rutuba wakati Tanzania bado kuna maeneo makubwa ya ardhi yenye kufaa kwa shughuli za kilimo na ufugaji wa kisasa. Hofu ya Watanzania ni uwezekano wa ardhi hii kuvamiwa na wageni kutoka nchi jirani na kuleta migongano ya ardhi, jambo ambalo ni tatizo kubwa na wakati mwingine huwa ndio sababu ya mapigano baina ya watu au makabila.

(iii) Uwezekano wa wageni kujinufaisha na rasilimali zetu asilia kutokana na uwezo wao mkubwa zaidi wa kimtaji na uwezo wa kifedha kuwekeza katika uvunaji wa rasilimali hizo kuliko sisi wa Tanzania. Bado nchi zetu hizi hazina ukweli na uaminifu. Kenya kwa mfano, mara kadhaa hujitangazia vivutio vya utalii vilivyopo Tanzania kama vile ni vya kwao. Mfano mzuri ni mlima Kilimanjaro au uuzaji wa magogo ya Tanzania. Kenya pia iliongoza kuuza *Tanzanite* wakati wazalishaji ni Tanzania. Je, tukiingia katika Shirikisho itakuwaje? Nini hatima yetu kwa haya? *(Makofi)*

(iv) Hofu kwa vijana wa Kitanzania kukosa ajira rasmi kutokana na ushindani wa soko la ajira, hili pia linachangiwa na mfumo wetu wa elimu na udhaifu wa lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa Kitanzania. Madhara yake ni kuongezeka umaskini, na vijana wetu daima watakuwa na kazi duni nchini mwao. Je, hili ndio lengo letu la kujitawala? *(Makofi)*

(v) Kukosekana kwa kitambulisho rasmi kinachomtambulisha raia wa Tanzania nalo ni tatizo kubwa sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kenya na Uganda tayari wanawatambua raia wao wote kwa vitambulisho vya uraia, bado Tanzania

hatujahakikisha kuwa na mikakati hii. Watanzania wana hofu kuwa raia wa nchi jirani ambazo zina migogoro kama vile Rwanda na Burudi na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (*DRC*), watasababisha kuzagaa kwa migogoro nchini. Hii itazidisha maovu ambayo kwayo tunapigana nayo.

(vi) Kila nchi hadi sasa inatumia sarafu yake, sarafu ambazo zinatofautiana sana kithamani. Kwa mfano, thamani ya sarafu ya Kenya ni zaidi ya mara kumi na tano kithamani ukilinganisha na ile ya Tanzania. Vivyo hivyo sarafu ya Uganda hailingani na ile ya Kenya au Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa ngazi za juu wa Serikali ya Zanzibar na wanachi walipata kutoa maoni yao kuhusu Shirikisho. Huko Zanzibar walipinga kuharakishwa kwa Shirikisho. Zanzibar pia ina mamlaka juu ya mambo ambayo si ya Muungano kama vile afya, elimu, kilimo, mawasiliano, na biashara. Mambo haya kwa mujibu wa mkataba wa Jumuiya ni mambo ambayo yamo ndani ya Shirikisho, lakini pia ni masuala yanayopaswa kushughulikiwa na Zanzibar kuwa na maamuzi huru. Sasa Zanzibar itawakilishwa vipi? Je, huku si kuporwa mamlaka ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa kufanya shughuli za Zanzibar ambazo si mambo ya Muungano? Huku ni dhahiri kuwa tunakiuka makubaliano ya Muungano pamoja na Katiba zetu zote mbili. Je, si tunaanzisha kero za Muungano ndani ya shirikisho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu hizi na nyingi nyinginezo ambazo hatukuzieleza bado zinatufanya sisi Kambi ya Upinzani, na Watanzania walio wengi kuona kuwa bado hakuna haja ya kuharakisha shirikisho hili. Ni vyema suala hili tukalipeleka kidogo kidogo na huku tukijaribu kutatua na kuyamaliza matatizo tuliyonayo sisi wenyewe nchini mwetu kabla ya kuyaunganisha matatizo ya nchi nyingine wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya kufikia Shirikisho mwaka 2013 ni ndoto au matarajio mema? Wakuu wa nchi zetu tatu walifikia makubaliano ya hatua muhimu za kutekelezwa kabla ya kufikia mwaka 2013. Hatua hizo ni pamoja na:- kuwepo kwa Umoja wa Bandari (*Customs Union*) mwaka 2005; soko la pamoja (*Common Market*) mwaka wa 2007; kutumika kimataifa kwa pasi ya pamoja ya kusafiria ya Afrika Mashariki hapo 2008 (*common passport*); na kuwa na umoja wa sarafu ifikapo 2009 (*Monetary Union/Common Currency*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hili lenye mpangilio wa hatua kwa hatua ni zuri sana. Hata wenzetu wa Umoja wa Ulaya (*Eroupean Union*) walianza hatua kwa hatua na bado hawajafikia shirikisho la kisiasa hadi sasa. Hatua hizo ziliaanzia kwa Umoja wa wazalishaji makaa ya mawe, wakaendelea na biashara pamoja na soko lake; umoja wa forodha na uchumi wa pamoja (*economic intergration*) na hatimaye umoja wa fedha za pamoja. Hata katika suala hili la fedha za pamoja kuna wengine kama vile Uingereza ambao bado hawajakubali wakizingatia zaidi maslahi ya uchumi wao. Umoja huu sasa ni zaidi ya miaka 50 na bado hawajaungana moja kwa moja kisiasa. Afrika ya Mashariki imeota nini kitachokuwa kizuri zaidi? Tunahisi ni ubinafsi wa baadhi ya viongozi wa nchi wanachama pamoja na nchi zenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sivyo, ni lazima tuchunge maslahi ya nchi zetu na watu wetu. Haya ndiyo tunayoyapendekeza katika Kambi yetu, yaani "*gradualistic approach*" ndio utaoleta faida kwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukitathmini hali ilivyo hivi sasa kwa Jumuiya hii, hali ya wasi wasi imekwishaanza kuwafunika mioyo Watanzania wengi. Umoja wa forodha uliotiwa saini tarehe 1/1/2005 ndio uliopewa kipaumbele kama ndio mkakati mkubwa wa kuelekea shirkisho hili. Ibara ya 75(7) ya mkataba wa Jumuiya inasisitiza:- kuwepo kwa uhuru zaidi wa biashara za nchi hizi bila ya nchi kuingiliana na mwenzake; kuendeleza zaidi uzalishaji wa bidhaa ndani ya nchi hizi za Jumuiya; kuendeleza uwekezaji wa ndani na nje pamoja na biashara ya mipakani na kuendeleza zaidi uchumi wa nchi zetu pamoja na kuwa na viwanda mbalimbali kwa lengo la kustawisha nchi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo haya bado yanatofautiana baina ya nchi zetu. Bado nia za nchi hizi haziko sawa. Kwa mtazamo wa Kambi yetu mambo yafuatayo yana mashaka:-

(i) Kenya ambayo iko mbele kimaendeleo kwa viwanda na kiuchumi, haina nia njema ya kuziinua Tanzania na Uganda kwa kuwa na uwiano sawa. Hili lipo wazi katika muda waliopewa Tanzania na Uganda wa miaka 5 kuwa ni muda wa kujiweka sawa (*grace period)* ni mdogo sana, usiotosha kuziinua nchi hizi kiuchumi.

(ii) Kenya bado inavutia kwake tu, hasa katika suala la mizigo inayotoka Tanzania katika magari ya Tanzania ambapo magari hayo hulazimishwa kupakua mizigo mpakani na kubebwa na magari ya Kenya, kwa kisingizo tu kuwa devera huyo wa Tanzania hana *"International Driving Permit" (IDP). (Makofi)*

(iii) Mbao zinazotoka Tanzania (Ludewa) kwa mfano zinasafirishwa hadi Kenya, na zinapofika Kenya hupigwa mihuri ya Kenya ili zionekane kuwa mbao hizo ni mazao ya Kenya.

(iv) Unyanyasaji wa wafanyabiashara za mipakani *(cross boarder traders)* unakua siku hadi siku. Je, haya na mengineyo mengi si yatatufanya Watanzania tuingie kichwa kichwa tu katika shirikisho hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo Tanzania au Watanzania bado hawana ari ya kufanya kazi kutokana na mfumo tuliokuwanao. Upungufu huu wa lengo *(lack of seriousness)* utatugharimu sana sana. Mizigo ilioko bandarini Dar-es-Salaam, kwa mfano inachukua wiki 3 ili iweze kutolewa wakati mizigo kama hiyo ikiwepo bandari ya Mombasa basi ni siku moja au mbili tu ili iweze kutoka. Hatima ya hili ni kuwafanya wafanyabiashara wetu watolee mizigo yao Mombasa na hivyo kuinufaisha zaidi Kenya.

Haya yote yanatuthibitishia ya kuwa matatizo tulionayo katika nchi zetu basi ni lazima tuyatatue mwanzo ili tunapoingia katika shirikisho hilo basi iwe matatizo hayo madogo madogo hayapo. Zaidi hii inathibitisha vilevile kuwa mwenendo hasa

unaotakiwa kufuatwa ili kuingia katika shirikisho hilo ni kidogo kidogo ili kutoa nafasi kwa nchi husika kumaliza matatizo yaliopo nchini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inaunga mkono dhana na shirikisho la Afrika Mashariki kama moja na nguzo imara katika maendeleo ya taifa letu. Kwa mtazamo wa Kambi yetu tatizo lipo katika utaratibu uliowekwa wa kufikia shirikisho hili, hasa kulingana na programu nzima ya "*fast tracking*". Hivyo basi Kambi yetu itapinga vikali mambo yote yatakayoonekana kupelekea uundwaji wa shirikisho ambalo halitakuwa na manufaa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirikisho imara litazaa matunda kwa kutupatia utulivu wa hali ya kisiasa, ulinzi na usalama wa pamoja, kujenga uchumi wenye nguvu, pamoja na kuwa na kauli moja yenye nguvu *(strong bargaining power).* Lakini ili kufikia huko tunapendekeza tufanye yafuatayo:-

(a) Nchi yetu ianze kuweka mikakati ya kujiandaa kiuchumi na kiushindani katika soko huria kwa muda wa kipindi kisichopungua miaka 15 toka sasa huku tukifanya tathmini ya mikakati hiyo. *(Makofi)*

(b) Tuboreshe mfumo wetu wa elimu na kuwaanda vijana wetu kiushindani wa soko la ajira la pamoja mapema na haraka iwezekanavyo.

(c) Kwanza tujenge demokrasia ndani ya nchi zetu na kutatua migogoro ya kisiasa na kijamii iliyomo ndani ya nchi zetu kabla ya kuharakisha kuunda Shirikisho litalokuwa na mizozo tele.

(d) Serikali itoe vitambulisho vya uraia kwa Watanzania wote wenye haki hiyo kisheria.

(e) Uandaliwe utaratibu wa kura za maoni katika kila nchi mwananchama ili wananchi wenyewe wawe na kauli ya mwisho kuhusu uanzishwaji wa Jumuiya hii au la. Tofauti na utaratibu uliotumiwa sasa ambao haukukidhi matakwa ya watanzania wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kusikitisha na baya zaidi ni kuwa viongozi wetu tayari wamefikia hatua ya mwisho ya mchakato wa kutafuta wimbo wa Shirikisho. Ahadi nyingine ni kuwa ifikapo mwaka 2013 Rais wa Shirikisho ataingia madarakani. Wakati haya yakisemwa, kwa mujibu wa Tume ya Profesa Wangwe Watanzania wengi wamepinga shirikisho. Je, hapa maamuzi ni ya Watanzania au viongozi wetu? Je, kwa hali hii uamuzi wa Wananchi katika maamuzi haya muhimu umezingatiwa? Kambi ya Upinzani kamwe haitakuwa tayari kuwatelekeza wananchi na Watanzania wote kwa ujumla katika suala zito kama hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inapendekeza hatua muhimu za kufuatwa ili tuweze kujenga shirikisho lililo imara katika mtiririko ufuatao:- kuanzishwa kwa eneo la biashara huru *(Free trade Area)*; kuwepo kwa Umoja wa forodha *(Customs*

*Union)*;  kuwa na Soko la pamoja *(Common Market)*;  kuanzisha utangamano wa kiuchumi *(Enonomic Intergration)* ambapo sera za kiuchumi na masuala ya fedha za nchi wananchama huwa sera katika nchi wanachama, na  kuundwa kwa shirikisho la kisiasa *(Political Federation)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo, Shirikisho la kisiasa ni hatua ya mwisho ambapo nchi wanachama zitakuwa zimejizatiti kiuchumi na kisiasa kutokana na kuwepo kwa uhuru wa kuingia na kutoka kwa watu na bidhaa zao baina ya nchi wanachma, kuondolewa kwa vikwazo vya ushuru katika biashara baina ya nchi wanachama, kuwa na soko kubwa la pamoja, na kuwa na sera za kiuchumi zenye kuafikiana.  Si vibaya, kuchuja ya wenzetu na tukayachukuwa yale tunayoyaona ni muhimu.  Umoja wa Ulaya ulipitia njia hii hii.  Haukufanya haraka na mpaka sasa kuna nchi ambazo hazitaki kupoteza utambulisho wa nchi zao (*identity*). Na sisi tusifanye haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, tunapoamua hatima ya Tanzania na watu wake, ni vyema tukawashirikisha wananchi wenyewe na maamuzi yao kuheshimiwa. Jumuiya au mashirikisho ya aina hii sasa yanaundwa kila uchao, na sisi Watanzania tusijitenge kwa hilo. Muhimu ni kutazama kwa undani zaidi vipi wananchi wetu watanufaika kutokana na Jumuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia hayo, basi tutazame matatizo yaliyomo katika nchi yetu na tuanze kuyatatua ili kutuepusha kuingia ndani ya shirikisho huku tukiwa na matatizo yetu. Pia lazima tuhakikishe kuwa yale matatizo yaliyosababisha kuvunjika kwa jumuiya hii hapo awali yote yamepatiwa ufumbuzi kabla ya kuendelea na shirikisho kamili. Tuwe na msimamo wetu kuwa shirikisho ambalo halitupatii faida kwa wananchi wetu basi hakuna maslahi ya kujiunga nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru pamoja na waheshimiwa wabunge wote kwa kunisikiliza, na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunashukuru sana Mheshimiwa kwa kuwasilisha maoni haya kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Ushirikiano Afrika Masharika na maoni ya Kambi ya Upinzani. Sasa tunaingia katika hatua ya uchangiaji, na kama nilivyosema mwanzo, ninayo orodha hapa. Watakaoanza kuchangia ni Mheshimiwa Zitto, Mheshimiwa Serukamba, Mheshimiwa Slaa, Mheshimiwa Lucy Nkya, pia wajiandae watafuata baada ya muda si mrefu. Tunaanza na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa kwa mara nyingine tena kuchangia moja ya hotuba za bajeti ya Mkutano huu wa Bunge la Bajeti unaoendelea na leo ni hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya  Mashariki. Nianze kwa kumshukuru au hasa kumpongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wengine wote wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki chini ya uongozi wa kaka yangu Mheshimiwa Balozi Juma Mwapachu, kwa kazi nzuri wanayoifanya mpaka hivi sasa. Baada ya pongezi hizo, sasa napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyofahamu ilipoanzishwa Jumuiya hii kwa mara ya pili, safari hii tulikuwa na makubaliano ambayo yanajulikana kama *treaty*, na *treaty* hiyo ilijenga msingi wa namna ambavyo ushirikiano wetu utakavyokuwa katika kipindi cha kuanzia tulipoanza na kuendelea hadi *infinitum*. Kwanza tunasema tutaanza na umoja wa forodha, soko la pamoja, sarafu moja na ikiwezekana shirikisho la kisiasa. Kwa bahati nzuri mpaka sasa hivi tumekwishaanza umoja wa forodha. Nilitarajia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri angetueleza mafanikio na matatizo ambayo mpaka sasa tumekwisha pambana nayo au tumeyapata chini ya umoja wa forodha. *(Makofi)*

Kama tunavyofahamu katika kutekeleza huu umoja wa forodha, tumejikuta katika hizi nchi tatu, nchi moja imeendelea zaidi ya nchi nyingine mbili kiviwanda, kwa sababu nchi zote hizi tatu zinazalisha mazao yanayofanana ya kilimo. Na kwa maana hiyo biashara yetu kusema kweli ni mazao ya kilimo isipokuwa kwa kiasi kidogo Kenya wenzetu wana mazao ya viwandani. Kutokana na hali hiyo biashara baina yetu sisi watatu ni ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yule anayetuzidi ndiye ambaye anatuuzia zaidi wengine kuliko sisi tunavyomuuzia yeye. Anayetuzidi hapa kiviwanda ni Kenya. Kwa hiyo, Kenya ndiye anayetuuzia sisi wengine kibiashara. Kwa kutambua hilo Umoja huu wa Forodha uliweka utaratibu wa kwamba bidhaa za kutoka Kenya kwenda Uganda na Tanzania zitakuwa zinatozwa kodi kwa kipindi cha miaka mitano ijayo na sasa imebaki miaka kama miwili. Mpaka hapo itakapofikia dhamira ilikuwa ni kwamba huenda na hizi nchi nyingine na zenyewe zitakuwa zimeanzisha viwanda vyake ili kuweza kushindana na Kenya katika eneo la viwanda. Suala la kujiuliza hapa ni kwamba kwa kiasi gani sisi kama Tanzania tumelizingatia hilo na tumejitayarisha endapo tutafikia mwisho au ukomo wa zile kodi (*duties)* tunazoziweka kwenye *imports* za kutoka Kenya kuja Tanzania; je, wakati huo tutakuwa na viwanda vya kuweza kuzalisha bidhaa za viwandani ili tuweze kuwauzia Wakenya na Waganda? Jibu ninaloliona mimi kwa kweli ninapata wasiwasi, sioni kama tuko katika hali ya kujitayarisha kuwa na viwanda ambavyo vitakuwa shindani na wenzetu wa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ningependa nisisitize tu kwamba, kama nilivyosema kwenye hotuba ya Wizara ya Viwanda na sasa nitarudia na nisisitize, kuna eneo moja sisi Tanzania tumelipoteza, eneo hili ni la Kiwanda cha Matairi (*General Tyre East Africa*). Kiwanda cha Matairi nadhani ndio kilikuwa kiwanda cha kwanza cha matairi *East Africa* na matairi yake yalikuwa yanapendwa sana katika *East Africa* nzima. Sijui kulitokea nini tukazembea. Mpaka sasa hivi kiwanda kile hakizalishi matairi kwa wingi na kuuzwa katika soko la Afrika Mashariki ambalo kusema kweli huu ndio ulikuwa ni wakati wa kuchukua faida ya soko kubwa kwa sababu hatima ya umoja huu kusema kweli ni kutengeneza soko kubwa ili tuweze kuwa na viwanda ambavyo vitatumia *economies of scale*. Kwa sababu badala ya kuwa na viwanda vidogo vidogo unapokuwa na kiwanda kimoja kikubwa kwa ajili ya soko kubwa hapo unakuwa na faida kubwa zaidi kuliko vinginevyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya Kiwanda hiki cha *General Tyre* kwa sasa tumekiacha kinahangaika. Matokeo yake wenzetu wa Kenya baadaye walianzisha kiwanda cha *fire stone*. Leo tunalalamika kuondoa *suspended duty* kwa matairi ya *fire stone* kutoka Kenya ili yaje Tanzania ambako tuna kiwanda cha *General Tyre* ambacho tumekiacha kinakufa! Kusema kweli hii hali haieleweki na ninazungumza maneno haya kwa uchungu kabisa kwamba hii ni nafasi ambayo tungeweza kuitumia, tumeiacha sasa *equation* imebadilika, badala ya sisi ku-*export* matairi tuna-*import* matairi ya *fire stone* kutoka Kenya!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nataka nilisisitize hili la kujiweka sawa kwamba katika kipindi hiki ambacho bidhaa zetu zinafanana na ili tuweze kutumia soko kubwa hili la Afrika Mashariki na sisi kama Watanzania tunahitaji kuanzisha viwanda vikubwa kwa ajili ya soko hilo kubwa. Nitoe pendekezo lingine tu kwamba aina nyingine ya viwanda ambayo nadhani tunaweza tukatumia soko hili kubwa ni viwanda vya *pharmaceuticals* na hasa katika eneo hili la sasa hivi la maradhi haya ya UKIMWI ambayo kuna nchi duniani zimegundua dawa za *ARVs*. Tukipata leseni ya *ARVs* kutoka katika nchi zinazoendelea kama sisi ambazo zimetuzidi kama India au Brazil wakaturuhusu kutengeneza dawa zao kwa leseni Tanzania, tukipata *license* hizo tunaweza tukatumia soko kubwa la Afrika Mashariki kutengeneza dawa hizi Tanzania na tukazipeleka huko kwenye soko hilo. Hebu tuchangamkie na eneo hili vile vile kwa ajili ya soko kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo tuna *comparative advantage* ambalo tunaweza tukalitumia vilevile kwa ajili ya viwanda ni eneo la nguo. Tanzania inalima pamba, tunalima pamba, wakulima wetu wanalima pamba lakini inasikitisha kwamba tunauza *(export)* nje pamba ghafi wakati tungeweza kuwa na viwanda vya nguo hapa nchini. Vipo baadhi yake, kimoja kipo Tabora kinaitwa Kiwanda cha Nyuzi. Unatumia pamba kutengeneza uzi ili uupeleke nje ya nchi kule watengeneze nguo wakurudishie wewe uliopeleka uzi ununue nguo, haieleweki tena! Kwa hiyo, ni suala la kuchukua na kutumia *comparative advantages* zetu katika hali halisi inayostahili.

Tuna pamba basi tuweke *integrated textile mills* zitakazotengeneza kuanzia uzi, *grey cloth*, mpaka kitenge, khanga na nguo nyingine zinazotokana na pamba. Kwa kufanya hivyo vilevile tutatumia tena soko hili kubwa la Afrika ya Mashariki mbali na *advantage* nyingine tulizonazo za mimea kama zabibu ambazo zinaweza kutengeneza *wine* nzuri tu tukawa tunatengeneza *wine* kwa ajili ya soko la Afrika Mashariki. Zaidi ya yote sasa hivi Tanzania inajulikana kama *the East African Power House*, tuna uwezo wa kutengeneza umeme mwingi sana, umeme huu soko lake ndiyo hilo la Afrika Mashariki basi tulichangamkie kwa haraka haraka.

Sasa nije kwenye eneo la *EPA*. Nilisema hili kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara lakini nadhani hapa ndiyo mahali pake. Sasa hivi kuna mazungumzo baina ya *European Union* na nchi zinazoendelea chini ya mifumo ya *customs union*. Tanzania, Uganda na Kenya kwa bahati mbaya katika hili hatutazamani macho kwa macho pamoja na kwamba wote ni watu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tanzania ina-*discuss EPA* chini ya *SADC*, Uganda na Kenya wana-*discuss EPA* chini ya *COMESA*. Huu ni

mtafaruku mkubwa ambao hauna sababu. Nashauri tukae kwenye meza moja tukubaliane (*compromise)* kwamba sisi ni wa Afrika Mashariki tuzungumze *EPA* chini ya Afrika ya Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la kuwawezesha wawekezaji Afrika Mashariki kupata fedha za kuweza kuwekeza. Tunacho chombo cha Afrika Mashariki ambacho kwa bahati kilipona kufa wakati Jumuiya ya Afrika Mashariki ilipokufa kwa mara ya kwanza. Chombo hiki ni Benki inayojulikana kwa jina la *East African Development Bank*. Tunahitaji kuitengeneza upya benki hii chini ya Afrika ya Mashariki mpya na kuiwezesha kifedha na kimtaji ili iweze kuwa ndio chimbuko la kusaidia maendeleo ya Afrika ya Mashariki. Tuchukue mfano wa *European Investment Bank* na kuifanya *East African Development Bank* iwe kubwa kiasi hicho kwa ajili ya maendeleo ya Afrika ya Mashariki, nasisitiza hili sana tena kwa dhati kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile nitume fursa hii kuzungumzia suala la nafasi ya *East African Legislative Assembly*. *East African Legislative Assembly* ipo lakini inapokaa na kutunga sheria na kutoa maamuzi, maamuzi yale hayawi *implemented* katika maeneo ya Afrika ya Mashariki bila kufanyiwa mabadiliko.

Sasa kama hivyo ndivyo wenzetu kule kwenye *legislative assembly* wanafanya nini? Kwa maana nyingine ni kwamba chombo hiki hakijapewa nguvu ya kufanya kazi za kisheria na kwamba wakiweza kuamua basi wameamua na tuendelee mbele ku-*implement* lakini hali hiyo haiko hivyo na tunatumia pesa kukifanya chombo hiki kifanye kazi, maana yake naona kama hizo pesa tunazipoteza kwa sababu kile chombo hakina meno.

Hatujakipa meno, tunawafanya wafanye kazi, wanatunga visheria wakimaliza wanasema *it cannot be implemented,* ikija Tanzania tunasema hiyo hatuijui mpaka tuipitie tena upya tuone kama inalinda maslahi yetu. Kwa maana hiyo kuna haja ya kutazama tena mfumo mzima wa kazi na shughuli za *East African Legislative Assembly* na *power* zake na kwa kiasi gani wanayoyafanya tunaweza na sisi vilevile tukayatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo la *harmonization* ya *documentations* kwenye suala zima la biashara ya ndani ya Afrika ya Mashariki, *documentation and harmonization*. Nadhani wataalamu wanaelewa nilitaka kujua tu kwamba suala hilo limefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote ningependa kufahamu kwamba katika mfumo mzima wa Jumuiya mpya katika zile hatua nne tuko kwenye hatua ya soko la forodha lakini hatujaambiwa hizi hatua nyingine za sarafu moja zikoje, mwanga ukoje, tunaona nini kule mbele? Kuna matayarisho gani mpaka sasa hivi? Tumeruka tukaenda kwenye *federation,* mbona hapa kwenye sarafu moja hatuzungumzi chochote? Hata hivyo, kwenye upande wa soko la pamoja kidogo ndio tumeambiwa matayarisho yanaendelea.

Nimalizie kwa kuuliza suala la viza moja kama *East Africa* limefikia wapi? Kwa sababu watalii wanaotoka nchi za nje si ingekuwa vizuri tu kama anayetaka kuja Tanzania akiende Ubalozi wa Kenya akichukua viza akaja Tanzania. Anakwenda Kenya kama vile ambavyo wenzetu wa *Europe* ukienda kuchukua viza kwenye nchi moja inatosha kukupeleka katika nchi zote za *EU*. Nadhani utaratibu huo tungeufanya vilevile *East Africa,* na kwa kweli tungeweza kurahisisha matumizi ya pamoja, hata ya balozi zetu kwa mambo ambayo yanafanana kwa Afrika ya Mashariki. Tuna kila sababu ya ku-*discuss* kwa pamoja masuala ya kidiplomasia pamoja na masuala ya kiuchumi na hasa tunapoichukua *East African Community* kama *block* moja ya kiuchumi tungeweza kabisa. Je, tunazitumia balozi zetu katika kufanikisha mambo haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kuweza kuandaa hotuba hii ya bajeti ambayo mimi nasema kwamba mwanagu Msabaha amejitahidi sana. Kwa sababu kama ulivyosema Msabaha chimbuko lake ni usukumani na ndio maana hakuna mzaramo mrefu kama Msabaha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi labda tu na mimi niseme kwamba kwanza naunga mkono hoja hii, haina ubishi lakini katika kuunga mkono nadhani si vibaya kutoa ushauri nasaha kwa Wizara hii. Wizara hii bado ni changa inahitaji kweli ipewe kila aina ya ushauri na pengine iweze kusaidia na kutekeleza majukumu inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina wasiwasi na Dr. Msabaha kwa sababu ni mtu amebobea sana kwenye masuala ya Kimataifa na msaidizi wake Dr. Kamala ambaye ni mchumi mzuri, mmoja ya wachumi wazuri katika nchi hii, kwa hiyo, *it is a good combination***.** Kwa msingi huo napenda vilevile kutumia nafasi hii kuanza kuwapongeza Wabunge wetu wa *East Africa*, safari hii nina imani kabisa tulipeleka Wabunge ambao kweli wanastahili na wameanza kuonyesha kazi nzuri toka mwanzo wa kipindi chao, napenda niwapongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bajeti ya Wizara hii linagusa sana hisia za Watanzania ambao tunaguswa vilevile na msisitizo wa ushirikiano na utengamano ndani ya Jumuiya yetu. Watanzania wengi bado tunasita sita kwamba je, tuingie kichwa kichwa au tusubiri kidogo na ndio maana hata kwenye Tume ya Profesa Wangwe Watanzania wengi wameonyesha kusita sana kwenda katika hatua ya mwisho ya *political federation* kwa sababu bado wanakumbuka yaliyotokea huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine ni muda muafaka kwa Watanzania kuweza kubadilika mawazo, lazima tu-*change* ile *mind set* kwa sababu hakuna jinsi sisi kama sisi tuka-*operate in isolation,* Lazima tu-*operate* kwa pamoja, lazima tuongeze nguvu za pamoja, tuongeze mtaji wa watu wetu, tupanue soko la bidhaa zetu, bila kufanya hivyo hatuwezi kupanua uchumi wetu. Lakini pengine wasiwasi mkubwa ni kukosekana kwa nia za kweli kweli miongoni mwetu. Naamini kwamba hata Tume ya Profesa Wangwe

kwanza kama ingetoa elimu kwa Watanzania juu ya faida na hasara, kwa nini tunakimbilia hatua ya *political federation* Watanzania wangeweza kuelewa zaidi. Lakini wakati huo Watanzania wengi walikuwa wanaambiwa tu faida bila kuambiwa hasara kwa nini wanajiunga, hii ilileta kidogo matatizo na ndio maana Watanzania wengi wamejaribu kuonyesha nia ya kusita sana kuweza kuingia kwenye *political federation*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza sana hatua za Rwanda na Burundi kuweza kushirikishwa kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki. Rwanda na Burundi zimekuwa na historia ya kipekee katika ukanda wa maziwa makuu, lakini haiwezekani kuendelea kukaa na majirani ambao wana matatizo bila kuwasaidia. Huu ni moyo wa kizalendo wa Watanzania, ni moyo wa kizalendo wa majirani zetu wa Kenya na Uganda kuweza kuziruhusu Rwanda na Burundi kuingia katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Naamini kabisa hii ni hatua muhimu sana tunapaswa kuipongeza kwamba sasa ukanda wa nchi za maziwa makuu tunaweza kushikamana na tukawa *very strong block* ambayo inaweza kuwa ina *bargaining power.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuangalia mfumo wa Watanzania, ukirudi nyuma kuna mambo tunahitaji tuyafanye tunapozungumzia suala zima la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kwanza, mfumo wa elimu kati ya nchi zetu unatofautiana, uwezo wa kutoa wahitimu unatofautiana. Inakuwa haina tija sana kwa Mtanzania kuweza kuona kwamba tukimbilie kule, hiyo ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka ukiangalia Watanzania tuko karibu milioni 38 lakini kwa mwaka tunatoa wahitimu wa vyuo vikuu na vyuo vya elimu ya juu kati ya 25,000 au 30,000 kwa mwaka, wakati Kenya wao wako milioni 28 wanatoa wahitimu zaidi ya 60,000 au 65,000 kwa mwaka. Uganda wako milioni 24 wao wanatoa wahitimu kati ya 35,000 au 40,000 kwa mwaka. Sasa ukiangalia tukishafungua mipaka kazi nyingi na shughuli nyingi zitafanywa na wageni zaidi kuliko Watanzania wenyewe kwa sababu bado hatuja-*match up* kutoka kwenye *competition* iliyo sawa na kuingia mahali ambapo tunaweza tuka-*match up*. Hili ndilo tatizo ambalo ningeomba sana Watanzania na kupitia Wizara hii watusaidie kuweka msukumo ambao utaweka mtekenyo wa aina yake katika kuwasaidia Watanzania waweze kukabiliana na haya mashindano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika suala zima hili mimi nizungumzie suala la Wabunge wetu wa Afrika Mashariki. Sisi ni Wabunge ambao tuna majimbo na hata kama siyo majimbo kuna viti maalum, baada ya kutoka Bungeni hapa tunarudi katika majimbo kuelezea kwamba nini kimetokea, kupeleka ule mwitikio (*feedback)*. Hivyo hivyo kabla ya kuja huku Bungeni tunakuja na ajenda kutoka kwa wapiga kura lakini toka tulivyoanza awamu ya kwanza Wabunge wetu wa Afrika Mashariki hawakupewa nafasi hiyo na mpaka leo hii hawana nafasi ndani ya Bunge hili kuja kutoa taarifa ya shughuli ambazo zinafanyika katika Bunge la Afrika Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inakuwa hakuna *communication,* hawa Wabunge wetu tumewatuma kule wakafanye kazi kwa niaba yetu, sisi ndio jimbo lao lakini tunadhani hatujawapa haki yao kutueleza wanafanya nini na kuwatuma wakafanye nini.

Kuna haja ya msingi kabisa ya kubadilisha utaratibu huu na kuweka sheria ili tuwape nafasi ya kuja hapa Bungeni watueleze wanafanya kazi gani na sisi tuwatume kwa maslahi ya Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote haya kuna mambo ya kuangalia sana, kwa mfano, suala zima la tofauti za kiuchumi. Hii inaleta nafasi ambayo inavunja ile hali ya Watanzania na baadhi ya wengine kudhani kwamba tunaweza tukashirikiana katika mchakato mzima wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ukiangalia Ukanda wa Ziwa kwa mfano mimi natoka Mkoa wa Mwanza, mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera ni mikoa ambayo imepakana na nchi hizi za Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi. Bado tunahitaji kuweka msukumo zaidi wa miundombinu ili kuleta changamoto kubwa hata kibiashara. Leo hii Mwanza *Airport* ukifika pale *Airport* unasema hivi nimepita kwenye kijiji gani kwa sababu haina hadhi kwamba inaweza ikawa *Airport* ya kuweka *hub* ya nchi husika za ukanda wa nchi za maziwa makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja ya kuweka msukumo wa makusudi kabisa katika bajeti yetu na kuharakisha mipango hii ili vitu ambavyo vinachangia au vinachochea maendeleo kwa haraka zaidi vipewa nafasi. Mimi ninaamini kwamba uwanja wa ndege wa Mwanza ukiwa *International Airport* watalii hawawezi kwenda Nairobi, hawawezi kwenda Entebbe, watapenda kuja zaidi Mwanza ili waende Serengeti kwa haraka zaidi. Kutoka Mwanza kwenda Serengeti ni kilomita 140 lakini ukishuka Nairobi kwenda Serengeti au kushuka *KIA* bado ni mbali zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa tunajaribu kukosa nafasi nzuri ya kuchochea uchumi wetu. Lakini pili kuna hii miradi kama huu mradi wa magugu maji, ukiangalia mradi huu umetumia fedha nyingi sana lakini leo magugu maji yamerudi katika Ziwa Victoria. Sasa sielewi kwamba mpango mzima wa kukabiliana na suala hili tunautekeleza kwa namna gani kwa sababu bado kuna tatizo kubwa sana na magugu maji yanaua viumbe ndani ya maji ambayo banuai inakuwa *so much affected* pamoja na samaki. Na hii ukiangalia hata mazalia ya samaki sasa yamekuwa na matatizo, samaki wanapungua lakini huwezi ukafunga samaki kwamba sisi tusivue huku kwetu Tanzania wenzetu wa Kenya watavua samaki, hawahitaji pasipoti kwenda Kenya au Uganda. Sasa ni suala ambalo lazima mjaribu kuwa na mkakati wa pamoja kwamba tunatumia vipi rasilimali zetu kwa uwiano na mustakabali wa wananchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la utalii kwa mfano, mahoteli, katika mikoa ambayo tunadhani kwamba ingekuwa kivutio zaidi ndio tumeweka msukumo zaidi na kuweka *incentives.* Najua mfano kama Dodoma hapa wakati tunasema tunahamia Dodoma tumesema mtu akitaka kujenga hoteli Dodoma anapewa *special concession* na kadhalika. Sasa Mwanza mpaka leo haina hoteli ya hadhi ya nyota tano, na Mwanza ni jiji la pili katika nchi hii. Hivi ni lini sasa mambo kama haya tutatoa msukumo kwa mikoa hii iweze kuvutia watalii ambao ni sehemu kubwa mojawapo inayoiingizia pato nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri mambo haya ajaribu kuyawekea uzito mkubwa sana. Leo hii Mwanza utakuta kuna hoteli lakini ni hoteli

ambazo bado hazijafikia ile *class* kubwa, tunahitaji kuongeza msukumo zaidi ili kuweka msukumo mkubwa katika suala zima la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la amani na utulivu ni suala la msingi sana. Kuna chama chetu cha Wabunge kinaitwa Amani *Forum,* kimefanya kazi kubwa sana katika ukanda wa nchi za maziwa makuu. Kimesuluhisha migogoro katika nchi za Rwanda, Burundi, Uganda lakini bado chama hiki kinatakiwa kipewe msukumo mwingine mkubwa. Kumeundwa chama kingine ambacho kinaitwa *Inter-parliamentary Forum* ambacho kinahusisha mabunge yote ya nchi za Maziwa Makuu lakini bado Bunge letu halijapewa ushiriki mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kupitia bajeti hii Wizara yetu itusaidie sana kuvipa chachu vyama hivi ambavyo vina umuhimu sana katika kusaidia masuala mazima ya amani katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu. Napenda nipongeze vyombo vya habari vya *IPP*, Hivi sasa vyombo hivi vinatoa picha nzuri na taswira nzuri sana, kila baada ya taarifa ya habari ya hapa Tanzania wanatupa habari za nchi zinazohusika za Uganda na Kenya. Hii inazidi kutupa ufahamu na kujua nini kinaendelea katika nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii *East African Channel* ambayo inasaidia sana kutoa taarifa, ningeomba vyombo vingine vya habari vichangie zaidi katika suala hili kuwaelimisha Watanzania kwa sababu Dunia ya leo hatuwezi kukaa kama kisiwa lazima tujue kwa wenzetu kuna nini kinaendelea. Jana Mheshimiwa Rais alikuwa anahojiwa kwenye kipindi maalumu cha *straight talk Africa* na Shaka Ssali. Yeye alizungumzia, akasema kwamba katika maoni yake kama Rais ni kuona Tanzania inatoka katika nchi maskini kwenda kwenye nchi ambayo ina kipato angalau cha kati, ndio maoni ya Mheshimiwa Rais wetu. Sasa haya yote tunapaswa kuyaelewa na kuyaunga mkono, hatuwezi kufanya hivi bila kuweza kuona wenzetu wanafanya nini. Nakipongeza kituo cha *Star TV* kwa sababu kinarusha matangazo haya. Nina imani Watanzania walifaidika kumwona Mheshimiwa Rais wao akizungumzia masuala mbalimbali pale, haikuwa mchezo, tumpongeze kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni pamoja na mambo mengine kwa uwekezaji wa ndani kwa hii Samiro *Lodge* pale jijini Mwanza. Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tu Wizara hii Mheshimiwa Waziri ni Dr. Ibrahim Msabaha, Mheshimiwa Naibu Waziri ni Dr. Diodorus Kamala, aliyekuwa anachangia sasa hivi ni Dr. Chegeni atakayefuatia kuchangia ni Dr. Lucy Nkya na baada yake atafuatia Dr. Wilbrod Slaa.

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na mimi ningependa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na Katibu wake Mkuu na wataalamu wake kwa hotuba

nzuri ambayo kweli imekuwa ni ya kisayansi, hata kama kuna masahihisho au maulizo lakini basi ni kwa vile lazima tui-*discuss*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia nichukue fursa hii kuwapongeza Wabunge wetu wa Bunge la Afrika ya Mashariki, ninawapongeza kwa kupita kwa kishindo na kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na naamini kwamba wataenda kule wakiwa na moyo wa uzalendo kuhakikisha kwamba wanaiwakilisha Tanzania kwa maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nisiwasahau wajumbe wa Tume ya Profesa Wangwe ambao kwa kweli wamezunguka nchi nzima na kuhakikisha kwamba wanawapitia wadau wa aina zote kuhakikisha maoni ya Watanzania kuhusu mchakato wa *political federation* unakuwa na sura ya uelewa wa Kitanzania, nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na wataalamu wake, ningependa kutoa maoni yangu machache kwa nia njema tu. Kwanza, ningependa kuzungumzia kuhusu maoni ya Watanzania ambao asilimia 75 wamesema kwamba wasingependa kuwepo kwa mchakato wa haraka wa *political federation*. Tunaanza kujiuliza ni kwa nini Watanzania wafanye hivyo pamoja na kwamba kihistoria sisi Watanzania tumekuwa ni nchi ambayo kweli inapenda sana muungano na ushirikiano katika Bara letu la Afrika kwa ajili ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Watanzania wame-*react* vile kwa sababu ya historia ya kwanza ya Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyokufa wakati ule. Tulikuwa na ndege nyingi na tulikuwa na mali nyingi lakini wenzetu wakawa wajanja, wakawa wameturusha, kwa hiyo, Watanzania wengi bado wana madonda rohoni wanakumbuka yale yaliyotendeka. Wanajiuliza hivi itakuwaje sasa hawa watu wamebadilika, wamekuwa malaika kwa ghafla, na wanakuja tena ili tuwekeze pamoja halafu waje waturushe baadaye! Kwa hilo tunahitaji kutoa ushauri nasaha na elimu kubwa sana kwa Watanzania ili mwananchi wa kawaida aelewe kwamba huu mchakato au muungano wa kisiasa utakuwa na manufaa gani. Na sijui tutatumia lugha gani lakini ninaamini kwamba elimu ya kutosha kwa wakati muafaka inaweze ikawabadilisha Watanzania, lakini hata hivyo wengi watasema kwamba basi tumekubali lakini hatutaweza kusahau yaliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kitu kimoja ambacho nimekuwa nakiona na kinanipa wasiwasi mkubwa katika huu mchakato. Sisi Watanzania ni wapenda amani, ni watu ambao tunasema basi kama imekuwa hivyo na iwe hivyo, lakini wenzetu wana *speed* kubwa katika nyanja za biashara. Wenzetu wamekuwa ni wajanja kuliko sisi Watanzania katika nyanja za biashara. Kwa mfano, mimi huwa nasikitika sana, kama unasafiri nje unasikia kwamba Kenya ina-*export Tanzanite*, wakati machimbo ya *Tanzanite* hayapo kwao. Yapo wapi Arusha na si kwao. Ukienda Arusha wengi wameingia kule, wengine wanafikia mahali mpaka wanaamua kujifunza na lugha ya makabila yaliyopo mpakani ili waonekane kwamba ni Watanzania, hawana kibali cha

kuishi, hawalipi ushuru wa haya madini wanayoingia  nayo mpakani kwenye *panya roads*, wanaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni biashara ya matunda. Wakenya hawa wamefika mpaka Morogoro wananunua machungwa yakiwa bado maua kwenye mashamba ya wakulima wetu. Wanatoka wanakwenda ku–*export* haya matunda pamoja na ndizi za kutoka Kilombero kwa jina la Kenya. Sasa kama wameanza sasa hivi kutudanganya na kutufanyia mambo ambayo hayaeleweki bila maadili sembuse tutakapokuwa nchi moja; tutakapokuwa tunazungumza lugha moja; tutakapokuwa tuna mikakati ya pamoja ya kibiashara, *they are going to be smatter than Tanzanians.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia tatizo lingine lililopo kule mipakani kwa mfano, Mkoa wa Mara, wale kwa sababu wanazungumza lugha moja na Wakurya wa Tanzania, na Wajaluo, na wanajiona wamesoma kuliko sisi, na siyo kwamba wamesoma kuliko sisi ila *they have got the art of English Language*, kwa hiyo, wanapo-*cross* wanasema kwamba wao ni watu wa Mara. Wana-*cross* kwa sababu wana majina yanayofanana na Wachaga na majina ya Kinyakyusa. Wengine wanasema kwamba wao ni Wanyakyusa wanakuja Tanzania. Nenda kwenye mashirika ya nje kwa mfano Shirika la *Global Fund*, nenda Dar es Salaam kwenye hizi kampuni zetu za simu, inasikitisha wale vijana karibu wote walio wengi si Watanzania, wanatoka Kenya na Uganda *by the issue* kwamba wanaweza wakazungumza Kingereza, je, sisi Watanzania tunaonunua simu tunazungumza Kingereza wote? Sasa kwa nini tuwahitaji hawa ambao wanazungumza Kingereza? *It has been very difficult* kwa *immigration* kuweza kuwakamata kwa sababu anaitwa jina la Kijaluo, unamkamataje ikiwa sisi tuna Wajaluo? Na anakutajia kwamba anatoka  kijiji cha kutoka kule Sirari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri tunapokwenda sasa kwenye Muungano ni vizuri tukaangalia hizi tofauti zetu za kuwa waadilifu kwenye biashara, za kuwa waadilifu wa kuangalia wewe ni nani kwenye uraia. Wenzetu wa Uganda wanaingia wakijitia wao wanatoka Mkoa wa Kagera, lugha ni ileile na *morphology* ni ileile *how do we control them*? Sasa kwa mfano wakati kama huu inakuwa vile, tutakapokuwa sasa tumekuwa na Muungano inakuwaje?

Tatizo lingine linakuja kwa hawa wenzetu walioingia wapya nao wanasema kwamba ni watu wa Ngara, tunao wengi Morogoro hata *Immigration* wakienda kuwakamata  anakwambia kijiji cha kutoka Kigoma au Ngara lakini si Watanzania. Kinachosikitisha ni kwamba baada ya kuchuma wanaondoka, unauliza mfanyakazi wake unasema huyu bosi wako kaenda wapi anakujibu kuwa amerudi Rwanda au amerudi Burundi.

Nitoe  mfano Chuo Kikuu cha Mzumbe kulikuwa na vijana wanafanya kazi pale wamesomeshwa kwa fedha za Watanzania, wamepewa madaraka makubwa, baada ya Serikali ya Rwanda ku–*settle down* wameondoka *even without a courtesy,* bila kulipa hata zile gharama ambazo tumewasomeshea.

Sasa kwa wenzetu ambao *they seem to be smatter than us* kwa sababu sisi *by nature* tumezaliwa ni wapenda amani na wapenda wenzetu, tuna ule msimamo wa kwamba sisi ni Watanzania, sisi ni Waafrika na Afrika ni moja lakini mimi nasema kwamba wema wetu ukizidi kipimo tutafika mahali tutaanza ku–*regret they are going to overscheduled our people* kama siyo leo ni kwenye kizazi kijacho cha watoto wetu.

Mimi ninashauri jambo moja, katika kutengeneza hii *Political Federation* ile *Memorandum of Understanding* iweke wazi kwamba kilicho cha Mtanzania ni kipi, kilicho cha Mkenya ni kipi na maeneo ambayo tunaweza tuka-*integrate* katika katika *federation* hiyo. Bila kufanya hivyo tutakuja kulaumiwa na watoto wetu na siyo kulaumiwa tu ni pale ambapo watakuja kuwafanya watoto wetu watumwa kwa sababu hatutazungumza tena kwa sababu ni wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie upande wa usalama. Inasikitisha kwamba huu ujangili wote ambao umefanyika katika mabenki yetu mpaka tunaona kwenye magazeti yetu wanatangaza kwamba kuna wahalifu au majangili yametokea Kenya yameingia. Wameingia sasa hivi ambapo tuna *restrictions* mipakani kwetu, je, itakapokuwa hakuna *restrictions how do we handle them*?

Naomba niulize, hawa watu kule kwao uzalendo unakuwa ni wa kikabila, hivi sisi ni mchawi gani ambaye atatusaidia tutakapoungana nao? Ule uzalendo wa kitaifa uweze kurudi na aweze kuwaagua ili ule uzalendo wao wa kikabila uishe waanze kujifikiria kama Taifa la *East Africa* kama sisi Watanzania tulivyo sasa hivi? Na wao watakuwa ni wengi kuliko sisi, ukijumlisha *by numbers how do we influence them*? Mimi nafikiri Wizara ituambie kwamba kwenye huu Muungano ni michakato gani ya kuhakikisha kwamba usalama, uzalendo, mshikamamo utakuwa umejengeka *within the system ya federation*.

Lingine ambalo ningependa nishauri ni kwamba sasa hivi ili kuweza kupunguza mapunjo tunayoyapata sisi kama Watanzania ningependa Wizara ichukue *extra mile* ya kuweza kuwaelimisha Watanzania kuhusu hizi Kamisheni ambazo zimeanzishwa kuhusu ushuru wa forodha wa pamoja kwa sababu wafanyabiashara wetu wadogo wadogo hawaelewi huu ushuru wa pamoja ni kwa ajili ya nani ni kwa ajili ya wale wafanyabiashara wakubwa?

Sielewi. Naomba Watanzania tupewe elimu ya kutosha kuhusu yale mambo ya pamoja manne ambayo tumepangilia kwamba yatakuwepo *at which level,* kwa kiwango gani kwetu sisi kama taifa la Kitanzania tunashirikiana katika haya mambo manne ambayo tumesema kwamba tutakuwa tumeunganika? Ikiwa mpaka sasa hivi nimesikia kutoka kwa mwenzangu aliyechangia hapa kwamba bado miaka miwili Kenya itakuwa inalipa ushuru na sisi tutakuwa hatulipi ushuru; je, *are we going an extra mile* kuhakikisha kwamba na sisi tunaingia kwenye *balanced trade*? *How much*? Na kwa njia gani? Kama hatujaweza je, kuna uwezekano wa kuweza kuongeza huu muda wa ushuru wa pamoja kwa kiwango ambacho kiko sasa hivi kwa maelewano ambayo tunayo sasa hivi na kwa faida ya taifa letu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na mengineyo wanaiba mazao yetu, wanayachukua na hawalipi kodi, wanawanyanyasa wakulima wetu kwa kuwapa pesa kidogo kwa sababu *we are desperate for money*. Kuna njia za panya, mahindi yanakwenda Kenya halafu wanakuja wanatuuzia tena wakati tuna njaa, wanachukua machungwa na ndizi zetu wanakwenda kuuza.

Je, kuna uwezekano wa kutengeneza soko la mazao karibu na mipaka ili tuweze tuka *control* hii *movement* ya biashara ya mazao yetu? Je, kuna namna ambavyo tunaweza tuka – *control* hii biashara ya machimbo? Wengine wanakuja mpaka kula Morogoro, wapo wanachimba dhahabu yetu, wanachimba rubi zetu na wanakwenda kuuza kupitia nchini kwao na faida inakwenda kwenye nchi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu lakini kwenye Umoja ni lazima tuweke maslahi ya nchi yetu mbele, tuweke maslahi ya wananchi wetu mbele, ni nani anayefaidi? Kwa kiwango gani? *How do you control it? Balance* iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ndicho ninachokiomba na na ningeomba pia kwa sababu mpaka sasa hivi kwenye viwango vyetu vya elimu ya juu tunatofautiana kwa sababu wao wana vyuo vikuu vingi na tuna-*export* wanafunzi kwenda kule kule kwao kusoma. Yaani wanasoma kule kwao na watoto wetu wanapokwenda kusoma kule wanakwenda kwenye vyuo ambavyo ni *sub-standard,* hawaruhusu kuingia kwenye vyuo vyao ambavyo ni vya pesa za juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo haya yote tunayaona, tunawezaje tukaweka uwiano kwamba kama sisi tunaleta watoto wetu kusoma kwenu je, kiwango chao cha elimu mnachowapa kinafanana na cha watoto wa kwenu? Inasikitisha kuona kwamba kuna watoto ambao wanasoma Uganda wengi tu wakati tuna sekondari nyingi hapa nchini. Hivi kama Taifa tunaweza tuka – *control* hii *movement* ya watoto hata mpaka wa *kindergarten* kwenda kusoma Uganda? Itafika mahali wao watakapokuwa ni nchi moja basi wataamua kwamba wao wamejenga shule nyingi, na ninyi kwa nini msipunguze *speed* kwa sababau shule zinatosheleza. Nafikiri kwenye huu mkataba wetu wa muungano hili liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni kwenye hili soko la ajira. Nimepata ki – *note* hapa kwamba Wakenya wameingia mpaka Njombe wanasomba mbao zetu kule na hizi mbao wanakwenda kuuza kupitia Mombasa na wanasema zimetoka Kenya, sasa hiyo misitu waliyonayo iko wapi? Tukiwaruhusu kuingia watatumalizia misitu, watamaliza madini yetu na watamaliza kahawa yetu, watachukua kahawa, watachukua karafuu. Mimi sijaona Mombasa kumepandwa karafuu lakini wanauza karafuu, wamelima wapi? Sasa kama sasa hivi wanatuibia *how do we control them* tunapokuwa sasa na *Political Federation*? Wakati Rais atakuwa ametoka kwao huko labda, Waziri wa Biashara atakuwa ametoka kwao, tunawafanyaje hawa? Mimi naomba hilo Mheshimiwa Waziri atueleze kwamba *control mechanism* ikoje? Hilo ni ombi langu tu.

Baada ya kusema hayo, nimechangia kwa nia njema, naomba niunge mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushuru sana Mheshimiwa Lucy S. Nkya. Mheshimiwa Peter Serukamba atakuwa wa mwisho mchana wa leo lakini atatanguliwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe, lakini kabla ya Mheshimiwa Zitto ataanza Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa. Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa karibu!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijasema naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto ambaye jana aliteuliwa na Kamati Kuu ya CHADEMA kuwa Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA. Pamoja naye ni Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugezi wa Kurugenzi ya Rasilimali na Uchumi. Nawatakia mafanikio katika kazi yao mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili niweze kuchangia vizuri naomba nianze na kunukuu Katiba kwa ruksa yako. Katiba yetu katika Utangulizi inasema: "Kwa kuwa sisi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayozingatia misingi ya Uhuru, Haki, Udugu na Amani…" Niende pia kwenye Ibara ya 8 ya Katiba yaani Ibara ya 8(1)(a) inayosema: "Wananchi ndio msingi wa Mamlaka yote na Serikali itapata Madaraka na Mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii… " Baadaye nitafafanua kwa nini nimesema haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sipendi kuzungumza kwa nadharia, ingekuwa kuna uwezekano ningekataa bajeti hii leo, nitaiunga tu bilioni 8 za Wizara hii kwa sababu moja kwamba tunahitaji Wizara hii iratibu yale mambo ya mpito ambayo tunataka yafanyike lakini ingekuwa ni suala la *federation* mimi ningekataa hata hizi bilioni 8 ziende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza kwa hali halisi katika misingi miwili, kwanza, biashara. Kule Karatu sisi tumekwishaonja joto la jiwe linalotokana na mipaka tuliyofungua. Sasa kwa maelezo ya kwamba tuko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Shirikisho tumeshafungua *Customers Federation* imeanza kazi, watu wako huru kupita wanaweza kuingiza na kununua kutoka kwetu wanavyotaka. Wenzetu wa Kenya wameingia wako kwenye vijiji vyangu 8, kule Tarafa ya Eyasi vijiji vinavyoitwa Dumbechand, Djiobaj, Mbuga Nyekundu, Qanded, Laghangareri, Malekichand, Endamaghang na Barazani ni maeneo yanayojulikana kwa kulima vitunguu katika Afrika Mashariki nzima. Vitunguu vyetu vyote vinauzwa katika nchi hii lakini viko Kenya, vinauzwa Uganda, Rwanda na Burundi lakini viko mpaka Uarabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndugu zetu wamekwenda mpaka katika vijiji hivi, wao wamenunua mashamba tayari kinyemela. Wamekuja na mfumo wanauita mfumo wa kununua vitunguu kwa kitu wanachokiita Neti, sina hakika Watanzania wangapi wanaelewa hiki kinachoitwa Neti. Sisi kwetu tumezoea kutumia magunia,

wamekuja na kitu kinaitwa Neti. Neti inaweza kubeba zaidi ya magunia mawili kwa pamoja lakini inafananishwa kwa bei ya gunia moja, huu ni unyanyasaji wa wakulima.

Wakienda kwao kwa taarifa niliyonayo, sina hakika na taarifa hii, naambiwa kwamba wanakwenda kufanya *packaging* ya vitunguu vyetu, wanasafirisha kwenda Uarabuni kwa *packaging* ya kwao, wanapata karibu magunia matatu, wamemnyonya Mtanzania mkulima maskini asiyejua haya. Naomba Wizara na Serikali na haya si ya Wizara hii, ninapozungumzia hapa sizungumzii tu Wizara ya Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, nazungumzia Serikali katika ujumla wake kwa sababu ni mfumo mzima tuliouweka.

Sisi Halmashauri tumeingilia suala hili, mkoa umeingia na unasema hapana, ni biashara huria waachieni wenzenu. Naomba Serikali iende ikaangalie mazingira yale wakulima wetu wamenyanyasika, tunataka miongozo sahihi, tunataka vitunguu viuzwe na mali yote aliyosema Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya iuzwe kwa manufaa ya Mtanzania na siyo kwa manufaa ya mtu mwingine wa nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nimesema hilo la biashara naliacha kwa sababu ya muda, nigusie kidogo katika maeneo ya ajira. Sizungumzii kwa nadharia naomba Serikali ifanye tathmini na nitapenda nipate tathmini ya kina ndani ya Bunge hili katika nafasi muafaka.

Naomba ama Wizara hii au Wizara inayohusika na ajira inipe taarifa na nitapenda Waziri wa Ajira anipe taarifa. Ni Wakenya wangapi wako kwenye mahoteli yetu yaliyopo kwenye ukanda wa Karatu? Mnafahamu wote kwamba Karatu ina hoteli nyingi za kitalii. Sitaki kuzitaja majina hapa kwa sababu ya biashara lakini kuna hoteli zimejengwa kule maeneo yetu walikuja wakaomba ardhi, tumewapa ardhi kwa maelewano kwamba wanavijiji wanaotoa ardhi watapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchungu mkubwa leo nasema wananchi wetu walipopeleka maombi ya ajira wote walikataliwa hata uhudumu. Hivi tunapofika mahali hata mhudumu na mfagiaji, mbeba masanduku anatoka Kenya, hii itakuwa ni nchi ya aina gani? Mbeba masanduku? Na walikuja mimi nilikwenda na *DC* wangu wakatuambia Mheshimiwa Mbunge mimi mwenye hoteli sitakubali nipate hasara kwa sababu mzungu anayekuja anataka sanduku lake libebwe na mtu anayeelewa Kingereza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipokuwa makini nchi hii itakuwa hata kazi ya kubeba masanduku hatutakuwa nayo tena, sasa tutakuwa nani? Watumwa ndani ya nchi yetu! Tunahitaji tuwe makini, mengine tunayafanya kwa nadharia lakini mimi nimesema sitaki kufanya kazi kwa nadharia, haya ni ya kweli nimekasirika na *DC* wangu tumeondoka na kwenda kuongea na wenye hoteli wanatuambia Mbunge maombi kweli tunayo hapa lakini hatuna hata mmoja wa *form four* wala *form six* katika kijiji chako, kwa hiyo tunachukua kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwaambia kwamba hivi mnanunua hata kuku, hata nyama ya *beef* na ya nguruwe kwa sababu mahotelini wanakula nguruwe, wasiotumia nguruwe wanisamehe; mnakwenda kuchukua nyama nje? Wakaniambia, Mheshimiwa

Mbunge watu wako hawana *quality* na wala hawana *standard* ya kuzalisha kuku, wala nguruwe, wala ng'ombe ni *beef* gani tutachukua Tanzania? Kule kwangu nina zaidi ya hoteli 7 za kitalii katika Wilaya ya Karatu. Hayo ndiyo tunayosema yangetoa ajira kwa Watanzania, lakini ajira hizo zote zimekimbia. Haya hatuyaongei tu kwa sababu tuyaongee lakini tunaongea kwa uchungu kwa sababu Tanzania tunaipenda. Nimeyazungumza ya Karatu nina hakika yalivyo katika maeneo yote ambayo yanazunguka maeneo yetu. Arusha mjini ukifanya tathmini nina hakika hali ni hiyo, Moshi pia na hata Mwanza hali itakuwa ni hivyo hivyo. Naomba niachie katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Profesa Wangwe na timu yake kwa kazi nzuri waliyoifanya, lakini wametuambia kitu kizuri sana hapa kwenye Ibara ya 145 ya taarifa yao, wanatumbia, lakini sijapata muda wa kusoma kwa sababu tumegawiwa asubuhi hii. Kwenye Ibara ya 145 Watanzania wamesema hawana elimu ya Afrika Mashariki, hawaelewi hata hicho mnachokiita kwamba tunataka sisi *federation.* Watanzania hawaelewi ndiyo maana ya kunukuu Katiba. Unapozungumzia umoja wa nchi tatu au nchi tano sasa ambazo tumeongeza Rwanda na Burundi unazungumzia kuhamisha mamlaka na unabadilisha mfumo wa utawala, Tanzania inakufa, Tanganyika inakufa, Zanzibar inakufa na hatimaye tunakwenda kuwa na Afrika Mashariki.

Watanzania ni lazima wao wawe waamuzi wa kitu hiki hawawezi kuamua kama hawana elimu ya kutosha. Waliopitia katika Ibara ya 145 hapa tunaambiwa wamesema hawana elimu ya kutosha, kwenye Ibara ya 148, anasema wengi wa Watanzania hawana hata ujasiri na uthubutu wa kueleza maoni yao. Ni mambo mazito haya tunazungumzia mwaka 2013 tuwe na Rais wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sitaunga mkono pendekezo hilo na ninaomba Waziri aniambie na ninapenda kusema suala hilo uamuzi wa viongozi si maamuzi ya Watanzania na ninapenda kusema kwa kauli yangu kama wataniunga wenzangu mimi nitashukuru na ninaomba niwashawishi, suala hilo lisitishwe, Urais wa Afrika Mashariki utokane na maamuzi ya Watanzania. (*Makofi*)

Viongozi watatu hawawezi wakakaa wakasema mwaka 2013, miaka sita ijayo tuwe na Rais wa Afrika Mashariki wakati Watanzania hawakupiga kura, hawajaona Katiba ya hiyo Afrika Mashariki. Hatuwezi kwenda tukaingia kwenye Afrika Mashariki hatujui mfumo wa utawala wa hii Afrika Mashariki; hatujui Kanuni zitakazoongoza; hatujui Bunge hilo litakuwaje; hatujui hizo Mahakama pamoja na hii tuliyonayo leo hatujui mfumo huko mbele utakuwaje, majeshi yatakuwaje. Tunakwenda kuingia kwenye kitu ambacho hatuna uhakika nacho. Ndani ya Bunge hili asimame Waziri leo aniambie rasimu ya Katiba tunayotaka kwenda kumchagulia huyo rais wa mwaka 2013 iko wapi? Na nitapenda anipe jibu wakati wa vifungu vya Katiba na rasimu ya Katiba ambayo tunakwenda 2013 yaani miaka sita ijayo. Iko wapi hiyo rasimu ya Katiba ambayo leo tunasema tunataka kwenda kuchagua rais wa Afrika Mashariki.

Tunachukua wimbo wa Afrika Mashariki, naweza kuvumilia wimbo lakini tumeuzindua kana kwamba tayari tuna Serikali na tuna nchi inayoitwa Afrika Mashariki. Hatukuwashirikisha wananchi tumezindua wimbo hata ulivyopatikana sijui kama tunafahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafanya utani na mambo mazito yanayohusu utawala wa nchi yetu. Kuna mwenzangu ameeleza hapa kwamba ulaya walianzia hivyo lakini walikwenda na mchakato, miaka miwili, sasa jumuiya ya ulaya bado wanahangaishana kuhusu Katiba, Uingereza wanasema hatuwezi kuingia, hela yetu tunataka kubaki na sura ya Malkia wetu, kitu kidogo sana sura ya Malikia. Sisi Tanzania tunasema kwamba tutaingia kule kichwa kichwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuendelea nigongewe kengele, ninapenda kusema kwamba sina tatizo na *customs union,* biashara sisi hatuwezi kuwa kisiwa ni lazima tuingie kwenye ushirikiano yaani ni lazima tufanye biashara. Sina tatizo na kutengeneza mkakati wa muda mrefu tukawa nchi moja katika Afrika Mashariki lakini ni hatua kwa hatua na hatua iliyodhibitiwa na hatua ambayo wananchi wameiunga mkono siyo hatua ambayo viongozi wanaiunga mkono peke yao. Wabunge tumejadili ndani ya Bunge hili Shirikisho kwa nusu saa kama mnakumbuka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili ni zito, naomba Waziri atupe maelezo ya kina baadaye, vyombo au *instruments* ambazo zinakwenda kwenye kitu hicho ziko wapi? Watanzania wameelimishwa kiasi gani? Na *referendum* au upigaji kura wa kwenda kupata Rais huyo zitafanyika kwa utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumalizia sitaunga mkono hoja mpaka nipate maelezo ya kina.

**MWENYEKITI:** Tunakushuru sana Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kwa kuunga mkono na sasa Kabwe Zuberi Zitto, na msemaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba.

**MHE. KABWE ZUBERI ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii ambayo kwangu mimi naiona ni Wizara muhimu sana kwa nchi yetu lakini pia wakati nachangia hotuba hii nitoe pongezi zangu za dhati na niwakumbuke mashujaa wa Taifa hili ambao walikwenda zaidi ya mipaka ya makabila yao na kuongoza makundi kwa makundi ya makabila ya Tanzania, akina Kinjekitile na kadhalika ambao waliona mbali, waliondoa hofu na wakaangalia ni jinsi gani ya kujenga taifa lililo imara lisilo na hofu na linaloangalia mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba *Chief Whip* wetu wa Kambi ya Upinzani hajanipa maelekezo yoyote kwamba hii ni *three line whip*, kwa hiyo, naamini kabisa kwamba tunatoa maoni huru bila kujali msimamo wa kambi wala kujali msimamo wa kibunge au wa Serikali.

Mimi ni mmoja wa Wabunge wambao tupo *on record,* ni mmoja wa watu ambao tunasema tunataka Shirikisho sasa. Nina sababu za msingi za kutaka hivyo na naamini kabisa kwamba watu wote ambao hawataki shirikisho sasa kwa sababu ya elimu yetu ndogo, kwa sababu ya kuogopa ajira, watu hao wana hofu. Ni hofu ambazo mimi naziona zitaliangamiza hili taifa, tutaendelea kuwa nyuma na tutakuwa ni watu ambao tunawafuata wengine wanataka nini, na ili nchi iweze kuwa imara ni lazima tu – *take a lead.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hizi tano za Afrika Mashariki sasa hivi zina jumla ya watu milioni 112, zina ukubwa wa uchumi wa jumla ya dola bilioni 36.3 ukiongozwa na uchumi wa Kenya kwa dola bilioni 16, uchumi wa Tanzania kwa dola bilioni 10.9, uchumi wa Uganda kwa dola bilioni 6.8, uchumi wa Rwanda dola bilioni 1.8 na uchumi wa Burundi dola 0.7 bilioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi hizi tano Tanzania ndiyo nchi nzee, yaani *The oldest Country,* ukichukua nusu ya wananchi wa nchi zote hizi za Afrika Mashariki, nusu ya Watanzania wana chini ya umri wa miaka 18, lakini nusu ya Waganda wana chini ya umri wa miaka 14, nusu ya Wanyarwanda miaka 17.5, nusu ya Warundi miaka 17, nusu ya Wakenya miaka 17.9. Kwa hiyo, Uganda ndiyo the *youngest nation* ndani ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini itakapofika mwaka 2050 Uganda watakuwa na jumla ya wananchi milioni 127, ndiyo taifa litakalokuwa na watu wengi zaidi kuliko mataifa mengine yoyote ya Afrika Mashariki, ni kwa sababu ndiyo *the youngest nation*, kwa hiyo, *fertility* yao iko juu sana na ndiyo sababu Waganda wanataka shirikisho.

Waganda wana ajenda, wanajua itakapofika mwaka 2050 watakuwa ni wengi sana na ardhi yao itakuwa ni ndogo, wanataka eneo kubwa zaidi waweze kusambaa zaidi. Sisi inawezekana kabisa kama taifa hatujui ajenda yetu tunataka nini ndani ya shirikisho, ndiyo maana tumejawa na hofu, tumejawa na hofu za ajira, tumejawa na hofu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nataka nitoe mfano mmoja. Mwaka 1971 wakati Nduli Idd Amin alipompindua Dr. Obote, Uganda ilikuwa na Chuo Kikuu kimoja yaani Makerere *University*. Mpaka mwaka 1986 baada ya mwanamapinduzi Yoweri Kaguta Museven kuchukua Serikali ya Uganda na kui–*stabilise* Uganda, ilikuwa na Chuo Kikuu kimoja. Sisi tulikuwa na Chuo Kikuu kimoja na mwaka 1984 tukaanzisha *SUA* yaani tukawa na vyuo vikuu viwili.

Leo hii Watanzania wanasimama wanalalamika wanasema Uganda wanatuzidi kielimu, ni aibu kubwa. Kwa sababu Uganda hii ambayo tulikwenda kuisaidia tukaikomboa mpaka mwaka 1986 walikuwa na Chuo Kikuu kimoja lakini sera sahihi za *National Resistance Movement* chini ya uongozi wa Rais Museveni zimeifanya Uganda sasa hivi Taifa ambalo lina wasomi wa kutosha licha ya vita walivyonavyo, licha ya kuwalaumu na ukabila wao lakini wamevijenga vyuo vikuu vingi zaidi vya umma na vya binafsi. Sisi bado tunalalamika elimu ni ndogo kwa sababu ama ya kutokuwa na sera sahihi ya kutokujiandaa na kutokuona kwamba tunakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa soko la pamoja. Jana nikiwa kama Waziri Kivuli wa Uchumi nilitoroka kidogo kwenda kwenye Kikao cha Kamati Kuu ya CHADEMA. Nikaenda kutembelea moja ya viwanda vikubwa kabisa Tanzania ambavyo vimewekezwa na watanzania wenyewe kinaitwa, *East Coast Oil and Fats Limited*. Kiwanda hicho peke yake kina-*saturate* soko la sabuni na mafuta nchi nzima na kinazalisha kwa uwezo wake wa asilimia 30 tu yaani ile *production capacity* asilimia 30 tu. Wanahitaji soko zaidi, wanahitaji wauze Rwanda, Uganda, Kenya na wanahitaji wauze Burundi, soko la pamoja ambalo lina sheria zilizo wazi ambalo lina taratibu zilizo wazi ambalo linaondoa ukiritimba na ni moja ya njia pekee ya kuweza kufanya viwanda ambavyo vinaendelea kuwekezwa hapa nchini viweze kupata masoko katika nchi ambazo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza sana watu wa *East Coast Oil and Fats Limited* kwa kuweka kiwanda kikubwa sana ambapo moja ya malighafi zake ni mawese ya kutoka katika Mkoa wa Kigoma. Mimi kwa kweli kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge wengine kutoka Kigoma itabidi tufanye kazi ya ziada ya kuweza kuhakikisha kwamba tunawapelekea hiyo malighafi ili watu wetu nao waweze kufaidika na uwekezaji huo mkubwa ambao umefanywa na Mtanzania huyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na lawama kwamba Bunge la Afrika Mashariki kwamba linaripoti kwa nani. Lakini mimi nafahamu kwa mujibu wa taratibu na nilikuwa naongea hapa na Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, kila mwaka Bunge la Afrika Mashariki linatoa ripoti yake kwenye Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje. Kwa hiyo, ili tuweze kujua kwamba Bunge la Afrika Mashariki linafanya namna gani kazi ni lazima Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje ilete ripoti yake ndani ya Bunge hili ndiyo tuijadili kama sehemu ya ripoti ya Kamati. Kwa sababu hakuna utaratibu kwa Bunge la Afrika Mashariki labda Spika wao au nani waweze kuja hapa na kutoa hiyo ripoti yao. Kwa hiyo, mimi nadhani ni wakati muafaka pia Waheshimiwa Wabunge, wajaribu kuangalia kwa sababu wanaweza kuwa kwenye Kamati nyingine, wasiwezi kujua Kamati nyingine inafanya nini? Lakini ninaamini kabisa *EALA* inaleta ripoti yake kama taratibu ambazo zinatakiwa na *EALA* Tanzania wana ofisi katika Ofisi ndogo ya Bunge Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kufuatana na umuhimu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na huko tunakokwenda Sheria nyingi za masuala ya kibiashara hazitakuwa zinaamuliwa na Bunge la Afrika Mashariki. Kwa mfano, leo sisi hatuna mamlaka ya ku-*change* sheria yoyote inayohusiana na Ushuru wa Forodha, yaani *customs.* Kwa sababu sheria hii sasa ipo chini ya *Custom Management Act* ya Afrika ya Mashariki ndiyo wanatunga Arusha na tunavyokwenda sheria nyingi zaidi zitakuwa zinatungwa na Bunge la Afrika Mashariki kuliko kutungwa na Bunge hili hasa hasa kuhusiana na masuala ya kibiashara. Kwa hiyo, Bunge la Afrika Mashariki ni Bunge muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba nitoe maoni na Mheshimiwa Waziri ayachukue ili wajaribu kuwasiliana na wenzao wa Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi Bunge hili liwe *expanded* liongezeke, liwe kubwa na tuangalie utaratibu

ambao watanzania wataweza kupiga kura moja kwa moja kuwachagua Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. Hii itasaidia sana kufanya hiyo elimu kwa sababu tutakapokwenda kwenye uchaguzi Vyama vitaweka Wabunge wao na kwa vyovyote vile njia pekee katika hili ni kutumia uwakilishi wa uwiano (*proportional representation)*. Kwa hiyo, kama kuna watu 10 ambao Tanzania inabidi iwapige kura, kila chama kitatengeneza orodha yake ya watu 10, itaenda kwa wananchi, tutajenga hoja zetu kila Chama kitasema msimamo wake wa kuhusu Afrika Mashariki ni nini. Kwa hiyo, ile itasaidia wananchi kuweza kupata uelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza kuwa na aina mbili ya Waheshimiwa Wabunge katika Bunge la Afrika Mashariki. Kundi la kwanza, wawe ni Waheshimiwa Wabunge ambao ni sawa kwa kila nchi. Kwa maana kama wanasema ni Waheshimiwa Wabunge 9 ni kwa nchi zote na wengine wagawiwe kutokana na idadi ya watu ya kila nchi na wananchi wapige kura moja kwa moja *through proportional representation* na hii itasaidia sana kuhakikisha kwamba Jumuiya inafahamika kwa urahisi zaidi kwa wananchi. Kwa sababu huko tunakokwenda sheria nyingi zitatungwa na Bunge la Afrika Mashariki kuliko kutungwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tupo kwenye Ushuru wa Forodha, tunaanza soko la pamoja haraka iwezekanavyo. Kutokana na majukumu mengi yanayoongezeka, napendekeza kwamba sasa Sekretarieti ibadilishwe na kuwa *commission,* iwe Tume iweze kufanya *Management* ya yale mambo ambayo tutashirikiana kwa pamoja. Kwa mfano, tutakwenda kuwa na *foreign policy*, *common defence policy, common higher education policy*, kwa ajili ya kuweza kuondoa hizo tofauti za Elimu ya Juu katika nchi mbalimbali na tutakwenda kuwa na *Common Trade and Investment Policy*, nilikuwa naomba uangaliwe uwezekano wa kufanya mchakato wa Sekretarieti ya Afrika Mashariki iweze kuwa Tume na kuweza kuhakikisha kwamba sasa *Arms* zile tatu kwa maana *Summit, Councils of Ministers* na *Secretariat* kuwa kama *Executive* na *EALA* iwe na nguvu yake jinsi ambavyo inavyotakiwa na Mahakama iweze kuwa na nguvu yake inavyotakiwa.

La mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Mheshimiwa Siraju Kaboyonga kuhusu *EPA*. Nafahamu Mheshimiwa Waziri juzi juzi hapa alikwenda *Brussels* kwa ajili ya suala hili la *EPA*. Niko kwenye *on record* katika Bunge hili na leo ninazungumza ni mara ya saba kuhusiana na suala la *EPA*. Tulizungumza kwamba hatuwezi kuwa kwenye *Customs Union* mbili ni lazima tuwe kwenye *Customs Union* moja. Nafahamu kwamba Wakuu wa nchi walipokutana kule Kampala mwaka 2003 walikubaliana *negotiation* ya *EPA* ifanywe kama Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Waganda na Wakenya wakaamua kwenda ku-*negotiate through ESA* ambayo ni sehemu ya *COMESA* na sisi tukaenda *SADC*. Kwa hiyo, hiyo ni historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini natambua kuna juhudi ambazo zimefanyika na *Council of Ministers* ikamtuma Mwenyekiti wake Mheshimiwa Elia Kateganya kutembelea kwa Wakuu wa Nchi kwa ajili ya kuomba ridhaa ili *East Africa Community* iwe ni *focal point* kwa ajili ya *EPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa Waziri wa Biashara wa Kenya ndugu Mukhisa Kituyi akaenda kinyume na maamuzi ya *Council of Ministers of East Africa.* Akaandika barua *Brussels* kusema kwamba wao Kenya hawataki *EAC EPA*. Ndipo hapo nasema lazima tu- *take a lead* tuna uwezo wa kuwa na EPA ya Afrika ya Mashariki bila ya kuwa na Kenya. Tunao uwezo kama Kenya wao wanaona kwamba ESA ndiyo *group* ambayo itawafaidisha *let them go,* tuwe na *EPA* ambayo *minus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika hiyo *EPA minus* Mheshimiwa Waziri na bahati nzuri yeye ni mwanafunzi wa *Strategic Studies*, nchi ya *DRC* tusiiache. Tufanye utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunaichukua *DRC* inakuwa ni sehemu ya *EPA* kwa bahati nzuri *DRC* yenyewe imekataa kusaini *EPA* na kundi lolote lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina mahusiano mazuri sana na *DRC*. *DRC* ni soko nzuri sana kwetu, tufanye utaratibu, tutume ujumbe kwenda kwa Mheshimiwa Rais Kabila waende wakamwombe hata kama hawi Mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, aje ashiriki katika *East African Community EPA* ili iweze kutusaidia kwa sababu sisi yale ndiyo masoko yetu. Rwanda, Burundi na *DRC* ndiyo masoko ya Tanzania lakini pia tunawaweza.

Rwanda, Burundi na *DRC* sisi tunawaweza. Inawezekana Kenya hatuwawezi, lakini hao wenzetu tunazungumza nao Kiswahili kizuri, tunawasaidia kwa njia mbalimbali. Mheshimiwa Rais Kabila ni mtu ambaye ameishi Tanzania na amesoma Tanzania. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba tukiweka utaratibu wetu mzuri tukatuma *delegation* nzuri kule Kinshasha tunaweza tukaifanya *DRC* ikawa nasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawambia baada ya muda mfupi sana *EPA* yetu itafanya kazi, Wakenya watakuja wanapiga magoti kuomba kurudi kwenye *EPA* kwa sababu itakuwa ni *successful,* kwa sababu ni *Customs Union* tayari, *COMESA* siyo *Customs Union*. Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri tusiburuzwe na mtu anayeitwa Mukhisa Kituyi. Naomba kabisa Mheshimiwa Waziri akienda Arusha akikutana naye amwambie kwamba Waheshimiwa Wabunge wa Tanzania hawataki kuburuzwa na mtu anayeitwa Mukhisa Kituyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na nitasubiri majibu Mheshimiwa Waziri atakayotoa ndipo niweze kuamua kama nitaunga mkono hoja hii ama sitaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwangu mimi ni Wizara muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Kabla sijaanza nianze kwa kumshukuru Waziri ametoa hotuba yake nzuri sana na imeandaliwa vizuri. Nadhani kwa sababu umesema ni Wizara inayoongozwa na Madaktari, kwa hiyo, sishangai kuona mambo yanakuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kuanzisha ushirikiano huu mpya wa Afrika Mashariki, kwanza ni kuondoa umaskini na kukuza uchumi wa nchi zetu. Tukianza kuamini hapo mambo mengi sasa ni rahisi kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza niwapongeze Waheshimiwa Marais wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuanzisha Wizara mahususi kwa ajili ya kushughulikia mambo ya Afrika Mashariki. Kwenye *partnership* hizi ni sisi peke yake *East Africa* tumeweza mpaka kuanzisha Wizara. Sasa nataka Waziri anisaidie. Kuanzisha Wizara zetu pamoja na mambo mengine lazima wananchi wetu wa nchi hizi zote wajue umuhimu wa ushirikiano huu. Umuhimu wa kuufahamu ushirikiano huu kwanza naangalia bajeti hii. Nikiangalia bajeti ya Wizara ni ndogo sana. Naanza kujiuliza, hivi kweli tunafahamu maana ya Wizara, maana hii Wizara ndiyo *focal point* ya *Economic Development* ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara hii kama tukiipa bajeti ndogo maana ya kwanza ni kwamba haitaweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Watanzania wetu hawatafahamu maana ya *East Africa Community.* Matokeo yake ndiyo maana watu leo ukiwauliza hawajui maana yake. Ndiyo zinaanza kuwepo hizo hofu ambazo mimi sizioni kama zina msingi wowote. Ni kwa sababu tu watu hawajafahamu vya kutosha. Kwa hiyo, unaweza kuona watu hawajafahamu vya kutosha sababu ya bajeti kidogo inayopewa Wizara hii. Najua hapo nyuma Naibu Waziri amezunguka sana akiwa anafanya kazi ku-*sensitize* wananchi umuhimu wa *policy federation.* Mimi nilidhani ilitakiwa tutumie muda mwingi sana kuwaambia wananchi waelewe umuhimu wa *customs union* katika maendeleo ya nchi yetu. Waelewe umuhimu wa *common market* katika maendeleo ya nchi yetu, umuhimu wa kuwa na *common currency then* baadaye ndiyo tuanze kujadili ushirikiano wa kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu mimi la muhimu zaidi ni *common market*, ni ushuru wa forodha na *common currency,* haya ndiyo ya muhimu. Huu ndiyo uchumi. Kwa hiyo, mimi ninaomba sana wenzetu watusaidie sana, wafanye kila linalowezekana kuwaambia wananchi wetu umuhimu wa haya mambo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza hii kazi inafanywa na nani? Kazi hii inafanywa na Wizara yenyewe, Waheshimiwa Wabunge wa *East Africa*, Sekretarieti ya *EAC*? Mimi kwa mawazo yangu ningetamani sana Mheshimiwa Waziri baadaye jioni aniambie anaoanisha namna gani haya makundi matatu kwa maana ya Wizara, maana ya Bunge la *East Africa* na kwa maana ya *Secretariat* kufanya kazi ya kuwaambia Watanzania ama wananchi wote wa *EAC* kuelewa umuhimu wa *East Africa Community*. Kuhusu hili nadhani Mheshimiwa Waziri atwambie ana mkakati gani wa hayo makundi matatu yote yafanye kazi ya namna moja. Mimi siamini tuwachukue Waheshimiwa Wabunge hao waende Arusha, wakitoka Arusha hawana kazi. Wanayo kazi kubwa baada ya kwenda Arusha kuwaambia watanzania, tuwaingize kwenye programu watanzania hao wajue umuhimu wa *EAC* kwa maendeleo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuongelea suala ambalo wenzangu wengine wameliongelea, ni suala la kuingia kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, Rwanda na

Burundi. Kwa Watanzania tunahitaji Warundi, Wayarwanda na Wakongo kuliko hata Kenya na Uganda. Huko ndiko kwenye uchumi wa Tanzania. Bahati nzuri Waziri kwenye *page* 46 ameonyesha biashara tunayofanya na Burundi na Rwanda. Ukiangalia mauzo yetu kwenda Rwanda ni bilioni 21, lakini wao kwetu wamenunua bilioni 1.2. Huwezi kuliacha hili soko kama unaangalia mbali kibiashara. Tuchokiuza Burundi ni bilioni 46, walichonunua kwetu ni milioni 834. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge hivi unahitaji nini tena kama siyo soko hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marehemu Mwalimu Julius Kambarage siku moja alisema wakati akiwa kwenye *South Africa Commission* kwamba tunakokwenda huko siku zijazo Wachina wataongoza dunia hii, lakini sababu kubwa ni kwa sababu ya *population,* kwa maana wanaweza wakauziana wenyewe. Kama mnataka Watanzania tubaki tunaanza kushindana wenyewe hapa tuko kwenye *box* ya hiyo nchi inaitwa Tanzania hatuwezi kuendelea. Kongo ya Mashariki yote kwenda Kinshasha ni mali kuliko kuja Tanzania. Kwa hiyo, lazima tuwe *aggressive* ku-*make sure* Kongo inaingia huko. Pale ndipo kwenye ukombozi wa nchi yetu na tunavyoanza kuongelea kukuza viwanda vya ndani soko lake lipo hapo sasa. Mheshimiwa Siraju Kaboyonga alisema tumeua leo *General Tyre*, lakini *General Tyre* ilipaswa ifanye vizuri zaidi kwa sababu tunalo soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kuna mambo tunafanya hapa mimi sielewi, lakini ninachotaka kusema ndugu sisi watanzania tunawahitaji Warundi zaidi na Wayarwanda na Wakongo kuliko Kenya na Uganda. Kwa hiyo, mimi ninaunga mkono nchi zilizokubali hao waingie kwenye *East Africa Community*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo ya kwamba nchi zao hazina amani yatakuwa *solved* na *East Africa Community.* Tukianza kushirikiana nao tutawapelekea namna mpya ya kuishi na sisi tutakuwa tumechangia kupeleka amani Burundi. Kwa nini tufanye kazi ya kuwapokea wakimbizi tu. Haiwezekani siku moja tukakataa wakimbizi haiwezekani. Lakini tukiwaingiza kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki na wao watajifunza *culture* mpya ya kuishi pamoja. Lakini wakati wanajifunza sisi tunatengeneza fedha nchi yetu inasoga mbele tunaweza kufanya shughuli zetu za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo wenzangu wameliongelea vya kutosha ni suala la hii *EPA federation.* Mimi naomba nichangie kidogo kwenye hili suala. Nadhani kwangu mimi hili suala ni la umuhimu sana. Sisi Watanzania tupo kwenye *SADC* na kuna nchi karibu 18 za *SADC*. Wenzetu wa Uganda na Kenya wapo kwenye *ESA* hiyo ya *COMESA.* Sasa leo *South Africa* wameanzisha *EPA* wanakwenda *straight* na nani na EU ambayo *TDCA*. Lakini tayari Botswana, Namibia, Lesotho na Swaziland wanaondoka kwenye *SADC* wanakwenda kujiunga na ile ya *South Africa*. Tayari Zambabwe, Zambia, Malawi na *DRC* wana *ESA* yao. Waliobaki kwenye *SADC* ni Tanzania, Msumbiji na Angola. Tukiendelea hivi maana yake ni kwamba tutakuwa tuna-*benefit through that door*. Mimi ninaamini ndiyo maana Marais wetu mwaka 2002 walivyokaa pale Kampala walisema lazima tufanye kazi twende tuka-*negotiate EPA* yetu kama *Block* ya *East Africa*. Maamuzi yale yalikuwa ni mazuri sana. Lakini baadaye

Kenya na Uganda wakaenda huko na sisi tukaenda huku. Hiyo ni historia kama alivyosema rafiki yetu Mheshimiwa Kabwe Zitto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Waziri hili analijua wamekwenda tunataka tu-*negotiate* kama *block* ya *East Africa*, Wakenya wamekataa. Mimi sina tatizo kabisa na Wakenya kukataa. Ninachoomba sasa Mheshimiwa Waziri atwambie tuchukue *initiative* twende tuka-*negotiate* kama nchi nne, tuachane na Kenya ili Wakenya hao tuwafundishe kwamba sisi tunayo nia ya kuendeleza *East Africa Community*. Kwa sababu tulisipofanya hivyo tuna-*destroy customs union* yetu. *Why are we doing that*? Twende tuachane na Wakenya, Mauritius leo wana-*negotiate* wao peke yao. Sisi tuko wanne, tukitoka hapo mimi namwamini Mheshimiwa Waziri tutamtuma *DRC,* tutawaingiza *DRC* tuwaache Kenya. Wale Kenya kama alivyosema Mheshimiwa Kabwe Zitto, watakuja kupiga magoti. Kwa sababu na wao wanalitaka hilo soko. Kama kuna watu wanataka hili soko *in-fact* ni wao zaidi. Sasa wasitupeleke kama wanavyotaka wao. *East Africa* inasifiwa kwa *common external tariffs* na *common trade policy* kama *the best* kwenye *WTO* walitusifu kwenye hilo. Tulinde maslahi yetu tusiwafuate Wakenya hao. Mimi ninachomwomba Mheshimiwa Waziri twende tuka-*negotiate EPA* yetu kama nchi nne na tuiongeze *DRC* tuachane na Wakenya hao ili tuwape *lesson* hao Wakenya tuwaonyesha *our commitment* katika *East Africa Community*. *(Makofi)*

Wasiturudishe kwenye historia ya mwaka 1977. Twende mbele, hawataki tuwaambie, " *fine go ahead,"* sisi tutaendelea na wengine na faida yake tukianzisha hizo nchi nne na *DRC* itakuwa ya tano. Ninawaambia nchi ndogo ndogo zenye *common small scale* zitakuja. *Egpty* wataomba, Sudan wataomba, hata Zambia na Malawi nazo zitakuja. Katika kufanya hivyo tutafaidika kupata fedha kwenye *EDF* 10. *EDF* 10 ya *EU* wangependa tu-*negotiate* sisi *straight* ili tupate fedha zitusaidie kwenye *infrastructure.* Huu ni wakati wa kutafuta maendeleo, ni wakati wa vita, inatakiwa tukimbie wakati wenzetu wanatembea. Siku moja Mahafiri alisema kama unataka kuendelea anayesimama njiani unamweka pembeni unaendelea. *(Makofi)*

La mwisho, Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka nichangie suala la umuhimu wa viwanda. Ni kwamba *economy* zetu ili ziendelee zinahitaji *Private Sector* zaidi na Waziri kwenye hotuba yake amesema kwamba lazima injini ya *growth* ya nchi zetu iwe *Private Sector*. Lakini tunayo kazi ya kuiendeleza *Private Sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliobakia hautoshi kuwa na mchangiaji mwingine. Lakini tutakubaliana kwamba uzito wa hoja na mijadala ambayo imefanyika hapa asubuhi ya leo ni ya kiwango cha juu sana na inahusiana na masuala ya uchumi. Waheshimiwa Wabunge, niwatangaze tu kwamba taarifa ya Kamati ya kukusanya maoni kuhusiana na suala la Afrika Mashariki ipo katika *pigeon-hole* zenu. Kwa hiyo, msisahau kuzipitia. Jioni ya leo wachangiaji wetu watakuwa watatu, ataanza Mheshimiwa Pindi Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Habib Mnyaa na wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Herbert Mntangi. Baada ya hapo atakuwa Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Waziri mwenyewe na tutaendelea na utaratibu kadri

itakavyokuwa. Vinginevyo kwa shughuli zilizopangwa asubuhi ya leo hapa mezani zimekamilika zote. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 6.55 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na majadiliano, sasa namwita Mheshimiwa Pindi H. Chana na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, ajiandae.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kuwa mtu wa mwanzo jioni ya leo. Nachukua nafasi hii kwanza kabisa, kumpongeza sana Waziri wa Wizara hii ya Afrika Mashariki na Naibu wake, kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya ndani ya Wizara hii ya Afrika Mashariki, ikiwa ni miongoni mwa zile Wizara chache ambazo Mheshimiwa Rais, alikuwa ameziziunda kuanzia mwaka jana na hii ni bajeti yake ya pili. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya watu wa Iringa, vilevile nampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa kutambua haja ya ushirikiano wa hizi nchi tatu; yaani Tanzania, Kenya na Uganda. Kimsingi wananchi wa hizi nchi tatu Tanzania, Kenya na Uganda, tukisimama tukivua magwanda yetu na mtu akituangalia si rahisi kutofautisha kusema huyu ni Mtanzania, Mganda na Mkenya, kwa sababu tunafanana sana na si hilo tu hata historia zetu kati ya hizi nchi tatu Tanzania, Kenya na Uganda kimsingi zinafanana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadri tunavyozidi kuendelea, maendeleo ya dunia na ya Taifa, suala la ushirikiano, kuungana kati ya nchi na nchi, watu na watu, kikundi na kikundi, mtu na mtu ni jambo ambalo ni la msingi sana. Dunia ya sasa hivi suala la kuwa na sauti moja katika masuala ya kiuchumi na maendeleo ni jambo la msingi sana. Mtu unapobaki peke yako au nchi inapobaki peke yake, inakuwa inapitwa na wakati. Duniani kuna aina nyingi sana za Muungano wa kiuchumi, kisiasa na kadhalika. *(Makofi)*

Nichukue moja ya nchi kadhaa ambazo ziliamua kuungana na leo sio mbaya tukiangalia zimefikia wapi katika maendeleo ya uchumi. Kuna nchi za Kiarabu *(United Arabic Emirates* - *UAE),* wao waliamua kuungana katika masuala ya uchumi. *European Union* leo hii wameungana na hadi wamefikia hatua ya kuwa na sarafu moja, ambayo inaitwa *Euro,* unaona wanaposimama kutetea maendeleo yao mbele ya uso wa Kimataifa wanakuwa na sauti moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi hata nchi ya Marekani wao waliamua wawe na aina yao ya Muungano, maana yake wao wanakuwa na *republic* mbalimbali na kila *republic* inaongozwa na *Senator* na baadaye wakaamua kuwa na Rais mmoja, ambaye anaitwa ni Rais wa *United States of America*. Kwa hiyo, wao wana muundo wao wa Muungano ndani ya nchi yao. Nataka kusema kwamba, kuwa na Jumuiya hii ya Afrika Mashariki ni jambo ambalo ni la msingi sana na kimsingi ni jukumu la wananchi sasa wote wa Tanzania Bara na Visiwani, kuunga mkono Jumuiya hii ya Afrika Mashariki,

kwa sababu ni Jumuiya ambayo kwa kweli inatusaidia sana katika masuala mbalimbali. Kimsingi hata sisi wenyewe Tanzania Bara na Visiwani, tumeamua kuungana na sisi tumekuwa na staili yetu ya Muungano. Tumesema katika Muungano wetu sisi tutakuwa na Serikali mbili; tutakuwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na tutakuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, masuala ya ushirikiano katika dunia hii ya utandawazi ni jambo la kulipa kipaumbele na ni kulifanyia kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna masuala ya utandawazi, tusipokuwa makini tukawa na umoja ndani ya nchi yetu na hasa na nchi za jirani katika masuala ya kiuchumi ni rahisi sana nchi hizi zinazoendelea *(Developing Countries),* ikiwa ni pamoja na nchi ya Tanzania kubaki nyuma. Unaweza ukakaa ukastukia sasa Mchina anakuja anakuwa Mmachinga nje ya mtaa wako unaoishi. Kwa sababu utandawazi umem-*force* amekuja mpaka katika mji wako. Kwa hiyo na sisi lazima tuungane hasa katika suala la uchumi tuwe kitu kimoja. Bidhaa zetu lazima tujitahidi ziwe na *quality* ili tuweze kuwa na sauti moja. Sasa baada ya kutambua hilo nini ambacho kinapaswa kufanyika? Ni kweli kabisa *Treaty* imeeleza wazi kwamba, kutakuwa na hatua kadhaa ndani ya Jumuiya hii ya Afrika ya Mashariki. *Treaty* hii ambayo imekuwa *signed* mwaka 1999 na ili-*get into force* mwaka 2000, imesema wazi kwamba, kutakuwa na hatua ya mwanzo ambayo itaitwa ushuru wa forodha ama *Customs Union.* Lakini lazima tujiulize; ni Watanzania wangapi wanafahamu nini maana ya ushuru wa forodha; ni Watanzania wangapi wanaweza wakafaidika na zile fursa ambazo zinapatikana katika huu ushuru wa forodha? Lakini kama Watanzania wengi hawafahamu juu ya suala hili la ushuru wa forodha, sasa ni jukumu la nani kuwafahamisha Watanzania habari ya ushuru huu wa forodha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Wizara hii itakuwa ina changamoto za kutoa elimu kwa kiasi kikubwa sana kwa Watanzania juu ya Jumuiya hii mpya ya Afrika Mashariki, baada ya Jumuiya ile ya mwanzo kuvunjika. Ni muhimu sana Watanzania wetu wakafahamu ni fursa zipi ambazo zinapatikana ili waweze kuzitumia fursa hizo. Tunaposema baadaye tunakuja kuwa na soko la pamoja, soko la pamoja hata mimi naliunga mkono katika misingi ya kwamba, unapozalisha bidhaa Tanzania unakuwa una soko la *population* la Tanzania ambayo ni watu milioni 36 lakini soko la pamoja la Tanzania, Kenya na Uganda maana yake utakuwa na soko la *population* la watu wasiopungua milioni 100. Mambo kama haya Watanzania ni lazima wakayafahamu kwamba, hizi ndizo fursa za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, lakini ni jukumu la nani ambaye anawaelekeza Watanzania umuhimu wa Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Tunajiandaaje, bado zipo changamoto upande wa elimu, ajira, bado zipo changamoto kuwaandaa wananchi wetu wakaweza kuli-*face* soko la ajira tena kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile suala la kuwa na sarafu moja ni jambo la msingi sana, tunaona nchi mbalimbali wameungana wamekuwa na sarafu moja na sarafu yao imekuwa ina nguvu sana. Nchi za Marekani wao hela yao ambayo inaitwa Dola ya Kimarekani sasa hivi kuna *Euro,* unaona kabisa hata unapokwenda kubadilisha pesa ile ni hela ambayo unaweza ukaitumia katika nchi nyingi. Katika nchi zetu, pamoja na mambo haya mazuri ni kwamba, hata lugha yetu ya Kiswahili itaweza kutambulika na kutumika katika eneo kubwa la dunia hii ya leo. Lugha ya Kiswahili ni muhimu sana, tukaangalia

jinsi ya kuitumia katika nyanja mbalimbali na itasaidia sana kuifanya nchi yetu ikafahamika katika dunia hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tumetambua kwamba, jambo hili ni muhimu na tayari tunayo *Treaty* ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni wajibu wetu sasa kujiuliza kwamba, tunaposema tunakuwa na ushirikiano wetu wa Tanzania, Kenya na Uganda ni namna gani huu ushirikiano uje na ni lini ushirikiano uanze ili yule Mtanzania hadi wa Ludewa kule Iringa, Kilolo na Makete, aweze kunufaika na kufaidika. Sasa ni lazima tujipange vizuri ili kuweza kuhakikisha kwamba, hata Mtanzania wa hali ya chini, ambaye analima nyanya, anapata na kulifikia hili soko la pamoja ambalo tumekubaliana kwamba, tutakuwa na soko la pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, lazima tuangalie suala zima la ulinzi. Katika mipaka yetu bado kuna changamoto, kazi ya Wizara kama walivyosema katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amesema kazi ya Wizara kubwa ni kuratibu. Naomba nitoe ushauri kama ifuatavyo: Pamoja na kazi ya kuratibu, ipo haja ya Wizara hii kuwa na jukumu la kushauri Wizara nyingine mbalimbali, ambazo zina mahusiano ya moja kwa moja na Jumuiya hii ya Afrika Mashariki. Lazima wawe ni washauri wa Wizara ya Elimu, masuala ya elimu tunajipanga vipi ili kuweza kukidhi mahitaji ya *labour market* ya leo hii. Lakini hata kushauri masuala ya ardhi, maana yake nchi yetu bado ina ardhi ya kutosha ukilinganisha na Kenya na Uganda na tunavyoingia kwenye Jumuiya hii ya Afrika Mashariki suala la ardhi tunajipanga vipi, lakini vilevile yako hata masuala mengine ya fedha.

Kwa hiyo, nilidhani pamoja na jukumu la kuratibu la Wizara, lazima Wizara iangalie jukumu la kushauri nchi na Wizara zake nyingine ambazo zina mahusiano ya moja kwa moja na Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wadau mbalimbali. Maana yake Jumuiya hii kama inavyosemwa, kazi yake ni kuratibu lakini sasa inakuwa na mahusiano gani na mikoa mbalimbali na sekta mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ipo haja yaku-*decentralise* shughuli za Wizara hii ya Afrika Mashariki zisiwe *centre* tu zinakuwa *monitored centred*. Wanaweza waka-*decentralised* majukumu yake na shughuli zake nyingine zikawa zinafanyika katika ngazi ya *Local Government Authorities* ili waweze kushauri Watanzania waweze kujiandaa kukumbana na hii hali ya ushirikiano kati ya nchi hizi tatu, ikiwa ni pamoja na masuala ya ardhi, kushauri, ku-*face* hiyo Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, masuala ya mifugo, kifedha na kadhalika. Lakini jukumu kubwa kabisa kama nilivyokwishasema ni kwamba, suala la kuendelea kuelimisha ni muhimu sana Wizara ikaangalia inakuwa ni jukumu gani na kuangalia ni jinsi gani wanaweza wakawashirikisha wadau wa aina mbalimbali. Kama watawashirikisha watu wa *Media* kuelezea juu ya Afrika Mashariki, kama watavishirikisha vyombo vingine vya aina mbalimbali ni jambo ambalo kimsingi ni la kuzingatiwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine niseme kwamba, ninaunga mkono hoja na ninakubaliana kabisa na Wizara hii na kazi nzuri ambazo zimekuwa zikiendelea kufanywa katika shughuli mbalimbali na Idara mbalimbali na nina imani kwamba,

wataendelea kufanya vizuri baada ya hoja zangu hizo ili kuweza kupata maisha bora kwa kila Mtanzania.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii angalau na mimi nitoe maoni yangu machache kuhusu hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Kwanza, napenda nimpongeze Msemaji wa Mkuu wa Kambi ya Upinzani katika Wizara hii, kwa hotuba yake iliyojaa ushauri, vielelezo na mapendekezo mbalimbali ya kututahadharisha sisi Watanzania, kuhusu mustakabali wetu na masuala haya ya Shirikisho hili. Pili, nampongeza Mheshimiwa Profesa Chacha Z. Wangwe na timu yake yote, kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuzunguka Tanzania nzima, Mikoa yote, Wilaya zote na kupata maoni ya wananchi na sasa nianze mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kwanza, nizungumzie kuhusu wastaafu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki iliyovunjika. Wenzetu Kenya na Uganda wastaafu wote wameshalipwa, lakini Tanzania bado, sababu ni nini hasa? Ni kitu ambacho kinashangaza kidogo; kwa nini mpaka leo miaka yote hiyo iliyopita iwe bado Watanzania hawajapata malipo yao wote? *Of course* wapo ambao wamepata mafao yao. Wengine wameshafariki, wameacha watoto wadogo, leo watoto hawa wa marehemu hao wanapofuatilia masuala hayo, wanaambiwa wapeleke nambari, sasa hizi nambari sijui zinapatikana wapi? Hivi tuseme Tanzania hawana kumbukumbu ni kwa nini mpaka leo kuna usumbufu huu? Huyo mtoto ambaye alikuwa tumboni, baba yake akafariki leo atajua nambari iko wapi, inategemea huyo mama yake alikuwa vipi! Kama *documents* zimepotea, lakini huku Serikalini hakukuwa na kumbukumbu, si wapo wakala wa vizazi na vifo *(RITA),* wanajulikana marehemu fulani warithi wake ni fulani, ikiwa hawajulikani jamani tuna tatizo Tanzania. Hili ni tatizo kubwa, haiwezekani watu hawa wasumbuke mpaka leo. Namwomba Mheshimiwa Waziri atupatie ufafanuzi wa masuala haya na namna gani wastaafu wote waliofariki na walio hai watapata mafao yao, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tumeona katika ripoti ya Mheshimiwa Profesa Chacha Z. Wangwe kwamba, mbali na kuchukua maoni kwa wananchi, walifika kule Zanzibar Baraza la Wawakilishi wakapata maoni ya wajumbe. Kwa ripoti inavyoonesha katika washiriki 70 kuna washiriki 11 waliochangia, walisema tusiharakishe suala hili la Jumuiya, mmoja akasema yeye ndio tuharakishe. Lakini watatu wakasema wao hawataki kabisa huu mpango wa kuwa na Jumuiya ya Afrika Mashariki, Shirikisho la Afrika Mashariki la Kisiasa hakuna kabisa. Sasa kwa ujumla, wenzetu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi asilimia 85 wanakubaliana na mpango huu wa Shirikisho la Kisiasa, lakini sio suala la haraka sana, lichukue muda na kufanya taratibu. Kwa upande wa Wabunge kati ya washiriki 227 inaonekana waliopata kushiriki kwa maandishi na kwa kuzungumza ni Wabunge 120 na kati ya hao Wabunge 114 walisema tusiharakishe. Ni Wabunge sita tu waliosema wanataka sasa hivi, yaani wanataka liharakishwe. Kwa ujumla asilimia 95 ya Waheshimiwa Wabunge wanakubali au tunakubaliana na wazo la Shirikisho la Kisiasa lakini sio kwa haraka, lichukue muda zipite taratibu tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni hayo ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na ya Bunge ni ya kutiliwa maanani, kwa sababu kwa ujumla yamechukua asilimia kubwa na hawa wote wanawakilisha wananchi katika Majimbo yao. Hata kama utaacha haya maoni ya Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge, wananchi wenyewe kati ya Watanzania 65,820 kuna Watanzania 18,321, sawa na asilimia 75.9 wanasema tusiharakishe, lakini wapo waliosema tuharakishe, ambao ni asilimia 20 na wapo kama wananchi 616 waliosema lisiwepo kabisa, hasa mpango huo usiwepo. Sasa basi maoni haya ningeiomba Serikali iyazingatie na wala wasikurupuke kulileta suala hili haraka haraka, isipokuwa maoni ya wananchi, maoni ya Waheshimiwa Wabunge na maoni ya Waheshimiwa Wawakilishi, yazingatiwe na yaheshimiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna dhana hii hapo hapo katika Uwakilishi wa Zanzibar, Tanzania tunataka kuingia katika hii Jumuiya kama Tanzania. Lakini hapo zamani Zanzibar ilikuwemo na ilikuwa na *status* ya kinchi hivyo; kwa nini leo Tanzania hatutaki kuingia kama nchi mbili katika hii Jumuiya hapo muda utakapofika; kwa nini tunakataa wazo hili? Hatuoni tutakuwa na *power* ya *voting rights* tukiingia kama nchi mbili, kuliko nchi moja? Leo Uganda ni moja katika nchi iliyotumia nguvu ili Burundi na Rwanda ziwemo katika Jumuiya hadi hivi sasa ni tayari. Tuna uhakika gani kwamba, wakati huo ukifika, Uganda, Burundi na Rwanda hawata-*vote* kama *block;* tuna uhakika gani? Kwa nini sisi tukatae na wazo la Zanzibar kuingia kama nchi mbili na wakati huo huo tukumbuke kwamba, *East African Currency Board,* Zanzibar iliwakilishwa kama ni nchi na wakati ule Rais Mstaafu, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, ndiyo aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi, leo pana utata gani?

Ningeomba suala hilo Serikali ilizingatie na tujiulize hasa kwa nini tunakataa. Haiyumkini hawa wanaokataa wana *agenda* yao ya siri, ndio hao wanaotaka kudhoofisha Muungano. Wanaokataa kwamba tusiingie kama nchi mbili, tusisahau Yugoslavia katika ule umoja wa Warsar Pact, waliingia. Yugoslavia wakati huo zilikuwa nchi tatu lakini ulipovunjika umoja ule haikurudi Yugoslavia ilirudi Serbia, Montenegro na Croatia. Sasa tuliangalie suala hili, tunaingia kama Tanzania lakini je, tuna uhakika gani kama hakutakuja kutokea madhara ya kuvunjika tena, ikija ikivunjika tutakuja rudi kama Tanzania? Kwa hivyo, yumkini kwamba hao wanataka tusiingie kama nchi mbili, ndiyo wana malengo mabaya. Uzoefu wa dunia ndio huo nilioutoa, tunaweza tukaingia kama nchi moja lakini mambo yakiharibika tukarudi kila mtu na upande wake. Ndiyo naomba lisitokee hilo, tuingie kwa kuiwakilisha Serikali mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hofu hii ya Jumuiya kwa nini watu wengi wana hofu? Kuna wachangiaji wenzangu waliozungumza habari ya elimu, ajira na kadhalika, lakini ni lazima kweli Tanzania tuwe na hofu. Mimi nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, siku Mheshimiwa Profesa Chacha Z. Wangwe, alipokuja kuchukua maoni ya Wabunge, Wabunge wengi walikiri kwamba, hakuna haja ya kuharakisha kwanza, tutatue matatizo yetu ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano huu tulionao wa Tanganyika na Zanzibar, bado una matatizo mengi tu, tuyatatue haya kwanza ndiyo twende kwenye Jumuiya. Ushahidi upo, tuna matatizo kibao Mheshimiwa Waziri Mkuu unajua na mpaka leo

hayajatatuka, kila siku kesho; kwa nini kwanza tusitatue haya tuliyonayo sisi? Sisi Tanzania tuna matatizo yetu ya ndani ni nyumba nzuri, nje ina rangi inapendeza, lakini ndani mna matatizo. Kenya wana matatizo yao, Uganda wana matatizo yao halafu tuunganishe. Mimi nakubaliana na Msemaji wa Kambi ya Upinzani, tunaunganisha Shirikisho hili tunaunganisha matatizo, haiwezekani, tutatue haya yetu kwanza tuliyonayo halafu twende huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli zile *principals* zilizowekwa za kiuchumi za kwanza kuwe na *Customs Union* na hii ilitakikana mwaka 2005 iwe imekamilika. Mheshimiwa Waziri, atueleze tumefikia wapi mpaka leo? Hilo soko la pamoja 2007 ndiyo hii, tumefikia *stage* gani na kwa nini tunasuasua? Kinachotakiwa mwaka 2007 likamilike na zinatakiwa mwaka 2008 kuwe na pasi za kusafiria za pamoja. Wenzetu Kenya, tayari wana vitambulisho vya uraia wao, Uganda, sisi Tanzania mpaka leo bado tunasuasua. Halafu mwaka 2008 hiyo hiyo iwe tayari na *common passport.* Mwaka 2008 ni kesho kutwa au kesho, leo hatujafanya lolote hata katika hivi vitambulisho vya uraia wa Tanzania. Tueleze tumefikia wapi na tutafanya nini. Hali kadhalika na hiyo sarafu moja, hiyo ndiyo ina matatizo kabisa kwa sababu sarafu moja uwiano wa hii sarafu ya Tanzania, Kenya na Uganda, ulivyokuwa mkubwa kuna nchi za Kenya, Sweden, Norway, Denmark hazipitani sana na mpaka leo hawajakuwa na sarafu moja, ingawa unaweza kwenda nchi hii ukatumia sarafu ya nchi hii. Leo uwiano huu ulete tofauti halafu mwaka 2009 tuwe na sarafu moja, inaelekea kwamba kwanza, tujitayarishe sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie nisipigiwe kengele. Haya matatizo ya Shirikisho la Kisiasa, inafaa wananchi waeleweshwe vizuri katika hali ya utaratibu, kidogo kidogo mpaka ifike miaka hiyo kwamba tuko tayari. Kwa sababu huu Muungano wa Tanzania, nakuhakikishia Watanzania wengine hawajaufahamu. Mfano hai, nina rafiki yangu mmoja Mheshimwa Mbunge wa Kanda ya Ziwa, siku moja aliniambia kweli bwana hizi ni kero za Muungano, kule Wilaya moja sisi ina Wabunge watatu tu, wakati Zanzibar Wilaya yetu ina watu laki tisa tuna Wabunge watatu, Zanzibar ina watu milioni moja ina Wabunge zaidi ya 50, nikasema Mungu wangu, looh! Ina maana hata Waheshimiwa Wabunge ule Muungano wa Tanganyika na Zanzibar hawaufahamu, leo mnataka kuingia Afrika Mashariki.

Juzi hapo katika Maonesho ya Sabasaba, Banda la Zanzibar walipata tabu kweli kueleza Muungano huu wa Tanganyika na Zanzibar, watu hawauelewi. Sasa ikiwa huu wa kwetu sisi wa miaka 40 na zaidi hatuuelewi au kuna watu miongoni mwao Waheshimiwa Wabunge, ije iwe Shirikisho la Kisiasa tunalotaka kuliharakisha! Tunaiomba Serikali hili suala ichukue maoni haya na iyazingatie wala isiharakishe suala hili. Asante sana.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza, nikushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ili na mimi niweze kuzungumza jioni ya leo katika Wizara hii maalum, inayoshughulikia na Mambo ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana Waziri, pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii, kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Tumedhihirisha hayo, kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakijitahidi kujibu maswali yetu mazuri katika kipindi hiki cha Bunge mwaka huu.

Naomba pia niwapongeze sana Wabunge wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuwa, radhi leo kuwepo hapa katika Bunge hili ili kumuunga mkono Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ambayo inawagusa sana, ndugu zangu karibuni sana hapa ni kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala hili la kutaka kupata maoni ya wananchi. Tumeshasikia Tanzania tumekwishatoa maoni yetu na inaonekana kwa asilimia kubwa, Watanzania wanasema tusubiri. Lakini tumesikia vilevile wenzetu wa Uganda, wamekwishatoa maoni yao na kwa kiwango kikubwa, Uganda wako tayari kuharakishwa kwa Shirikisho. Sina uhakika wenzetu wa Kenya wamesimamia wapi, lakini inawezekana na wao pia wakawa wako nyuma ya Uganda kutaka Shirikisho liharakishwe. Tumewaruhusu Rwanda na Burundi, nina imani kabisa tutawapa nafasi ili nao watoe maoni yao. Sasa sijajua na pengine ni vizuri Mheshimiwa Waziri akanielekeza na akalishauri Taifa kwamba, nini itakuwa matokeo au tutafanya uamuzi kwa kutumia vigezo gani, iwapo kwa mfano Kenya, Uganda wamesema ndiyo, Tanzania tumesema hapana na vilevile Rwanda na Burundi wamesema ndiyo, kwa hiyo, nchi nne zimesema ndiyo Tanzania imesema hapana? Kwa msimamo huo maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba, sasa Tanzania imeshindwa na hivyo Shirikisho litakuja haraka, kwa sababu nchi nne zimesema ndiyo sisi tumesema hapana. Vinginevyo, hebu tuambiwe basi nini itakuwa haki ya Watanzania waliosema tusubiri Shirikisho hata kama wenzetu nchi nne zitakuwa zimesema tuendelee na Shirikisho? Tuelimisheni Watanzania tujue nini matokeo, iwapo msimamo utakuwa katika hali hiyo niliyoieleza? Hilo ni muhimu sana.

Lakini la pili ni Elimu. Tunazo ngazi zile nne ambazo tayari tulikwisha kukubaliana kwamba, ndizo tutakazofuata ili tuweze kufikia Shirikisho. Tumewadhihirishia wananchi kwamba, wananchi wengi hawafahamu utaratibu huo. Sasa nimetazama katika maombi ya fedha ya Wizara hii ili niangalie kama kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya elimu kwa Watanzania, Wakenya, Waganda, Warwanda na Warundi, lakini kwa upande huu wa Tanzania, sioni kipengele kinachoonesha kwamba kuna mpango maalum wa kuwaelimisha wananchi kuhusu zile hatua tatu zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaona fedha zimeombwa kwa mchango wa uwanachama, sina hakika kama fungu hili nalo ndilo fungu linalozungumzia elimu. Shilingi bilioni 5.4, shilingi milioni 319 kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Sasa jukumu la kutoa elimu liko mikononi mwa nani? Ni matumaini yangu litapaswa kuwa mikononi mwa Wizara hii inayoshughulika na Mambo ya Afrika Mashariki. Basi ni vyema Mheshimiwa Waziri pia akatueleweshe hapa kwamba, jukumu hili amekabidhiwa nani na litaendeshwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa turudi katika mfumo mzima wa Shirikisho. Mimi nawapongeza wananchi wangu wa Wilaya ya Muheza, wao walishiriki katika kutoa maoni na hayakutofautiana, wako ndani ya ile asilimia 75 ambao walisema Shirikisho

tusiriharakishe. Ninawapongeza sana huo ni msimamo mzuri. Lakini hebu tutafakari kwa umakini; nini maana ya Shirikisho? Nitalizungumza kwa kifupi sana kwa maoni yangu mimi Shirikisho maana yake ni kushibana. Sasa tutashibana kwa namna gani? Maana yake kama mko watatu, mnadhani mna mambo mnayoyazungumza yanayoelekeza kuwaisaidieni ninyi kwa pamoja, kwa hisia moja, basi mtakuwa na uwezo wa kusimamia msimamo mmoja kama mtakuwa mmeridhiana au mmeshibana. Kama hamjashibana, hamuwezi kwenda katika Shirikisho. Sasa katika Shirikisho hili ni mambo gani yanayotufanya sisi tujisikie kwamba tumeshibana, tumejiwekea vigezo vinne.

Kigezo cha kwanza ni hili la Umoja wa Forodha. Je, Tanzania, Kenya, Uganda na sasa Rwanda na Burundi katika mfumo huu wa umoja wa forodha tumeshibana? Jibu sina uhakika nalo, lakini kwa sababu nafahamu yapo matatizo katika utekelezaji wa huo umoja wa forodha wenyewe, basi nasema hatujashibana hata katika hatua hii ya kwanza. Ni vizuri basi tukatazama matatizo yaliyoko hapa, tukayachambua vizuri tukayaweka sawa ili baadae tuulizane, Wakenya, Waganda, Watanzania, Warwanda na Warundi, kwa mpango huu wa umoja wa forodha tumeshibana. Tukiafikiana ndiyo tunakwenda hatua ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua hii ya pili ni hatua ya soko la pamoja. Sasa katika hatua hii ya soko la pamoja inaonekana kuna baadhi ya nchi ambazo tayari wameshavuka hatua ya kwanza ile ya umoja wa forodha, wapo katika soko la pamoja. Sasa sijui kama hilo ni soko la pamoja kama hatujaridhiana na hatujashibana. Lakini wenzetu wengine, wanatekeleza mfumo wa soko la pamoja. Tumesikia hapa Waheshimiwa Wabunge, wametoa mifano mbalimbali. Lakini na mimi nataka niungane nao kwa kutazama nini kinachotokea pale Muheza Wilayani kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa nchi za jirani wameingia pale, wanafanya biashara nzuri ambayo sisi watu wa Muheza tunaipenda kwa sababu mwisho wa yote, mkulima wangu anapata fedha ya machungwa aliyozalisha. Lakini ni kwa utaratibu gani biashara hiyo inafanyika sasa? Wenzetu Wakenya wanakuja wananunua machungwa kwa fedha za Tanzania. Hivi huo ndiyo mfumo wa hilo soko la pamoja, tumeshafikia huko, wanatoa wapi fedha za Tanzania? Ni wazi, wanakwenda kwenye *Bureau de Change* Nairobi, Mombasa na hela zao za Kenya, wananunua fedha za Tanzania kule si zipo halafu ndiyo wanakuja nazo kununulia bidhaa Tanzania na wala si Muheza. Wabunge wamesema Karatu, viazi na vitunguu, Morogoro wametoa mfano na sehemu nyingi tu na ndivyo wanavyofanya. Kwa hiyo, wanabadilisha fedha zao. Sisi tunaingia katika Mfumo wa Biashara sasa hivi kabla ya hilo soko la pamoja na hatupati hata senti tano ya fedha za kigeni kutoka nchi za kigeni za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Hiyo ni *unfair trade*. Hivi Watanzania hatuwaoni Wakenya hawa? Tunawaona, hata mimi nawaona, lakini mimi ndiyo kazi yangu ya kwenda kukamatana nao? Ni kueleza vyombo vinavyohusika ili tutazame na tuendeshe utaratibu utakaowezesha mfumo wa biashara, utakaonufaisha nchi zote mbili. Ni kweli sisi tunataka wakulima wetu walipwe fedha za machungwa wamefanya kazi, lakini je, huo ndiyo mfumo mzuri wa biashara ya kisasa ya kimataifa? Hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nasema wenzetu wanataka Shirikisho haraka kwa sababu kwanza, wamekwishafanya vizuri katika huu umoja wa forodha na sasa wamekwishaingia katika hilo soko la pamoja, bila sisi wengine kutoa idhini ya kuingia soko la pamoja. Sasa ni vyema Watanzania tukashauriana, tukaunda utaratibu mzuri kwa sababu bado kweli tunahitaji Wakenya wanunue machungwa, tunahitaji wanunue vitunguu na bidhaa nyingine kwa sababu tunazo za ziada zaidi ya uwezo wetu katika soko la nyumbani, lakini tunataka biashara hii ifanywe kwa uhalali. Nasema tu kwamba, wanafanya biashara bila hata *business license.* Wanafanya biashara hiyo hata kodi hawalipi. Maana yake tuna wafanyabiashara ndani ya nchi hata kodi hawalipi! Kuna watu wanawaita madalali wao au watu wakati wao ndiyo wanaojibana pale. Lakini ukweli wanafanya biashara na kweli hata katika maeneo mengine inawezekana ikathibitishwa kwamba, kweli wamenunua ardhi na sheria inasema hapa kuuza ardhi kwa wageni. Watanzania tuko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye jambo lingine ambalo pengine litasaidia. Tuna matatizo kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, hasa katika mwelekeo wa *EPA*. Tumepisha na wenzetu Wakenya na Waganda; Tanzania tumebaki peke yetu. Lakini hebu tusaidieni, tuna mpango mwingine na mawazo mengine ya ushirikiano wa nchi za Maziwa Makuu; tunasema nini kuhusu mpango huu wa nchi za Maziwa Makuu? Kwa sababu nina imani kabisa kwamba kwanza, katika uanachama, pendekezo hili la nchi za Maziwa Makuu lina wanachama wengi zaidi hata kuliko hiyo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Sisi kama Jumuiya ya Afrika Mashariki, ambayo tumeshapiga hatua kubwa zaidi kuliko hata Jumuiya nyingine katika Bara la Afrika, kwa kuwa na *Custom Union*; je, tunachukua hatua gani za kuwavuta wanachama wenzetu katika mfumo ule wa Shirikisho la nchi za Maziwa Makuu ili waweze kujiunga nasi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki?

Wenzetu wamezungumza vizuri sana hapa kwamba, tusiiache *DRC*, lakini ukienda mwisho wa ukingo wa Afrika juu ya *DRC,* kuna nchi nyingine ziko kule Gabon wako kule, kuna Sudan na nchi nyingine nyingi, lakini ukishuka chini kuna Zambia, Malawi, hebu tujaribu kuangalia kama bado hatujachelewa. Tujaribu kuwavuta wenzetu waingie katika Jumuiya hii ya Afrika Mashariki, tuweze kuwa na nguvu zaidi tuweze kwenda *EPA* kwa mfumo wa nchi nyingi zaidi kuliko nchi tatu au nne kama zilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuingia katika mpango wa sarafu moja, sisi watu wa Afrika Mashariki kweli kihistoria kabla ya ukoloni ndani ya ukoloni tulikuwa na sarafu moja, kwetu hilo si jambo geni, lakini hatuwezi sasa tukaenda huko kabla ya hatujashibana, tushibane kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho niseme tu kwamba, huko tunakokwenda Watanzania hatujasema hatutaki Shirikisho, tunachosema tusiharakishe kuingia katika Shirikisho. Shirikisho ni muhimu kwa sababu linatoa fursa nyingi sana za kiuchumi, ambazo nchi kama Tanzania, pamoja na huo udhaifu tunaojiona tunao, bado fursa hizo zipo, bado nafasi ipo, tunapaswa kusimama imara tuzichangamkie ili taifa hili liweze kunufaika. Tusiogope, hatuna njia yoyote lazima tujiunge na wenzetu tufanye kazi

kwa pamoja, tufungue macho ili tuzione fursa hizo na kama kuna fursa ambazo ni nzuri zaidi kwa Watanzania kuliko Wakenya na Waganda. Je, hizo ambazo wenzetu wanaziita zinatupa sisi *comparative advantage,* hizo nazo tunasemaje sisi Watanzania; hivi tunahitaji watu kutoka nchi za nje waje watuambie Tanzania mna *comparative advantage* kwenye jambo hili hivyo lichangamkieni, hatuna wataalam, hatuna wachumi wa kutosha? *Deduction* ni muhimu sana, tujitume Watanzania tutafanikiwa. Nawatakia kila la kheri, ninaamini siku moja Shirikisho litafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushuruku sana Mheshimiwa Herbert Mntangi, kwa mchango wako.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE.SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi kuchangia kidogo. Pamoja na kazi inayofanya ya kukusanya maoni, lakini pamoja na hayo yote sisi tulio mipakani pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kagera, hatuoni liwe ni suala la kuharakisha. Tuna mifano ya Ngara na Uganda, tumekaribisha wakimbizi ambao umekuwa ni mzigo mkubwa na matatizo makubwa wamekuwa wang'ang'anizi walikuja wakiwa binadamu kuwasaidia, wametulipa unyama mkubwa kama mnavyojua mipaka yetu ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,majambazi wengi ni majirani zetu ambao ni wakimbizi na sasa tumeanza kuvamiwa na Wasomali, wanaingiaje kwenye nchi yetu? Wamefanya hivyo, je, tukifungua mlango au milango kuingiza panya, mijusi, sisimizi bila hata kujua? Uganda mpaka leo kuna watu wanaosema Mto Kagera unarudi Kampala. Kenya wanajidai na Mlima ya Kilimanjaro wanajidai ni wao, nao je, hivyo kweli leo hii sisi wenyewe tuwakaribishe. Uganda wanaua wananchi wetu kwenye Ziwa Victoria wakitoka Mtashi Karagwe wakiwa kwenye mitumbwi lakini wenyewe kuja huku. Hakuna anayewazuia.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Warundi kukatana mapanga wao kwa wao kwa sababu wenyewe bado wana ukabila, Watusi na Wahutu, je, kweli mambo hayo na vipengele vyote nilivyoainisha hapa na nimeshiriki kwenye mkutano wa Bunge Afrika Mashariki, Hoteli ya Kilimanjaro nilikuwa nasikia matamshi yao, sasa leo hii ndio hayo yananisumbua. Naomba majibu sahihi yanisaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha maoni yangu.

**MHE. MOHAMED G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara yake pamoja na pongezi hizi naunga mkono hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ninayo mawazo yafuatayo ambayo namwomba Mheshimiwa Waziri anipatie majibu yenye ufafanuzi. Katika mchakato mzima wa *East African Community* tulikubaliana juu ya *harmonization of external tariffs* mpaka sasa

hivi hatujafanya hivyo. Kwa mfano, mafuta ya kula *(crude palm oil – cpo),* Tanzania tunalipa ushuru wa 10%, wenzetu wa Uganda na Kenya hawatozi hiyo, inaathiri soko letu la ndani kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, hivyo Mikoa ya Mara/Mwanza, Kagera, Arusha, Kilimanjaro na Tanga inanunua bidhaa zaidi kutoka Kenya na Uganda badala ya Tanzania. *We become uncompetetive.*

Mheshimiwa Mwenyekiti,*crude palm sterin* (ushuru) Tanzania ni 10%, wakati Kenya na Uganda ni 0%. Mchele, ushuru wetu ni 75% wakati wenzetu ushuru wao ni 25% na 35% *respectively.* Ngano, ushuru wa Kenya ni 35% na wa Tanzania ni 10%. Kwa hii tuko *competetive advantage* lakini wenzetu Kenya wanatutoza kodi za ajabu hivyo kufanya bidhaa zetu *uncompetative.*

Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba Mheshimiwa Waziri, wakati anahitimisha hoja yake anipe ufafanuzi wa kina ili Watanzania kwa ujumla wafahamu utata huu ambao unaathiri mchakato mzima wa masuala ya kodi na ushuru kwa bidhaa zetu. Pia suala zima la Umoja wa Forodha litazamwe upya kwa manufaa ya wananchi na Watanzania kwa ujumla. Naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti,nianze kwa kumpongeza Waziri wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kuwasilisha hotuba yake kwa ufasaha mkubwa. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nimefarijika na tamko la Waziri (ukurasa 18) kuwa maoni ya wananchi wa Tanzania kuhusu uharakishwaji wa Jumuiya yatazingatiwa. Kauli hii ni kama ile aliyoitoa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, wakati akipokea taarifa ya Kamati ya Wangwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kusisitiza tu kuwa mwaka 2013 uliowekwa kwa kuanzishwa kwa Shirikisho hautoshi au kwa maneno mengine ni *unrealistic.* Kama lengo ni kutaka kutumia shirikisho la kisiasa kusukuma mabadiliko ya kiuchumi, basi lengo hilo halitafanikiwa kwa kuwa msingi wa uchumi ndiyo unaobeba mabadiliko endelevu ya kisiasa. *It is the economic base which always determines the superstructure.* Hivyo basi utaratibu tuliojiwekea chini ya mkataba wa Jumuiya (Ibara ya 5(2) wa kujenga Jumuiya kwa awamu na ngazi hadi kufikia shirikisho *(a building block approach),* ni mzuri na wenye uhakika kutufikisha tunakotaka. Uharakishaji na kuweka *definite time line* ya kufikia shirikisho hautatusaidia kwa vile mchakato mzima ni tegemezi! Tunategemea *development partners* watubebe kwa zaidi ya asilimia 50, halafu tunaweka ratiba! *The whole thing is unsustainable.*

Naomba nimalizie kwa kusisitiza kuwa uharakishwaji wa shirikisho una vikwazo kadhaa ambavyo lazima vizingatiwe kabla hatujajitosa huko:-

(i) Uendeshaji wa Jumuiya bado unategemea, kwa karibu asilimia 50, michango ya wahisani. Hatuwezi kujenga Jumuiya endelevu na hatimaye shirikisho kwa kutegemea nguvu ya fedha toka nje;

(ii) Tuna tatizo la *Buganda Kingdom* kudai daima *autonomy* au utawala huru. Tutalitatuaje ili lisiwe tatizo kwenye shirikisho?;

(iii) Tuna tatizo la Zanzibar kutaka kero za Muungano zitatuliwe zote kwanza kabla ya shirikisho;

(iv) Tuna mifano maalumu ya ardhi Uganda (Mailo) na Kenya *(freehold),* ambayo inawapa wachache milki ya ardhi yote na kusababisha *pressure* kubwa ya ardhi kwenye nchi hizo na kuifanya Tanzania kuwa kimbilio la wengi. Kuna umuhimu kuwapa Watanzania uhakika wa maslahi yao kwenye ardhi yao waliyoitunza kwa miaka mingi;

(v) Utaifa tayari umejijenga na kukomaa, hivyo *fast tracking* ifanywe kwa uangalifu mkubwa ili kutotibua Utaifa wa wadau;

(vi) Hatuna huduma za pamoja, sarafu moja na soko la pamoja, mazingira yaliyokuwepo miaka ya 1960, mazingira ambayo yangerahisisha sana ushirikiano wa kina zaidi wa Afrika ya Mashariki;

(vii) Uganda bado inakabiliwa na hali ya wasiwasi sehemu ya Kaskazini, hali ambayo lazima iondoke kabla ya shirikisho;

(viii) Ukabila bado umejikita katika nchi wanachama na katika nchi tulizozikaribisha, Rwanda na Burundi, hali ambayo itatugawa kimtandao kuliko kutuunganisha; na

(ix) Bado hatujakomaa kisiasa na kiutawala kiasi kwamba vitendo vya kubadili Katiba ili kiongozi mmoja aendelee kutawala vinaendelea Afrika ya Mashariki! Hicho ni kipimo tosha kuwa bado hatuna misingi ya kutosha kuingia kwenye Jumuiya. Narudia tena kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuajlia uzima na afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nakupongeza wewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge kwa kutuongoza vizuri hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti,muda wa kuingia katika Jumuiya ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki bado haujafika ni vyema tukamaliza matatizo yaliyomo ndani ya Muungano wetu kabla ya kuingia katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Tanzania, Kenya na Uganda hazilingani kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiusalama. Ni vyema tukawa makini katika vipengele nilivyovitaja na vinginevyo ili tutakapoingia katika Jumuiya tuwe tumejiimarisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Watanzania wapatiwe elimu juu ya umuhimu wa kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki na athari zinazoweza kupatikana iwapo hatukujiunga na Jumuiya hiyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ni vyema tukatafakari matatizo yaliyosababisha kuvunjika kwa Jumuiya iliyokuwepo ili tutakapojiunga isije ikavunjika katika muda mfupi tu baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti,tutakapounda upya Jumuiya ya Afrika Mashariki ni vyema lugha ya Kiswahili kutumika kama lugha rasmi. Hii itawezesha kukuza lugha ya Kiswahili pamoja na kurahisisha mawasiliano baina ya wananchi wa nchi zetu.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake pamoja na wataalamu wa Wizara hii. Napenda niseme kuwa naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,uimarishaji wa mahusiano ya wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Chang’ombe iliyo mbele yetu sote katika hizi nchi tano sasa zinazoiunda Jumuiya hii. Naipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuendelea kuthamini maoni na michango ya wananchi wake juu ya jinsi gani wananchi wanapenda kuhusiana. Inafurahisha kuona kuwa taarifa sahihi juu ya Jumuiya hii zinaendelea kupelekwa kwa wananchi. Kazi hii ni muhimu sana ikeendelezwa kwa juhudi zote bila kutafuta njia yoyote ya mkato.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mahusiano baina ya wananchi wa nchi wanachama wa Jumuiya yataendelea kukua kama Serikali zetu zitaendelea kurahisisha mawasiliano baina ya wananchi hawa na kuboresha viwango vyao vya kufaidika na biashara halali baina yao. Tukumbuke kuwa asilimia kubwa kabisa ya wananchi wa nchi wanachama ni wakulima ama ni wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na uvuvi. Hapo ndiyo nadhani tunapaswa kuendeleza zaidi (ku-*promote* zaidi) ukaribu baina ya wananchi hawa. Urasimasishaji wa biashara katika viwango hivyo utarahisisha sana kusogeana kwa wananchi wetu na kuaminiana na pia kutegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti,natambua umuhimu wa kusogeza zaidi wafanyabiashara wakubwa baina ya nchi hizi kurahisisha utembeaji wa mitaji ya wawekezaji wananchi wa Jumuiya (pia wa nje), lakini kama tutataka kudumisha na kuimarisha ushirikiano baina ya wananchi wetu na kuaminiana na pia kutegemeana.

Mheshimiwa Mwenyekiti,natambua umuhimu wa kusogeza zaidi wafanyabiashara wakubwa baina ya nchi hizi, kurahisisha utembeaji wa mitaji ya wawekezaji wananchi wa jumuiya (pia wa nje), lakini kama tutataka kudumisha na kuimarisha mshikamano baina ya wananchi hawa basi lazima lakini tujielekeze katika kuwasogeza hawa karibu kupitia shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nashukuru kwa fursa hii na nasema tena naunga mkono hoja hii.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watumishi wa Wizara hii kwa kazi nzuri zenye mpangilio mzuri katika Wizara hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri ama awaye yoyote katika Wizara hii aliyeshiriki kwa njia moja au nyingine katika na waandaji wa hotuba ya Bajeti ya Wizara hii. Ni hotuba nzuri na naunga mkono hoja. Hata hivyo ninaomba nichangie katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Kuhusu Serikali kuanzisha Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Wizara hii hasa katika kipindi hiki. Ninaamini itafanya kazi nzuri ya kuwa naunganisha watanzania na wenzao wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa maoni ya wananchi kuhusu kuharakisha shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki, kwanza kabisa naomba kuipongeza Tume iliyopewa jukumu la kuyakusanya maoni hayo kutoka kwa wananchi wengi kazi iliyowezekana na kwa makini na muda mfupi matokeo yalikuwa mazuri na ya haki kwa hali yetu ya hapa nchini hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,pamoja na matokeo kuonesha kuwa asilimia 75.9 ya wananchi walipendekeza uundwaji usiharakishwe na asilimia 20.8 walitaka, kutokana na hali ya wengi wape ndiyo msimamo wa nchi yetu tuliochukua, napenda nitumie fursa hii kuiomba Serikali sasa itumie fursa hii ya kuahirishwa kwa uanzishwaji, kuwaelimisha wananchi kwa kuwaambia ukweli kuwa tutake, tusitake shirikisho kuundwa ni suala la msingi na ni muhimu kwa ustawi na maendeleo ya eneo letu ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuanzishwa si uamuzi wa mtu mmoja, wala kiongozi mmoja, kuanzishwa kwa shirikisho kwa maoni yangu ni mahitaji ya msingi ya mazingira ya kiuchumi kisiasa na kijamii tunamoishi. Hata tukiendelea kusisitiza hatimaye kwa kutaka au kutokutaka tutajikuta tumeshajiunga/tumeanzisha. Ni msukumo wa kiulimwengu na kidunia! Hivyo ni fursa sasa kila nchi itumie fursa hii inayoelekea kujitokeza ya kuchelewesha ijiandae vyema ili baadaye ikawa mzigo na kikwazo kwa maendeleoya eneo letu. Yapo mambo mengi yanayotokea ambayo hatuna sana uwezo wa kukubali/kukataa, mifano ya wazi ni soko huria na utandawazi. Nani aliyeshirikishwa katika kuanzishwa kwa utandawazi na soko huria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu Serikali itusaidie kubaini ni katika maeneo gani tuko nyuma na tukiingia hivyo katika shirikisho tutaendelea kuwa nyuma au tutawakwamisha wenzetu katika eneo letu katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,maeneo ambayo nashauri ni kuendelea kuboresha na kuimarisha elimu yetu ili matunda ya ajira ndani ya nchi, Afrika Mashariki, Afrika na ulimwenguni kote. Eneo lingine ni kuboresha mtandao wa miundombinu ya usafirishaji na usafiri kwa eneo hili naipongeza Serikali kwa hatua inazozichukua hasa katika kuimarisha barabara za ndani na pembezoni mwa nchi. Juhudi hizi ziendelezwe tena kwa kasi kubwa zaidi.

Kuhusu kuimarisha Wizara hii, Wizara hii pamoja na umuhimu wake wa kutuweka karibu na jirani zetu tunaotakiwa kuwafahamu fika kwa kuratibu ikiwezekana kwa kila wakifanyacho kila siku mema na mazuri kwetu. Kwa mawazo yangu ninategemea kuwa Wizara hii inastahili kuwa na maofisa (na mafungu kwa ajili ya kuratibu yanayotokea katika Wizara ya nchi jirani). Tuwe na *desk* la biashara, utalii, viwanda na elimu ili tuweze kuwa tukienda sambamba na mabadiliko yanayotokea katika nchi za majirani zetu. Ninachokiona hapa kwa Bajeti iliyoletwa na Mheshimiwa Waziri kuwa bado hatujawa makini hata kidogo. Wizara hii kwa Bajeti hii ni idara tu katika Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nashauri au tuwe na Wizara hii au tutoke kama hatujawa tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Bajeti hii ni ndogo mno. Bajeti hii inadhalilisha Wizara hii na majukumu yake. Tumekuwa kama tumeiunda kwa nia ya kuridhisha mtu mmoja bila kufahamu umuhimu wa mahitaji yake. Naomba sana Bajeti yake ipangwe upya na idara zake za uratibu ziimarishwe kwa fedha na utaalamu. Heshima yetu inaanzia ndani ya maandalizi na ushiriki wetu katika Jumuiya na Shirikisho la Afrika Mashariki. Ni vyema tukawa na uhakika kuwa ndani ya Jumuiya na Shirikisho hatuna mjomba, hatuna wa kutuhumiwa. Tukiingia tunajiandaa kutumiwa tutatumiwa kweli kweli. Tuamue na wananchi waandaliwe si kwa maneno bali kwa vitendo. Wakati ndiyo huu tuanze tena mapema. Wizara hii tuiwezeshe, Wizara hii ni muhimu sana, tuijenge na kuiimarisha kwa dhati kabisa na kwa nguvu zetu zote. Tukiiimarisha itatuwezesha kujiunga na majirani zetu, juu ya yote naunga mkono hoja.

**MHE. HEMED MOHAMED HEMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti,ni vema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uzima siku ya leo. *Alhamdullillah.*

Mheshimiwa Mwenyekiti,pia nachukuwa fursa hii kukupongeza wewe kwa umahiri wako hapa Bungeni. Pia nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Naibu wake kwa hotuba yao ambayo mwelekeo wake ni Shirikisho.

Baada ya maelezo yangu hayo napenda kutoa mchango wangu katika hotuba husika niseme, Watanzania bado kujiunga na Shirikisho la Afrika Mashariki ni vema Watanzania tuiangalie nchi yetu na nchi za wenzetu kiuchumi, kisiasa, kielimu pia kiusalama. Tukiangalia suala la uchumi kati ya nchi yetu, Kenya na Uganda kipofu na anayesikia anajua Kenya inaongoza. Je, kujiunga na mwenye kuwa nacho ili hali wewe maskini si kutafuta utumwa? Hatma ya utumwa ni kutawaliwa. Watanzania tumejitawala, tubaki tumejitawala hadi hapo uchumi wetu utakapokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu elimu, pamoja na dhana yetu kwamba Watanzania tuko mbele kielimu, mimi hili nina wasiwasi nalo. Moja ya sababu ya kukua kiuchumi kwa nchi ni elimu. Kama kweli hili ni vema tuwe wakweli. Uchumi wetu bado ni mdogo kutokana na ukosefu wa sifa ya upungufu wa watalaamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu lugha ya Kiswahili. Nchi yetu ya Tanzania ndiyo yenye wasemaji wengi wa lugha hii. Lakini watalaamu wa lugha hii zaidi wako Kenya na Uganda. La kusikitisha zaidi ni pale ilipoonekana lugha ya Kiswahili iwe lugha

ya Jumuiya ya Afrika na pia kuwepo kwa walimu wa lugha hii ili waweze kuzifundisha baadhi ya nchi duniani. Mpaka leo Watanzania bado hatujaamua lugha yetu ni ipi. Mfano mdogo ni Bajeti, vitabu vyote vinaandikwa kwa lugha ya kigeni (Kingereza), kwa kujua walio wengi lugha hii hawaijui, haki ya kusoma vitabu vinavyoonyesha azma ya Serikali yao juu yao hawawezi kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu usalama, kama Kenya na Uganda ina imani na somo hili basi walimu wao ni Tanzania. Nchi yetu imetulia sana na niseme mlio wa bunduki wao ni kufa kabisa. Hii ni kusema tunaishi kwa amani nchini mwetu. Tukiangalia Kenya kila leo watu wao wanauana kikabila. Uganda vita kila leo ni vita vya kijeshi, wanasiasa wanataka madaraka. Ni kweli hawa tutaweza kuishi nao, mtazamo mdogo ni vifo vya Watanzania vilivyosababishwa na ujambazi utasikia majambazi kutoka nchi jirani. Wenzetu hawajali kuua. Ni vyema Tanzania ibaki kama Tanzania yenye mwelekeo wa kupiga hatua kiuchumi, kielimu na kadhalika, ujamaa ni hali ya kuishi kwa pamoja kama vile ndugu, tuendelee na umoja wetu. Naitakia mafanikio mema Wizara husika. Ahsante.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda nichukue fursa hii kuipongeza Wizara na hasa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake akishirikiana na watendaji wote kwa kutoa hotuba nzuri yenye mwelekeo wa kuboresha uanzishwaji wa Jumuiya na Shirikisho. Napenda nichangie masuala machache ambayo ningependa nipatiwe ufafanuzi. Watanzania kama nchi tungefurahi sana kuingia katika Muungano/Shirikisho hasa ukiangalia hali halisi ya dunia, kwa kuwa kuna kutegemeana katika nguvu za pamoja kwenye kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kabla ya kuingia katika Shirikisho kunahitajika maandalizi kwani tumeona jinsi maoni ya wananchi yaliyokusanywa kwamba bado kuna kazi. Je, Serikali imejiandaa vipi katika kutoa elimu kwa jamii juu ya tofauti katika Jumuiya na Shirikisho la Afrika Mashariki, je, mkakati wa kutoa vitambulisho vya uraia unafikia wapi?

Je, Serikali imejiandaa vipi katika ushindani wa biashara na uwekezaji wa miundombinu hasa barabara za Afrika Mashariki ambazo zipo kisheria na uongezekaji wa viwanda?

Je, ni vipi wananchi watajengewa uwezo wa ndani na nini ushiriki wetu kama nchi kuelekea ushindani? Je, ni kwa kiasi gani wajasiriamali wadogo wadogo wameandaliwa/wataandaliwa ili kuweza kuingia katika ushindani wa fedha, ni vyema Serikali iongeze Wizara kwa hizi fedha. Kwa kuwa Kiswahili ndiyo lugha ambayo inatumika sana na kwa ufasaha Tanzania, mkakati endelevu uwekwe ili tuweze kuwa walimu wazuri na kutoa elimu kwa nchi nyingine za Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nipatiwe ufafanuzi wa hayo hapo juu. Naunga mkono hoja.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba kuchangia hoja ya Wizara hii na napenda Waziri wakati akijibu hoja atolee maelezo hoja zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu suala la Shirikisho, yamekuwa yakikusanywa maoni kuhusu Shirikisho. Kwa hakika wananchi hawaoni umuhimu wowote wa kuwa na shirikisho kwa kuzikaribisha nchi zenye matatizo ya kutokuwa na usalama wakati wote. Msukumo wa kuanzishwa Shirikisho kunatafsiriwa na wananchi kuwa ni kutoka kwa viongozi wenye uchu wa madaraka katika kuunda Shirikisho hilo. Kutokana na sababu hii ndiyo maana asilimia 80 wanataka kuanzishwa kwa Shirikisho kusiharakishwe mpaka tujiridhishe na nia ya hizo nchi zinazotaka kujiunga na asiliamia 20 ni idadi ndogo sana ambayo ndiyo yenye shinikizo. Kabla ya kuanza kwa Shirikisho, nashauri itolewe elimu kwa jamii kuhusu Shirikisho kwa kuelezea tofauti iliyopo kati Muungano na Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti,yapo mambo ya msingi ambayo yalitakiwa yafanyike kwanza na nchi zinazohusika kabla ya kukubaliana na suala la Shirikisho. Mambo hayo ni kuhusu miundombinu. Utekelezaji wa hilo ndilo litaonyesha kuwa nchi zote zina nia njema ya kujiunga na shirikisho hilo. Lugha iliyopo ni kuwa shirikisho litaibua vurugu zaidi ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu wakimbizi kutoka Burundi, juhudi za Serikali ya Tanzania ni kuondoa kero kubwa tuliyonayo ya kuendelea kuwa na utitiri wa wakimbizi. Tayari urejeaji wa wakimbizi kurudi kwao mbali na kuwa hali ni salama, wameanza kujua kuwa shirikisho ndio pekee litasitisha urejeaji wao kwa sababu litakuwa ni sehemu ya Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti,wakati yote hayo yanafanyika, nashauri wananchi wanaopata matatizo ya ukimbizi waonewe huruma. Zoezi hilo lisitishwe kwanza ili dhamira ya urejeaji wa wakimbizi kutoka nchi zenye wakimbizi likamilike.

Aidha, uandaliwe utaratibu wa haraka wa kupata vitambulisho vya uraia wa Tanzania ili muda wa Shirikisho ukifika iwe inajulikana idadi ya Watanzania. Mbali ya hiyo ni kuweka utaratibu wa kuwa na vibali vya kutoka nchi moja kuingia nyingine (*PPT*).

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya kupata maelezo kuhusu niliyoyauliza, nitaunga mkono hoja.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda nianze na kuwapongeza viongozi wetu kwa kukubali kuruhusu nchi ya Rwanda na Burundi kuwa sehemu ya Shirikisho. Hii itasaidia kupunguza migogoro inayoizungukia nchi hizi na baadaye huathiri nchi yetu.

Naomba Wizara hii izidi kuimarisha uhusiano mzuri wa mipaka. Mpaka sasa wananchi wanaoingilia mipaka ya Rwanda na Burundi wanaitwa wahamiaji haramu wakati wanaotokea Kusini si wahamiaji haramu, uhamiaji haramu usiwe wa mkoa mmoja

tu (Kagera), suala hili linakuzwa na tatizo la ukabila. Naomba ushirikiano huu uangalie tofauti hizi zinazojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mwisho suala la *East African Partnership* itakuwaje baada ya Shirikisho. Nchi tano hizi zinaingiliana na kusaidiana vipi? Je, miundombinu ipi itapewa kipaumbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba ufafanuzi wa hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara hii ya Afrika Mashariki. Ni Wizara mpya na huu ni mwaka wa pili wa Bajeti hii ya Wizara ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nchi hizi tatu Tanzania, Kenya na Uganda zinahistoria zinazofanana tangu wakati wa Uhuru, tukivua magwanda yetu tukasimama mstari huwezi kutofautisha Mtanzania, Mkenya na Mganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kama alivyosema Waziri kuwa jukumu kubwa la Wizara ni la kiutaratibu. Ni muhimu katika kuratibu huku Wizara ikashiriki kikamilifu kushirikiana na Wizara nyingine ili tunapozungumza juu ya Afrika Mashariki kila sekta ikawa imejiandaa. Wizara inapaswa pia kushauri Wizara nyingine kama ya elimu, viwanda mwelekeo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ili tupate kujiandaa kama Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,aidha, suala la kushirikiana hasa kwa nchi zinazoendelea ni suala la msingi kushirikiana kiuchumi ili tuwe na soko kubwa, sarafu moja na hatimaye Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ninaposema ushauri ni kama kuishauri Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Katiba na Sheria iweze kujiandaa na masuala ya ardhi yatakuwaje. Jukumu la ushauri *(advisory role)* ni jukumu la msingi ili Wizara zetu zingine ambazo zinaingia katika masuala ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ziweze kufanya vizuri na hatimaye maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti,baada ya majibu juu ya jukumu la kuishauri *(advisory role)* na haja zingine katika Wizara nitakuwa tayari kuunga mkono hoja. Hivyo jukumu la Wizara liwe kuratibu na kushauri masuala yote yenye uwiano na Jumuiya ya Afrika Mashariki kushauri masuala ya fedha, elimu, ardhi na kadhalika.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa mara nyingine kupata nafasi ya kutoa maoni yangu, japokuwa kwa maandishi. Awali ya yote namshukuru *Allah* kwa kutuweka katika hali ya afya njema wote kwa ujumla hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nikianza kuchangia hotuba hii kwanza nampongeza Waziri kwa kuwasilisha hotuba yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu Afrika Mashariki nina maoni kuwa kufanya Shirikisho sio tatizo hata kidogo ila lisiharakishwe kama wanavyotaka viongozi wetu. Sijui mimi viongozi wana haraka ya nini kuhusu suala hili!

Mheshimiwa Mwenyekiti,nchi zetu za Afrika Mashariki bado zenyewe zina matatizo ya ndani ya nchi hata siasa zetu bado hazipo safi hususani Tanzania na Uganda, haijambo kidogo Kenya kwa hili ingawa nako kuna siasa za ukabila. Hapa Tanzania ni nchi ya vyama vingi lakini mpaka leo kuna baadhi ya wananchi wanasumbuliwa kwa sababu tu ya kujiunga na vyama vya upinzani na bado watu wenye elimu na wafanyabiashara hawajiungi na vyama wanavyovipenda kwa sababu tu ya kuogopa Serikali ingawa Serikali hili ukilisema inajitetea lakini ukweli ndio huo.

Meshimiwa Spika, vile vile kuna tatizo la mpasuko wa kisiasa huko Visiwani Unguja na Pemba na mpaka hivi sasa halijashughulikiwa na Serikali ya Tanzania lakini inashugulikia mambo ya nje wakati ndani kwetu kuna tatizo. Hivyo basi mimi napendekeza kwanza haya matatizo ya ndani tumalize kwanza na ndio tuingie kwenye mambo mengine ya nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti,mimi kwa leo sina zaidi ila ni kutoa maoni yangu haya tu, ahsante sana.

**MHE. AME PANDU AME:** Mheshimiwa Mwenyekiti,kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nami nitoe mchango wangu kuhusu Wizara hii ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ili Wizara yetu iweze kumudu kuendesha majukumu yake, Wizara hii iongezewe pesa zaidi kwenye Bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara hii inakabiliwa na majukumu makubwa ya kiutekelezaji sawa na Wizara nyingine. Kwa hiyo, Serikali iangalie vizuri zaidi katika kuipangia Bajeti Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Serikali pia iangalie vizuri juu ya ardhi ya Tanzania kwa hawa wenzetu wa Kenya, Uganda, Burundi na Rwanda. Wenzetu hawa wameshajiweka tayari kwa kuzivamia rasilimali zetu zilizomo humu Tanzania na Watanzania bado kabisa hawajajiweka tayari kwa lolote juu ya Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Shirikisho la Afrika Mashariki halitatusaidia lolote Watanzania bali linaweza kuwanufaisha hao wenzetu tu. Sisi wenyewe Watanzania yaani Tanzania Bara na Zanzibar bado tunzao kero za Muungano hatuwezi kuzitatua, tunakwenda kuzidisha matatizo, je, tutakuja kufanya nini mambo yatapokuja kuzidi kusonga? Watanzania tusijitie tu katika matatizo kwa tamaa ya utajiri tusio na uhakika nao hiyo ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja kwa asilimia arobaini tu.

**MHE. STEPHEN J. GALINOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuthibitisha kuwa naunga mkono hoja hii.

Pili, naelewa haja ya kujenga ushirikiano miongoni mwa nchi za Shirikisho la Afrika Mashariki kwa njia za kutumia vyombo vya habari. Lakini kuna uhalali au umuhimu gani kuonyesha hapa Tanzania katika *TV* matukio madogo madogo yasiyo na maana yoyote kwetu? Kwa mfano, ni jana tu *ITV* ilituonyesha tingatinga linazoa takataka mjini Kampala. Iko mifano mingi ya taarifa za kipuuzi kama hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nashauri Serikali iangalie na hoja ya kufanya hivyo isipokuwa katika matukio makubwa na muhimu. Tuwe *selective.* Papo hapo kuna hakika gani kwamba Kenya na Uganda nazo zinatutangaza sisi Tanzania katika nchi zao? Mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. ALI AMEIR MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninampongeza Waziri na wasaidizi wake kwa hotuba yake fasaha. Wizara hii inapaswa kuwa ya Kimuungano kwa sababu ilivyojiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini mpaka sasa Wizara hii haioneshi muundo wa Kimuungano, inaonekana hata Rais alipounda Wizara hii haikufuata ule utaratibu wa Wizara nyingine za Kimuungano ambapo Waziri akitoka upande mmoja wa Muungano, NaibuWaziri hutoka upande wa pili wa Muungano. Si hivyo tu hata watumishi wa Wizara hiyo karibu wote wamechukuliwa kutoka upande mmoja wa Muungano mpaka hivi karibuni alikuwepo mtumishi mmoja tu kutoka Zanzibar, tena aliazimwa kwa muda kutoka Wizara ya Mambo ya Nje. Kama tujuavyo Jumuiya inashughulikia mambo ya Ushirikiano ambapo si ya Muungano kwa mfano mambo ya uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu kukosekana kwa kitengo maalumu katika Wizara kinachoratibu maslahi ya Zanzibar katika Jumuiya nadhani ni kasoro. Sijui hivi sasa maslahi ya Zanzibar yanawakilishwaje katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti,lipo suala la wananchi kuelewa vizuri Jumuiya katika mchakato wa kupata maoni juu ya wazo la kuharakisha Shirikisho la kisiasa la Afrika Mashariki iliidhihirika wazi kuwa wananchi walio wengi hata hawajui kuwapo kwa Jumuiya ya sasa na inafanya nini. Mimi nashauri Wizara ifanye juhudi maalumu kuwaelimisha wananchi kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki .

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa kuwa Watanzania wengi wameonesha kutotaka kuharakishwa kwa Shirikisho, ni vema hatua zinazochukuliwa za kukamilisha mtangamano wa kufikia Shirikisho zikaeleweka vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Jumuiya nalo ni jambo la kutiliwa mkazo. Inaonekana pamoja na uamuzi wa kutumia Kiswahili kuwa lugha mojawapo ya Afrika Mashariki inaonekana Kiingereza ndicho

kinachotawala. Hali hii inapaswa kutekebishwa ili Kiswahili kipewe nafasi yake katika shughuli za Jumuiya. Kwa ujumla suala la ushirikiano ni jema lakini uwe ushirikiano wa wananchi na siyo wa mikutano ya uongozi tu. Hawa wananchi hawaeleweshwi yanayoamuliwa na hawaoni faida yake katika maisha yao ya siku kwa siku hata hii Jumuiya itakuwa kero badala ya chombo cha kuwaletea maendeleo wananchi wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,pamoja na maoni hayo naunga mkono hoja nikutumaini Wizara itafanya jitihada za kuwashirikisha wananchi kikamilifu tu.

**MHE. FATMA ABDUKHABIB FEREJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti,naomba kuchangia hoja hii inayohusu Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu suala zima kuhusiana na Jumuiya ya Afrika Mashariki halieleweki kwa wananchi walio wengi. Bado wananchi wana maswali mengi wanayojiuliza kuhusiana na faida itakayopatikana kutokana na Tanzania kuwa katika Jymuiya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati ya Rais ya kukusanya maoni juu ya uharakishwaji wa uundwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki ilipokuwa ikipita nchini kwa kazi hiyo, ilipata kazi nzito kutokana na uelewa wa wananchi wetu juu ya suala hilo. Ingekuwa vizuri sana kama wananchi wenyewe, wawakilishi wao yaani Wabunge, wangeshauriwa juu ya uanzishwaji wa Jumuiya hiyo kabla ya wakuu wa nchi kuamua kuanzisha tena Jumuiya hiyo iliyovunjika mwaka 1977. Kinyume cha hayo, viongozi wakuu ndio walioridhia uanzishwaji wa Jumuiya hiyo mpya mwaka 1999 na sasa ndio maoni ya wananchi juu ya kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki yanatafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,maoni ya wananchi wa Tanzania kwa asilimia 79.9 wamekataa kuridhia uharakishwaji wa uundwaji wa Shirikisho la Afrika Mashariki. Naiomba Serikali izingatie kwa makini maoni hayo ya wananchi katika suala hilo kwani maamuzi ya Serikali katika suala hilo yana athari kubwa kwa maisha ya kila siku ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ni vizuri pia sisi kama Watanzania tutatue matatizo yetu ya ndani yaani Muungano. Ni vyema basi tukashughulikia utatuzi wa kero za Muungano wetu ili tutakapofikia katika hatua ya Shirikisho la Afrika Mashariki tuwe wenyewe tuko kitu kimoja na hatuna matatizo ya ndani. Naomba kuwasilisha!

**MHE. MBAROUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watalaamu wengine wa Wizara hii muhimu kwa hotuba yao nzuri sana na kwa kazi nzuri na mahiri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti,suala la Umoja wa Forodha bado lina matatizo makubwa. Kwanza, wananchi wengi hawana uelewa wa kutosha. Kuna umuhimu mkubwa wa kuelimisha wananchi. Pili, wenzetu wa Kenya bado wana vitimbi vingi vya *non-tariff barriers*. Tatu, yapo makundi Kenya yanayojihusisha na *organized smuggling*.

Mheshimiwa Mwenyekiti,wananchi wetu wanapata shida sana kuingia na kuishi Kenya. Huwa wananyanyaswa sana kutokana na hali hii na ukweli kwamba hali ya kisiasa Kenya na kwingineko katika jamii si tulivu kama Tanzania. Ni maoni yangu kwamba pasiwepo haja ya kuharakisha mchakato wa kufikia *Political Federation.*

Mheshimiwa Mwenyekiti,suala la *Joint Negotiations* katika *WTO, WIPO, EEC/ACP* na kadhalika ni muhimu kwa kuzingatia umuhimu wa kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na *synergies* katika majadiliano na wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ipo haja ya Serikali kuamua haraka iwezekanavyo kuhusu Jumuiya ambayo Tanzania itaendelea kuwemo katika majadiliano ya *Economic Partnership Agreements (EPA)* kwa kuzingatia kwamba sisi tupo katika kundi la *SADC* na wenzetu wengine wapo katika kundi la *ESA*. Hali hii ikiendelea bila uamuzi thabiti ufaao, ipo hatari kubwa ya kudhoofisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,naunga mkono hoja asilimia mia moja na kuitakia Wizara utekelezaji mwema na wa mafanikio.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,kuhusu Shirikisho la Afrika Mashariki, mimi nitakuwa na mitizamo tofauti na Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tanzania hatupo tayari kwa ajili ya hili Shirikisho. Awali ya yote viwanda vyetu vimebinafsishwa, hatuna viwanda vya ku-*produce* vitu vya ku-*offer* katika soko hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nchi kwa mfano Kenya, wao wali-*invest* sana kwenye *Human Capital,* hivyo tayari wana wataalamu wengi pia wanavyo viwanda vingi sana. Kwa mfano, *Supermarket* zote nchini vitu vyote vilivyoko ndani ya maduka haya vinatoka Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Shirikisho likianza Tanzania tunajiandaa kuuza bidhaa gani ili tuweze kushindana na wenzetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti,vile vile kuhusu hili Shirikisho, lianze kwa awamu kwa kuwaelimisha tuanze kwanza labda na *customs union,* ikifanya kazi, tunaendelea na vingine. Hii itawapa watu moyo wa kwamba hili linafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,watu walishaona Jumuiya ya Afrika Mashariki ilikufa, watahitaji wapewe matumaini/imani kwamba haiwezi kuvunjika tena. Pia katika Shirikisho, naamini kabisa maoni kutoka kwa wananchi yatapewa kipaumbele, wasije wakayachukulia maamuzi ya kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nashauri Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuwe na programu maalumu shuleni *especially* kuendeleza kazi za viwandani, kupata wataalamu.

Baada ya hapo kuwe pia na ushirikiano na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko jinsi ya kufufua viwanda vyetu. Siyo hivyo tu, Wizara ya Kilimo na Wizara ya

Mifugo kuwasaidia kilimo cha kisasa na bidhaa hizi ziwe *processed* hapa hapa ili tuweze kushindana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Tanzania tuna vitu vingi sana vya ku-*offer,* hivyo tukiwa na mipango mizuri na hizi Wizara kushirikiana, tutakuwa wa kwanza kwa vitu zaidi ya wengine. Bila kusahau utalii tulionao Tanzania ambao haupo katika nchi nyingine zozote Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara ya Miundombinu ni muhimu sana kuhakikisha barabara zetu zinapitika mpaka vijijini na umeme uwepo kuanzia ngazi za vijiji ili tuwaonyeshe Kenya kila kitu kinatokea Tanzania.

Mheshimwa Spika, Tanzania ni nchi yenye amani siku zote. Tumeona katika mabenki yetu, wezi/majambazi yote yanatokea nchi jirani! Swali, je, Serikali imejiandaa namna gani kudhibiti haya majambazi wakati hata Shirikisho halijaanza?

**MHE. COL. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakupongeza wewe kwa jinsi ya uwezo wako mkubwa wa kuliongoza Bunge letu Tukufu vizuri; haki kwa kila Mbunge na busara za hali ya juu kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuimarisha vyema Wizara yetu ya aina yake ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kutamka mapema kwamba naunga mkono hoja ya Wizara kwa asilimia mia moja. Aidha, naomba kutoa maoni yangu machache kama ifuatavyo:-

Moja, naiomba Serikali yetu pamoja na Mkuu wa nchi wetu tujipange vizuri na tujitayarishe kielimu, utaalamu na mambo mengine kulingana na hali ya utandawazi iliyopo.

Pili, lengo kubwa la ushirikiano unaotajwa ni kuimarisha uchumi wa nchi zetu, kwa maana hiyo ni vyema tukaimarisha vizuri bandari zetu, viwanja vyetu vya ndege na miundombinu yetu.

Tatu, wakati tukielekea kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki, lazima tuwe na tadhadhari ilivyokuwa Tanzania ina eneo kubwa la ardhi tena yenye mali na utajiri mkubwa, tujihadhari na wawekezaji, watakuja kuchukua ardhi na mali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarejea tena kusema ninaunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia na kubakia na matumaini kwamba Serikali itayaangalia kwa utulivu masuala yote ya manufaa ya watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kuwasilisha.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni nyeti sana hasa katika dhana nzima ya diplomasia ya uchumi. Naamini kabisa pamoja na suala nzima la kuwa na Jumuiya ilikuwa ni kutokana na historia ya nchi zote tatu. Ukizingatia mila na desturi zetu hazitofautiana sana. Pamoja na hayo lakini sababu zingine zilizopelekea Jumuiya yetu hii ni za kiusalama, kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kujielekeza zaidi kwenye suala zima la diplomasia ya uchumi kwani naona ndio kitu kikubwa katika dhana nzima ya Muungano wa nchi zote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti,nina wasiwasi na hali ya uchumi wetu kuwa nyuma ya nchi wanachama wa Jumuiya hii hali ambayo inatia wasiwasi Watanzania wengi. Tuko nyuma karibu katika kila kitu. Maandalizi ya kutosha yanatakiwa katika kuinua uchumi wetu. Wizara hii inatakiwa iwe kichocheo kwa Wizara nyingine kama Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko hata Wizara ya Nishati na Madini katika kuongeza hali yetu kutoka ilipo sasa kuelekea katika hali nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Wizara hii ihakikishe itifaki ya Umoja wa Forodha inanufaisha nchi yetu pia ambapo ilianza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2005. Nchi wanachama zinalenga kupunguza vikwazo visivyo vya ushuru *(non tariff barriers)* kwa lengo la kuboresha mazingira ya kuendeleza biashara katika Jumuiya nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana ya kutaka itifaki hii ihakikishwe na Wizara inanufaisha nchi ni katika kutoa msukumo kwa Wizara nyingine na wananchi kwa ujumla katika kukuza uchumi ili na sisi tuweze kusafirisha vitu kuelekea nchi wanachama kuliko sisi kuwa wapokeaji, matokeo yake litageuka soko lao hasa la nchi ya Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nchi yetu haijazifikia nchi za Kenya na Uganda katika sekta ya elimu kuanzia ya awali mpaka ya juu. Pamoja na uchache wa wahitimu wa Vyuo Vikuu ni mdogo, lakini pia elimu ya sekondari ya Tanzania elimu itolewayo siyo bora ukizingatia hata maabara hatuna katika shule za msingi na sekondari zetu. Hii inaonyesha kuwa watalaamu wengi watatoka Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni vyema Wizara hii ikashauri Wizara zinazohusika na elimu ya awali mpaka Vyuo Vikuu zihakikishe zinaboresha utendaji wake ili kushindana katika soko huria hasa la ajira na sayansi na teknolojia. Kwani naamini Wizara hii ina maono zaidi kwani inashirikiana kwa karibu na Wizara kama hii zilizopo katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Wizara muhimu sana, inahitaji ushirikiano kutoka nchi nzima, kwa wananchi na Wizara karibu zote ikiwepo Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia bila kuzisahau Wizara ya Nishati na Madini ikiwemo ya

Viwanda na Biashara na Masoko. Tuondoe hofu Wizara hizo zijizatiti kukabiliana na *challenge* zilizopo ili nchi yetu isitetereke katika Jumuiya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mchango wangu uzingatiwe. Wizara hii haitakiwi iachwe pekee yake, haiwezi kufika mbali katika Shirikisho hilo.

**MHE. PROF. PHILEMON M. SARUNGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniruhusu kwa niaba ya wananchi wa Wilaya mpya ya Rorya ambayo kwa nchi kavu inapakana na Jamhuri ya Kenya na Majini katika Ziwa Victoria inapakana na Jamhuri ya Kenya na Jamhuri ya Uganda kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, wataalamu wa Wizara na wakuu wa vitengo kwa kuletea Bajeti iliyoandaliwa kwa makini na kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutamka kuwa ninaunga mkono hoja hii. Baada ya pongezi hizo naomba kutoa maoni au ushauri kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 28 wa katibu cha hotuba ya Waziri kuhusu Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria. Nashauri kuwa Tume hiyo isambaze huduma zake katika vijiji vilivyopo kando kando mwa Ziwa Victoria kwa kufungua ofisi ndogo katika maeneo wanamoishi wanavijiji kando kando ya Ziwa Victoria. Katika Wilaya ya Rorya kuna vijiji 34 kandokando ya Ziwa Victoria. Bandari ya Sota ni bandari kubwa katika Wilaya ya Rorya. Nashauri ofisi ndogo ya Kamisheni ya Bandari ya Victoria ifungue kituo Sota kwa ajili ya kusimamia mazingira na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii katika vijiji 34 kwa faida ya wakazi wa Tarafa ya Nyamcha Wilaya ya Rorya. Naomba Kamisheni itakapoanza shughuli zake, ushauri/ombi hili lizingatiwe kupitia Wizara. Ukurasa wa 29 kuhusu miradi ya maendeleo ukurasa wa 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri/ombi langu ni kuhusu mradi wa kuendeleza makazi ya wananchi waishio kando kando mwa Ziwa Victoria. Mradi huu usikomee katika kuhusisha miji 22 tu katika nchi tatu, bali pia uhusishe vijiji kama vile vijiji vya Sota, Msonga, Mningo, Rwangenyi, Nyangombe, Nyihara, Kibuyi na Kinesi ni baadhi ya vijiji vyenye wavuvi na mialo mikubwa. Katika vijiji 34 wanavijiji wameunda vikundi vya kusimamia hifadhi ya mazingira ya Ziwa Victoria *(Beach Management Unit)*. Naomba Wizara iwashirikishe wananchi waishio kando kando mwa Ziwa Victoria, Wilaya ya Rorya kuibua miradi ya maendeleo katika vijiji vyao ili waweze kunufaika na mradi huu wa kuendeleza makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Rorya, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ziara aliyofanya Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Wizara ifuatilie kwa makini uamuzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kujenga soko la biashara katika kijiji cha Kirongwe, Kata ya Buhura, Tarafa ya Nyamcha, Wilaya ya Rorya. Kama uamuzi huu haupo, wananchi wa Rorya wanaomba iingizwe katika miradi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu Umoja wa Soko na Forodha. Kijiji cha Kirongwe ndicho kitakuwa kituo cha uhamiaji katika Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Nampongeza mtoa hoja, Waziri mwenye dhamana, nampongeza Naibu Waziri kwa jinsi anavyonisaidia Waziri na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu lugha ya Kiswahili. Kiswahili ni lugha inayozungumzwa takribani na Watanzania wote. Vile vile, Kiswahili kinaeleweka na kuzungumzwa hata kama ni kwa uchache na nchi zote zilizozunguka zikiwemo Malawi, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda na Congo *(DRC).*

Kiswahili kipewe uzito na umuhimu wa kipekee katika kukikuza, kukitumia na kukienzi katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ingefaa Kiswahili kitumike sana kuliko hivi ilivyo sasa. Wanatakiwa wakalimani katika matukio mbalimbali ikiwa imekubalika kutumika katika Bunge la Afrika, basi kumbe Kiswahili kinakubalika kipewe nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Kiswahili, ipo lugha moja inakua na itakuja kuhitajika na kutumia sana Afrika Mashariki, hiki ni Kifaransa. Kwa kuwa tutakuwa tunapokea wageni kutoka nje, Watanzania watapwaya na kukosa ajira fulani fulani kwa sababu ya kutojua Kifaransa, kwa hiyo, sambamba na Kiswahili, Kifaransa kisionwe kuwa ni lugha isiyotuhusu Wizara nilizozitaja, mshirikiane nazo ili Kifaransa kifundishwe sana mashuleni kwetu.

Pili, uboreshaji wa bandari zetu ni muhimu sana. Ili kuwepo na ushindani wa kiuchumi katika Afrika Mashariki, bandari zinategemewa sana. Tanzania iweke nguvu mpya katika kukuza na kuboresha utendaji wake wa kazi bandari zetu, ikiwemo Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili zipokee mizigo mingi hali itakayonufaisha nchi yetu kiuchumi, zikiwemo ongezeko la nafasi za ajira, mapato ya nchi na kukuza miundombinu mingine zikiwemo barabara na miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari zetu zitupiwe macho kupitia Wizara hii. Kwa hiyo, basi wawe wakatengewa fedha za maendeleo ili waweze kuyashughulikia maeneo yanayowagusa kama hili la bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nisemee suala zima la vitambulisho vya uraia viwahi pamoja na kuwatambulisha Watanzania, iangaliwe kuilinda ardhi yetu isijekuporwa na wageni. Hapa liangaliwe suala linaloendelea kujadiliwa la uraia wa nchi mbili, wenye uraia wa nchi mbili wasikubaliwe kumiliki ardhi yetu maana hii ni rasilimali isiyohamishika, ibaki kwa wenye uraia wa Tanzania pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kuwatakia heri katika kazi za Wizara husika. Nawasilisha.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza Wizara hii inayosimamiwa na Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala na Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi zao na kuwasilisha hotuba ya Bajeti ya matumizi ya fedha kwa awamu hii ya Serikali ya Nne inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa makusudi juhudi ichukuliwe na Wizara kuhusu Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuwe na mambo maalumu kwa mambo ya Bajeti iwe ya kudumu Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa vitambulisho vya uraia ili kuepuka wageni wasiotambuliwa na wanaosumbua au wahalifu pindi Shirikisho la Afrika Mashariki lianzapo jitihada za ukamilishaji kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu iwepo kikamilifu kwa mtandao wa Afrika Mashariki, barabara na mambo mengine ya kushirikisha biashara bila matatizo. Sekta hii sera zake ziwe kikamilifu na ziwe za faida lakini lengo kubwa Tanzania tunafaidika vipi? Kwa jukumu la Serikali liandae na kusimamia sio usemi tu Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Bunge letu la Afrika Mashariki basi liwe na uwiano na utekelezaji wake. Tanzania ilete tija na kuleta maendeleo ya uchumi na mambo ya faida kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Kitengo hiki kiwe cha msingi Mahakama ya Rufaa, muundo uwe wa kulingana wakati kungali haki sio wa kusumbua kama mfumo wa awali Majaji wawe kama Majaji na maamuzi au hukumu zizingatie sheria ya ushirikiano wetu. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Magogoni walioniwezesha kuwa Mbunge na mimi mwenyewe. Naunga mkono hoja mia kwa mia.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Katibu Mkuu wa Wizara na watumishi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni Wizara mtambuka *(cross cutting),* Wizara hii inaingia maeneo yote yanayohusu mtengamano wa Jumuiya yetu ya Afrika Mashariki, ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki ni wa muhimu sana kiuchumi na kiusalama, Jumuiya ya Afrika Mashariki inaunganisha ushirikiano wa nchi zetu kikanda, uhusiano wa kindugu, kibiashara na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inagusa maeneo mengi ya kila Wizara ndani ya Serikali yetu, kwa maana masuala ya ulinzi ni lazima yawemo katika Wizara hii, kadhalika viwanda, miundombinu, afya na kadhalika yote lazima yaiguse Wizara hii katika kuoanisha majukumu na mashirikiano ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kuona Wizara pamoja na unyeti wake, kiwango cha fedha zilizotengwa kwa Bajeti ya mwaka 2007/2008 bado ni kiwango kidogo kiuendeshaji, naomba Serikali itoe kipaumbele na kuijali Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwenye masuala ya nchi yetu katika mashirikiano ya Jumuiya hii naomba yafuatayo yazingatiwe:-

(i) Kuendelea na elimu zaidi kuhusu kuelimisha wananchi wetu juu ya masuala yote yanayohusu Jumuiya, nini maana ya Jumuiya na faida zake.

(ii) Wananchi tuwaandae katika ushindani wa soko kibiashara ili kuharakisha maendeleo ya nchi na wananchi kwa ujumla.

(iii) Itifaki izingatiwe kama ilivyopendekezwa awali kabla ya kufikia Shirikisho Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, sarafu moja na kisha Shirikisho.

(iv) Maoni ya wananchi wa Tanzania kuhusu Shirikisho yazingatiwe na yasipuuzwe ile 79.5% iheshimiwe na Wizara ifanye ufafanuzi juu ya hoja zinazokataa kuharakisha Shirikisho zilizotolewa na asilimia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi za Burundi na Rwanda zinapatikana uanachama wa Jumuiya juhudi za kuzipima na kuzichunguza nchi hizi kimienendo kutokana na tabia za nchi hizi hasa kuhusu masuala ya amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje ambaye pia inashughulikia Wizara hii, naomba Wizara izidishe juhudi za kuitangaza sana jumuiya kwa wananchi ili wananchi wetu wajiandae kabla ya Shirikisho. Naunga mkono hoja.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, umefika wakati Tanzania ibadilike hasa pale ambapo inajiunga katika taasisi mbali mbali za kiuchumi badala ya kujiunga kama Tanzania ijiunge kama Tanzania Bara na Zanzibar. Suala la kujiunga katika Ushirikiano wa Afrika Mashariki kama Tanzania na Zanzibar kuingizwa humo halikuwa na maslahi ya kiuchumi wala kujenga nguvu za uamuzi kwa Tanzania katika Ushirikiano huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kama katika Ushirikiano huo ingekuwa Tanzania Bara (Tanzania) na Zanzibar ni wanachama kila mmoja basi katika ushirikiano huo tungekuwa na wajumbe 18 katika Tanzania, kwa hilo ni dhahiri nchi yetu ingakuwa na nguvu kubwa ya kura katika Ushirikiano huo. Pia hata mgawanyo wa miradi ya maendeleo taabani tungefaidika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuuliza Mheshimiwa Waziri ingekuwa kama nilivyoeleza nchi yetu ingapoteza nini? Kama tatizo ni Katiba basi ipo haja ifanyiwe marekebisho ili itakapofika wakati wa kuwa na shirikisho basi Zanzibar iwemo kama nchi kwa ajili ya maslahi kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu tulikuwa katika mchakato wa kuulizwa juu ya uharakishwaji wa kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki chini ya Tume ya Profesa Samwel Wangwe. Lililojitokeza katika mchakato huo kuwa inavyoonekana uamuzi wa kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki umeshafanywa. Jambo hilo ni zito na kubwa na wananchi hawakushirikishwa. Ni vyema ili uamuzi huo ufutwe na baadala yake washirikishwe wananchi kama walivyoshirikishwa katika Tume ya Profesa Samwel Wangwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kuwa na Umoja au Shirikisho la nchi za Afrika. Lakini suala la kuwaruhusu nchi za Burundi na Rwanda kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki, umekuwa wa haraka mno. Leo nchi hizo hata wakimbizi kutoka nchi zao hawajamalizika kurejea kwao. Tuone mfano wa Uturuki katika kujiunga na Jumuiya ya Ulaya ambapo imepata utulivu wakati wote lakini ili ikubaliwe kujiunga ni mwaka 2017. Je, Mheshimiwa Waziri haoni haraka hizo zinaweza kutuletea matatizo.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Kwanza napenda kutoa pongezi kwa kuiendesha Wizara mpya. Naiunga mkono hoja kwa asilimia mia Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wabunge wa Afrika ya Mashariki kutoa ripoti Bungeni Tanzania. Tunaona Wabunge watokao Tanzania hatupati sehemu tena ya kuonana nao baada ya kuwachagua, je, Serikali haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuweka mipango maalumu ya kuwapa nafasi ya kuleta waliyoyapata katika Bunge la *East Africa* na vile vile sisi tuwatume mambo yetu ya Tanzania yaani tupate ukumbi wa kuwa nao kwa mazungumzo rasmi ndani ya Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ziwa Victoria, mavuno ya samaki yote huvunwa sana na Kenya na Uganda kwa vile wao wana vifaa. Tuangalie uwezekano wa sisi wote kuwa na mavuno sawa.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono Bajeti ya Wizara hii na sina pingamizi nayo isipokuwa napenda kutanabahisha kuwa huu ni ushirikiano, kwa sasa kwa nchi tatu, kuelekea kwenye nchi tano. Tanzania ni nchi mbili zilizoungana na wakati tunapoenda kwenye Jumuiya hii, tunaenda kama Tanzania, kupitia kwako, lakini vile vile, kupitia kwa Wizara hii sasa umefika wakati, baadhi ya mambo yawekwe bayana hasa yahusuyo uchumi wa Zanzibar. Zanzibar ni Kisiwa, kina uchache wa ardhi na kimezungukwa na bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Muungano kama itakuwa na dhamira ya kweli kuisaidia Zanzibar hapana shaka Shirikisho na Jumuiya hii itakuwa na manufaa makubwa sana kwani sote, ni vizuri kwa hiyo basi waangalie, ama kwa Tanzania au Afrika ya Mashariki, Zanzibar itaachiwa sehemu kubwa kujiimarisha, kiutalii, bandari na uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu kubwa hizi waachiwe Zanzibar kutokana na mazingira ilio nayo kimaendeleo na kadhalika mfano Makao Makuu ya Sekta ya Utalii

iachiwe Zanzibar, kiuratibu na kiusimamizi, Makao Makuu ya Bandari ya *East Africa* yawe Zanzibar na kuimarishwa viwanda vikubwa vikubwa vya uvuvi katika Kanda Mashariki ya Bahari ya Zanzibar wakati hayo yanaendelea, tufanye hima Serikali ya Muungano kumaliza suala la uchimbaji wa mafuta au madini Tanzania kwa hivyo, tuhimize Serikali zote mbili ya Muungano na Zanzibar (SMZ) zikamilishe namna ya mgao wa mafuta na madini muafaka ufikiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa kwenye matarajio ya kupata mafuta na Uganda hivyo hivyo, sasa wakati tutakapooanisha nyanja za soko la pamoja na labda baadae Shirikisho, mambo haya yawe tayari yamepatiwa ufumbuzi. Miaka mitano iliyobakia kufikia mwaka 2013 ni muda mdogo sana na kumbe hivi sasa tumechelewa. Wakati huo tutakapotaka kufanya Shirikisho la nchi hizi tatu nalo liwe limeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala lililo mbele yetu la Jumuiya ya Muungano wetu kiuchumi kama ya *SADC, East Africa* na *COMESA*. Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake jioni ningemwomba sana afafanue utata uliopo juu ya suala hili. Inaonekana kuibuka makubaliano ya baadhi ya nchi hizi tatu kwa tano baadhi zipo *COMESA* hazipo *SADC* na baadhi ziko *SADC* hazipo *COMESA* lakini la ajabu ni kuwa baadhi ya hizo nchi kama Uganda, Kenya na Tanzania wameshakuwepo na kujenga uwezo na mwelekeo wa soko la pamoja la *East Africa.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo yatakuwaje? Ni kweli katika mfumo uliopo hivi sasa itawezekana tuunde na mifuko mitatu sambamba. Hii ni dalili ya mambo kutushinda au umoja wa kati ya nchi hizi kuvunjika.

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, yeye atachangia kwa muda wa dakika 20.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Naungana na Mheshimiwa Waziri, kutoa rambirambi na pongezi zote alizozitoa leo hii asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwa kujibu baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali. Naomba kwa kuanza nianze na hoja aliyochangia kwa maandishi, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, alieleza kwamba kuna vikwazo vingi visivyo vya kodi. Wengine wengi wameeleza kwamba, kuna vikwazo vya namna hiyo miongoni mwa nchi wanachama. Naomba niseme kwamba, kifungu cha kumi na tatu kupitia Itifaki ya Umoja wa Forodha, kinazitaka nchi wanachama wote kuondoa vikwazo visivyo vya kodi. Lakini vilevile itifaki hiyo ya Umoja wa Forodha, kifungu cha 41, kinaeleza utaratibu wa kisheria utakaotumika kwa nchi itakayoonekana kuendelea kuweka vikwazo visivyo vya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kutambua kwamba, vikwazo visivyo vya kodi vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara, leo unaondoa hivi

kesho vinakuja vingine, lakini mbaya zaidi vikwazo hivi mara nyingine vinahamasishwa na wafanyabiashara wenyewe kwa kutaka kuzuia wafanyabiashara wengine wasinufaike na soko husika. Tarehe 22 Julai, 2007 katika nchi yetu, tumezindua Kamati ya Kitaifa itakayofanya kazi ya kuratibu na kushughulikia maswala yote ya vikwazo visivyo vya kodi. Kazi kubwa ya Kamati hii itakuwa ni kupokea kwa haraka, malalamiko yoyote kutoka kwa wafanyabiashara yoyote na kuyafanyia kazi kwa haraka. Kamati hii inaratibiwa na Wizara ya Afika Mashariki, lakini ina wajumbe mbalimbali, ambapo ingekuwa ni vizuri niwataje hapa ili kila mmoja aweze kuelewa.

Kamati hiyo ina wawakilishi wa *CTI*, Kamati hiyo inawawakilishi kutoka Tanzania *Chambers of Commerce*, *Industry and Agriculture*, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, wawakilishi kutoka *TANROADS*, *TRA*, Serikali za Mitaa, Chama cha Wasafirishaji wa Mizigo na wawakilishi wa Wafanyabiashara. Kwa nini wapo wote hawa? Wako wote hawa, kwa sababu unakuta vikwazo visivyo vya kikodi mara nyingi vinatoka sehemu mbalimbali.

Wakati mwingine vinaweza vikatoka kwenye masuala ya barabara au masuala ya afya. Kwa hiyo, tunasema Kamati hii ipo na wafanyabiashara wetu tutawapa fomu ambazo watakuwa wanaendanazo, ukifika pale mpakani unakwenda Kenya, likitokea tatizo unajaza fomu ile na badala ya kusubiri kuwasilisha fomu ile, unaweza ukapiga simu kwenye Wizara ya Afrika Mashariki na sisi tutalifanyia kazi haraka iwezekanavyo. Lengo la Kamati hii ni kuhakikisha tunashughulikia vikwazo visivyo vya kibiashara. Natoa wito kwa Watanzania waitumie Kamati hii, kwa sababu ukikumbana na matatizo ya vikwazo visivyo vya kodi, ukakaa kimya basi na sisi hatuwezi kujua umekumbwa na tatizo gani, lakini ukilifikisha pale Wizarani kwenye Kamati hii, Kamati hii inaweza ikalifanyia kazi kwa haraka na tunaweza tukapata ufumbuzi kwa haraka, kama ambavyo wengine waliotumia fursa hii walivyoweza kunufaika kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, alitoa hoja na hoja mojawapo alisema kwamba, katika Tanzania kule kwenye eneo lake kuna baadhi ya ndugu zetu wa Afrika Mashariki, ambao wanafanya kazi katika mahoteli na kazi hizo anavyoona yeye, zingeweza kufanywa na Watanzania. Napenda kusema kwamba, kuwepo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hakumaanishi hata kidogo kwamba, sasa mambo yanaendeshwa kiholela na bila kufuata taratibu.

Nirejee tu juzi juzi hapa, Naibu Waziri wa Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana alijibu hapa Bungeni kwa niaba ya Serikali na akasema kwamba, Wizara ya Kazi imeanzisha upya Kamati itakayosimamia utaratibu wa kutoa vibali vya kazi na Kamati hiyo kwa nia nzuri tu imeweka wawakilishi mbalimbali kutoka *TIC*, Chama cha Waajiri, Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi na Wawakilishi kutoka Idara ya Vijana. Lengo la Kamati hii ni kwamba, vibali viende kwa wale watu ambao kwa kweli ndani ya Tanzania,hatuna watu wenye kufanya kazi hizo na Kamati hiyo itafanya kazi kubwa zaidi ya hiyo. Kamati itapitia maeneo yote kujiridhisha kama kweli wale ambao wanafanya kazi katika maeneo mbalimbali, wanastahili kufanya kazi hizo. Ikigundua kuwa hawastahili, watachukuliwa hatua na hata kama walipata vibali kwa bahati mbaya basi

watanyang'anywa vibali hivyo. Nimwombe Mheshimiwa Dr. Slaa aote ushirikiano kwa Kamati hiyo lakini na Waajiri tuwaombe Waajiri watoe ushirikiano kwa Kamati hiyo, kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha zile ajira ambazo ni za Watanzania basi zifanywe na watanzania na ajira chache tu ambazo tukithibitisha kwamba ni kweli hatuna watu wenye uwezo wenye kuzifanya kazi hizo ndiyo basi tutoe vibali kwa ajili ya kazi zote.

Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, pia alitoa hoja kwamba, vitunguu vya maeneo yake kule na mengine, vingi vinauzwa Kenya. Nasema kama hawa wakulima wasingekuwa na soko hilo la Kenya, wewe kama Mheshimiwa Mbunge, tatizo la kwanza ambalo ungekuwa nalo wangekwambia Mheshimiwa tunazalisha hapa vitunguu vyetu, vinaoza na havina soko lolote lile. Lakini sasa kumbe tatizo lililopo si hilo, tatizo lililopo ni kwamba, vinanunuliwa na Wakenya kwa bei ndogo. Kwa maneno mengine, soko lililopo si zuri kama ambavyo tungetafuta soko lingine zaidi na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa amesema kwamba, watu wao wakishapeleka vitunguu Kenya, basi wanaviuza nje ya Kenya. Kwa maneno mengine ni kwamba, kuna soko kubwa zaidi ya Kenya; swali la kujiuliza je, Watanzania hatuna uwezo wa kuthubutu kuweza kwenda kwenye soko lingine zaidi ya Kenya? Je, jambo la kufanya hapa ni kukaa na kulalamika tu kwamba, Wakenya wanachukua vitunguu vyetu ama tuzinduke na tuchukue hatua za makusudi?

Ndiyo maana nasema kwamba, tuzinduke na tuchukue hatua za makusudi na ndiyo maana Serikali kupitia Wizara mbalimbali, imekuwa ikitoa fursa mbalimbali za kuwezesha wajasiliamali waweze kufanya hivyo. Tunayo mipango mbalimbali ya kuweza kudhamini watu ambao wako tayari kutafuta masoko nje ya nchi. Fursa hizi zipo, natoa wito kwa Watanzania wazitumie badala ya kukaa chini na kulalamika kwamba, hili linatokea. Lakini vilevile niseme pale Morogoro kuna Bwana mmoja ameanzisha kiwanda cha kusindika machungwa nilipotembelea, kiwanda kile aliniambia jambo moja likanishangaza kwamba, kuna wataalam fulani walikuja pale kutoka nchi moja, wakamwomba kwamba wangependa wakinunue kiwanda kile, kwa sababu kile kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuchukua matunda mengi. Wakamwambia tungeomba hiki kiwanda tukinunue, lakini huyu bwana akasema nilikataa. Nilikataa kwa sababu nataka kuwawezesha Watanzania kupata ajira, nilikataa kwa sababu natekeleza sera sahihi za Chama cha Mapinduzi za kuwezesha viwanda vya kuongeza *value* kwenye mazao yetu tunayozalisha. Akasema ndiyo maana alikataa na mimi nikamshukuru nikasema sasa kama na *private sector* wameanza kuelewa na kutekeleza sera zetu za Chama cha Mapinzuri, hilo ni jambo bora na huo ndio mwelekeo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Siraju Juma Kaboyonga, ametoa hoja nzuri na nyingi tu, lakini akasema angependa ajue kama tumeshafanya tathmini ya Umoja wa Forodha wa pamoja. Niseme ni kwamba, hadi sasa Umoja wa Forodha tangu uanze ziko changamoto, lakini yapo mafanikio. Kwa mfano, kabla umoja wa forodha haujaanza, yalikuwepo mawazo kwamba, tukianzisha Umoja wa Forodha mapato yanayotokana na ushuru wa forodha, yataporomoka. Lakini ushahidi uliopo unaonesha mwaka hadi mwaka, mapato yanayotokana na ushuru wa forodha badala ya kuporomoka yanaongezeka.

Lakini vilevile wako watu waliokuwa wanafikiri kwamba, Tanzania hatutakuwa na chochote ndani ya Soko la Afrika Mashariki. Nilipofanya ziara kwenye mipaka mbalimbali ya nchi hii, nilichogundua na nilichoona ni kwamba, ziko bidhaa zenye ubora zinazotoka Tanzania kwenda nchi jirani. Nikiwa pale Namanga, nilishuhudia magari yakiwa yamebeba makontena yaliyo na transfoma zikipelekwa Kenya na Uganda. Niwakauliza kwa nini wanauza; wakasema wameweza kuuza kwa sababu ya kuwepo kwa soko ndani ya Afrika Mashariki na kuondoa baadhi ya ukiritimba. Nilipowaulizia wenye kiwanda kile, wakasema sasa wana *order* nyingi kuliko uwezo wa kuzalisha na kwa kweli sasa wanafikiria kupanua kiwanda kile ili kuweza kutosheleza soko la Afrika Mashariki.

Lakini juzi nilipokuwa natembelea Maonesho ya Sabasaba pale nilitembelea kibanda cha *Tanzania Tea Blenders,* wakaniambia kwa kweli wameanzisha kitu kinachoitwa *three in one.* Wanachukua sukari wanachanganya na maziwa, pamoja kahawa, wakasema wamepata soko zuri la ile *product* ya *three in one* Mombasa kuliko ambavyo wamepata soko hilo Tanzania. Kwa hiyo, wakasema wao *Tanzania Tea Blenders* wanamshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuwepo Ushuru wa Forodha wa pamoja na wana soko la uhakika Mombasa.

Lakini vilevile nilipotembelea maeneo mengine, nikakuta hata maji kutoka viwandani yanaenda kule Kenya, nikauliza kwa nini? Wakasema maji yetu ni mazuri kuliko maji ya wenzetu. Siku za nyuma, sabuni zilizotengenezwa kwenye viwanda vya Tanzania, zilikuwa zinachukuliwa kama zenye ubora kidogo, hata dawa za meno zilikuwa zinaonekana zina ubora, lakini hivi sasa wote ni mashahadi, sipendi kutaja hapa viwanda isije ikaonekana kwamba, labda napigia debe bidhaa za kiwanda fulani.

Jibu ni kwamba, viwanda vyetu vimeanza kuongeza ubora wa bidhaa zake na sasa vimeanza kuuza ndani ya Soko la Afrika Mashariki. Kwa kweli leo hii nikienda London, nikifuatana na Naibu Waziri kutoka Uganda na Kenya, tukikutana na wafanyabiashara, akiulizwa Naibu Waziri wa Kenya anauza nini Tanzania, yule atasema analeta chumvi na *sausage* Tanzania. Lakini mimi nitasema Tanzania tunauza *transfoma* Kenya. Wale wafanyabiashara wataniona mimi nimeukata zaidi kuliko yule anayetuletea *sausage.* Niseme tu hata hizo *sausage* wamekuwa wakituletea, kwa sababu viwanda vyetu vilikuwa vimeyumba hapa kati kati. Hivi sasa kwa nia nzuri tu, tumeanza kufufua viwanda vyetu vya kuongeza ubora wa nyama na muda si mrefu, mtaona *sausage* zitaanza kwennda Kenya badala ya kutoka Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiangalia mauzo yetu ya biashara nje, mwaka 2000 tuliuza Kenya bidhaa zenye thamani ya dola milioni 40.7, mwaka 2006 tumeuza bidhaa Kenya na Uganda zenye thamani ya dola milioni 117, ambayo ni sawa sawa na ongezeko la asilimia 189. Lakini vilevile na tulichonunua kutoka Kenya kimeongezeka kwa asilimia 77. Kwa hiyo, sisi kasi yetu ya kukua kwa uchumi na kasi yetu ya kuuza nje, kuna ongezeko zaidi kuliko sisi kasi yetu ya kununua kwao inavyoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme jambo moja ambalo ni la msingi, kununua vitu kutoka kwa mwenzako si jambo baya. Leo hii ukienda Mkoa wa Kagera,

ukiwauliza wananchi faida ya Afrika Mashariki, watashukuru kwa sababu tulikuwa tunanunua saruji kwa bei kubwa, kwa sababu saruji ilikuwa haitoki Uganda sasa inatoka Uganda. Ukiangalia saruji ya Tanzania na Uganda bei zinatofautiana. Ukimuuliza muuza mabati, atasema sasa mabati yanapatikana kwa bei nzuri zaidi kutoka Uganda na changamoto hii tunawaambia wenye viwanda waliokuwa wanafikiri kwamba Arusha ni pembezoni mwa Tanzania. Waliokuwa wanafikiri kwamba, Kagera ni pembezoni, waanze kufikiria kupeleka viwanda Kanda ya Ziwa na maeneo mengine yaliyokuwa yanafikiriwa kuwa ni pembezoni, si pembezoni tena. Kwa sababu kibiashara mipaka ya Tanzania sasa imepanuka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende haraka kengere ya kwanza imegongwa. Namshukuru Mheshimiwa Pindi H. Chana, kwa mchango wake alioutoa pamoja na Mheshimiwa Juma H. Killimbah, walielezea hoja nyingi tu. Ninaishukuru Wizara hii masuala yake, kazi yetu kubwa ni uratibu na kimsingi Serikali ni moja, mambo yote yaliyo ndani ya Serikali tunachofanya ni kugawana majukumu tu kwamba, nani anafanya nini kwa wakati fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kumjibu Mheshimiwa Mohamed G. Dewji, alitoa hoja nzito. Alisema *crude palm oil*, Tanzania tunatoza asilimia 10, Kenya na Uganda wanatoza asilimia 0, 0. Tunasema ndio, hiyo ni sawa, lakini tunafanya hivyo kwa sababu ya kulinda wazalishaji wetu wa ndani wa mafuta ya alizeti, mafuta ya pamba na wengine, kwa sababu tuligundua hii waliyokuwa wanaiita *crude oil,* si *crude oil*. Sasa ukiruhusu *crude oil* iingie Tanzania, ukaiita *crude oil,* maana yake unaua wakulima wako wa ndani na kuwaneemesha wakulima wa mawese wa Malaysia. Tunasema Kigoma tuna ardhi kubwa na Tanzania ina ardhi kubwa, kama kuna mtu anataka, basi awekeze kwenye kilimo cha mawese Kigoma au awekeze kwenye kilimo kingine kuliko kuendelea kuagiza *palm oil* kutoka nje. Lakini Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea kulitafiti hili. Nimwombe Mheshimiwa Mohamed G. Dewji, awe na subira mpaka hapo utafiti utakapokuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mheshimiwa alisema sabuni *crude palm* ni aslimia 10. Hapo nyuma ilikuwa ni aslimia 25, lakini hivi viwanda vinavyozalisha sabuni vinavyoitwa stand *alone, raw material* ya kwao inaitwa *sterring*. Sasa tukasema kama kweli ni *raw materials* na wakathibitisha, tukashusha kutoka asilimia 25 mpaka aslimia 20 ili viwanda vyao visiondoke kwenye soko, na kwa Kenya ni hiyo hiyo na kwa Uganda ni hiyo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niende haraka haraka, alitoa hoja kwenye mchele kwamba, kwa nini Tanzania ina asilimia 75. Ni asilimia 75, kwa sababu ndani ya nchi tuna watu wenye uwezo wa kujituma, wenye uwezo wa kuzalisha mchele kwa wingi, tukiruhusu mchele uingie tu, maana yake hawa wakulima wetu tutakuwa tumewanyonga kiuchumi. Ndio maana ni aslimia 75. Tumefanya hivyo si kwa bahati mbaya, siyo kwa kushangaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Kenya walituomba kwenye Jumuiya kwamba, wao wana Mkataba na Pakistan kwamba, Pakistan inanunua chai yao, sasa kama

wangeacha kununua mchele wa Pakistan, wangeweza kupata tabu. Tumewapa muda mpaka 2008, waendelee kuingiza mchele kwa asilimia 25, baada ya hapo itabidi warudi kwenye 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mbunge, aliulizia ngano, alisema mbona Tanzania ni asilimia 10 na Kenya ni aslimia 75? Kenya ni asilimia 75 kwa sababu wanazalisha sana ngano kuliko sisi na hapa Tanzania, tunazalisha lakini kidogo, lakini hii ngano inatumiwa na watu wengi kwa ajili ya chapati na vitu vingine. Tukaona tukiifanya hii asilimia ikawa kubwa, tutafanya maisha ya wananchi yasiwe bora bila sababu ya msingi. Ndio maana tukaweka asilimia 10 na tutaendelea kuitizama hii na kupima hali ya maisha inaendaje kwa wananchi. Tukiona bado ni mzigo, tunaweza tukaishusha kwa nia ya kufanya maisha bora kwa kila Mtanzania, yaendelee kuwa bora. Lakini tutafanya hivyo tu kama tuna uhakika, ndani ya nchi hatuna ngano tunayozalisha kwa wingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, kwa michango yake kuhusu Kiswahili na ndio maana tuna nia kwamba, hapa Tanzania iwe Makao Makuu ya Baraza la Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, alisema je, ikifika 2010 tumejiandaa vipi kama tutakuwa hatujakaa sawa kuhusu viwanda vyetu? Ikifika 2010 ni kwamba, tulisema kodi kwa bidhaa kutoka Kenya zinapungua taratibu, ikifika 2010 itakuwa sifuri.

Lakini vile vile katika Itifaki inayoanzisha Umoja wa Forodha inasema, tutazingatia ile *Principle* inayoitwa *Arthmetry* kwamba, kama kuna jambo lolote la kiuchumi linaonesha kuleta madhara ya kiuchumi kwa nchi fulani, hatuwezi kuruhusu likaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ikifika 2010 tutafanya tathmini na mwaka huu kimsingi tutafanya tathmini kama nchi, ukiacha ile ya Jumuiya Mashariki kuangalia tunaenda namna gain, kwa nia ya kuwakumbusha wenzetu wale ambao hawajajiandaa, waendelee kujiandaa kuangalia ni wapi tuongeze nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa uchangiaji wako huo mzuri sana, uliosababisha Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kuniandikia barua kwamba sasa anaunga mkono Ushirikiano wa Afrika Mashariki. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba niungane nawe, kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa mchango wake mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza, niwatambue waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni nao ni wafuatao: Mheshimiwa Teddy L. Kasela-Bantu, kwa niaba ya Kamati ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Dr. Wilbroad P. Slaa, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Mohammed Juma Habib Mnyaa, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi na Mheshimiwa Dr. Diodorus B. Kamala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo pia waliochangia kwa maandishi ambao ni Mheshimiwa Mohammed G. Dewji, Mheshimiwa Juma H. Killimbah, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro, Mheshimwa Zaynab M. Vulu, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya, Mheshimiwa Col. Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Fatuma Abdulhabib Fereji, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Ame Pandu Ame, Mheshimwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Severina S. Mwijage, Mheshimiwa Profesa Philemon M. Sarungi na Mheshimiwa Paul P. Kimiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nikubali kwamba, leo mjadala katika Bunge hili juu ya hoja ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ulikuwa mzuri sana na wa kiwango cha juu sana kutoka pande zote mbili za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme kwamba, kwa upande wa Kamati ya Mambo ya Nje, nakubaliana kabisa na maoni ya Kamati na Wizara yangu itachukua maoni haya na kuyafanyia kazi kikamilifu. Yapo mengi kama ambavyo yamesomwa na Waheshimiwa Wabunge, wanayo nakala ile juu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili tuweze kuboresha miundombinu sisi wenyewe, kuandaa elimu na kadhalika. Haya yote yaliyozungumzwa katika Kamati na ushauri wake kwa Wizara yetu, tutayachukua na tutayafanyia kazi. Labda niseme tu kwamba, kuhusu suala la kufundisha Kiswahili, tayari Serikali imeshapokea maombi kutoka Uganda na Burundi, kuwapelekea walimu na Waheshimiwa Mawaziri, wanaohusika humu ndani, wanafahamu suala hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, palitolewa hoja kadhaa na Kambi ya Upinzani kupitia kwa Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani. Niseme tu kwamba, kimsingi mimi nakubaliana na Msemaji Mkuu wa Upinzani, juu ya changamoto zinazotukabili katika kuboresha zaidi ushirikiano wetu na kuboresha zaidi maslahi ya Tanzania. Kwa mfano, kuboresha elimu, miundombinu, kupata vitambulisho na kufuatilia kero za wafanyabiashara, kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri, amezifafanua. Haya mimi nakubaliana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lazima niseme kwamba, siwezi kukubaliana na ndugu yangu, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kuhusu Mambo ya Nje, kwenye masuala haya yafuatayo:  Kwanza, sikubaliani na Msemaji Mkuu wa Upinzani kuwa, nchi yetu haikusoma funzo la Jumuiya iliyovunjika.

Akasema pia kwamba, kuingia kwa Rwanda na Burundi, yeye anaona kwamba ni matatizo.  Tatu, Tanzania haijafaidi chochote na Jumuiya, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri sasa hivi ametoka kuzungumzia faida ambazo nchi hii tayari imeshazipata. Pia akazungumzia kwamba, tutatue matatizo yetu sisi wenyewe kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii imejifunza sana kutokana na kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika, iliyovunjika mwaka 1977.  Ndio maana basi, Jumuiya ya sasa ya Afrika Mashariki, Waingereza wanaema: *"People centred,"* ni Jumuiya iliyoundwa kwa muono wa kwamba, iwe ni Jumuiya ya Watu *(People Centred)*.  Pili, ndio maana basi tumeepuka kukimbilia kuwa na miradi kama iliyokuwa katika Afrika Mashariki iliyokuwa awali, kwa mfano, kuwa na *Common Services* kama vile Ndege, Reli, Bandari na kadhalika. Tumekwenda kwa tahadhari sana kwenye sekta hiyo.  Tatu, ndio maana tumeanzisha *Customs Union,* inayozingatia tofauti ya maendeleo kati ya nchi zetu.  Nne, ndio maana hata katika majadiliano yajayo juu ya Soko la Pamoja *(Common Market),* tutahakikisha kwamba, tunakwenda katika majadilino hayo kwa uangalifu mkubwa, tukitilia maanani maoni na maslahi ya Watanzania juu ya ajira zao, juu ya ardhi yao na juu ya rasilimali ya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kitendo cha kukusanya maoni ambacho Serikali ilikiidhinisha hapa na kuunda Kamati Maalum, pekee ni ishara kwamba, Serikali hii inajali watu wake na inazingatia ushiriki wa watu wake na maslahi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni suala la ufinyu wa bajeti, ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kadhaa.  Nitatumia mtindo wa mada kueleza mambo yaliyozungumzwa badala ya kwenda jina hadi jina, kwa ajili ya kuogopa kurudia na pia suala la muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ufinyu wa bajeti, limezungumzwa pia na Kamati ya Mambo ya Nje, Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine. Mimi niseme kwamba, bajeti tuliyotaka mwaka huu inatosha kwa kazi tuliyonayo mwaka huu wa 2007/2008.  Wizara hii ndio imeanzishwa, kuna suala la uwezo wa kuweza kutumia kinachopangwa na pia kazi ya Wizara kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ni kuratibu utekelezaji ulioko katika Sekta au ulioko katika Wizara za Kisekta.  Kwa mfano, mambo ya miundombinu, yako kwenye Wizara ya Miundombinu, mambo ya viwanda na biashara yako Wizara ya Viwanda na Biashara na kadhalika.  Lakini nataka niseme kwamba, kwa kweli kazi hizi za uratibu, tutaweza kuzifanya katika mwaka huu wa fedha. Kadri Wizara itakavyoimarika, mimi ninaamini kabisa na kulingana na vipaumbele ambavyo Serikali inatoa, basi ninaamini kabisa bajeti ya Wizara hii, itakuwa inaongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lililozungumzwa ni ushiriki wa wananchi katika hatua za mtangamano *(Integration Process)*. Suala huili limegusiwa sana na ndugu zetu wa Kambi ya Upinzani. Mfumo tulionao sisi hapa ni wa uwakilishi, ndio maana tuna Bunge, yaani demokrasia yetu siyo ile ya moja kwa moja, kama ilivyokuwa enzi za kale. Tunayo demokrasia tunayoiita demokrasia ya uwakilishi *(Representative Democracy)*. Tunachozungumzia sasa kwa kweli si suala la Shirikisho, kama ambavyo wenzetu wameliweka kwamba, hatua hii ya Shirikisho imefikiwa au tunakwenda nayo bila ya kushirikisha wananchi. Tunachozungumzia sasa ni suala la Jumuiya kama ilivyo hivi sasa na hatua yake ya kwanza hii ya *Customs Union,* ambayo tayari tumeshaingia. Hatua ya Shirikisho ikifikiwa, kwa vyovyote vile patakuwa na kura ya maoni kama tunataka au hatutaki.

Hatua hii ya Shirikisho itakapofikiwa ni muhimu kuliko zote, kwa sababu itahusu kufuta utaifa wa Taifa moja moja na kuunda Taifa jipya. Kwa hiyo, haiwezekani kutegemea kwamba, Serikali inaweza kwenda kama wengine walivyosema hapa kwamba, tusijipeleke kichwa kichwa tu, Serikali ikaingia kwenye masuala ya Shirikisho bila ya kuwa na uhakika kwamba suala hili limezingatia maoni ya wananchi wake na limezingatia maslahi ya wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetolewa mfano wa Wimbo wa Afrika Mashariki, kama mfano wa namna Serikali inavyojipeleka kutokushirikisha wananchi na sijui wimbo huu umepatikana namna gain, mpaka umefananishwa kama ni wimbo wa Shirikisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu wimbo siyo wimbo wa Shirikisho ni wimbo wa Jumuiya kama ulivyo hivi sasa, siyo wimbo wa Shirikisho, hilo la kwanza. Lakini la pili, mchakato wa kupata wimbo huu, ulishirikisha taasisi na watu mbali mbali. Hapo nchini kwetu paliundwa Kamati, paliundwa na kikundi kilichoshiriki. Mheshimiwa Mwenyekiti, humu Bungeni mwetu yuko mtaalam wa mambo haya Mheshimiwa John Komba ambaye ameshiriki katika Kamati hii ya kushughulika na wimbo wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima nimeseme kwamba, wimbo huu kwanza bado wala haujapitishwa. Wimbo huu unasubiri michango ya Rwanda na Burundi na baadaye mchakato utapitiwa upya, kuufikisha mbele ya kikao cha Wakuu kuona kwamba ni wimbo gani unafaa kwa ajili ya Jumuiya kama ilivyo na siyo kwa ajili ya Jumuiya kama Shirikisho la kisiasa. Kwa hiyo, naomba tutenganishe haya ili wananchi wetu wasipate taarifa ambazo siyo sahihi sana. Hakuna wimbo wa Shirikisho ambao nchi yetu imeuidhinisha. Wimbo uliopo hapa sasa hivi ni wimbo wa Jumuiya kama ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kubwa ambalo limezungumzwa hapa ni sualala *EPA* ya Afrika Mashariki. Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia. Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Mbarouk K. Mwandoro na wengine wengi ambao wamelizungumzia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe ufafanuzi ufuatao: Kwanza, *EPA* siyo Kanda ya Kiuchumi kama vile *East African Community, COMESA* na *SADC,* ingawa

inaweza kuwa inahusiana. Pili, uhusiano wa *EPA* na Kanda za Kiuchumi ni pale inapotakiwa Kanda ya *EPA* iwe na *Common External Tariff* yake yenyewe na pia *Development Fund* inayotarajiwa kupatikana kutolewa kwa kujenga Kanda ya Kiuchumi. Moja ya madhumuni ya *EPA* ni kuhakikisha kwamba, wanaimarisha Mtangamano *(Integration Process)*. Tatu, mkiwa na *Customs Union* kama ambavyo *Community* yetu inayo na *SACU* kule Kusini mwa Afrika wanayo, ndiyo inakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kufanikisha kuwa na *EPA,* ambayo inazingatia masuala ya biashara na pia *EPA* ambayo inazingatia masuala ya msaada wa fedha za maendeleo. Nne, Tanzania haikusababisha *East African Community* isiwe na *EPA* yake. Hili suala ni lazima tulielewe, Tanzania siyo iliyosabisha, kama ambavyo ilisemwa hapo awali, ni kwamba suala hili lilikubaliwa na viongozi wa nchi za Afrika Mashariki, halafu baadaye wenzetu wakaenda kwenye *ESA* na sisi Tanzania tukalazimika kwenda kwenye *SADC – EPA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nieleze kwamba, Mkutano wa Kilele wa Kampala miezi michache iliyopita hapa, uliamua kwamba, suala la *EPA* litazamwe upya na Wakuu hawa waliamua kwamba, mkutano wa pamoja uitishwe baina ya Mawaziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Mawaziri wa Biashara ili kulipitia upya suala hili na kuweka msimamo wa pamoja, kwa madhumuni kwamba, ikiwezekana tuwe na *EPA* moja ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mkutano huu wa pamoja wa Mawaziri utafanyika tarehe 16 Agosti, 2007, Mjini Arusha. Kikao kijacho cha Wakuu wa nchi kinatarajiwa kufanyika tarehe 20 Agosti, 2007, Mjini Arusha. Moja ya mambo ambayo kikao kile kitashughulikia ni kutoa uamuzi juu ya suala hili la *EPA*. Kwa hiyo, nadhani tuvute subira ili suala hili lishughulikiwe kikamilifu. Napenda nimalizie suala hili la *EPA* kwa kusema yafuatayo: Kwamba, maslahi ya Tanzania na Serikali yetu inaamini hivyo kwamba, maslahi ya Tanzania yatahifadhika zaidi, yatakuwa mazuri zaidi kama patakuwa na *EPA* ya Afrika Mashariki, hatuna kigugumizi na hilo. Itasaidia kulinda mafanikio yaliyopatikana katika *Customs Union*, huo ndio msimamo wetu. Lakini kama nilivyosema, suala hili linafanyiwa kazi na tutakwenda nalo mpaka tuone na wenzetu nao mwafaka gani utafikiwa na Wakuu wa nchi watatoa uamuzi wa aina gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa pia hapa suala la kujiunga kwa Rwanda na Burundi katika *Community* kama ni tatizo. Baadhi yao wamezungumza kama ni tatizo na wengine wamezungumza kama ni jambo jema. Mimi napenda niungane na wale wanaosema kwamba, kujiunga kwa Rwanda na Burundi ni jambo jema. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. Sisi katika nchi hizi tano sasa tutakuwa na idadi ya watu wasiopungua milioni 115, maana yake ni soko kubwa na nguvu kubwa ndani ya nchi zetu na nje ya nchi zetu. Halafu hii ndio sera yetu ya mambo ya nje kwa miaka mingi. Siku zote Tanzania tumekuwa tukipigania umoja wa nchi zetu za Afrika na inapotokea fursa kama hii, nadhani ni muhimu tukaona kwamba ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubali kwamba, nchi hizi zimetokana au zimekuwa na matatizo ya ndani kwa muda mrefu, lakini nazo pia zimepiga hatua. Kwa hatua zilizofikia sasa hivi, zimepiga hatua ya kujirekebisha ndani na ndio maana nchi hizi

zimeingizwa katika Jumuiya sasa. Waliomba huko kabla, lakini kwa sababu mwanzo hawakuweza kutimiza vigezo ambavyo tumeviweka katika jedwali la hotuba tuliyoitoa hapa Bungeni, wakaambiwa wasubiri mpaka wafikie hatua lau kama ya kuwa na uchaguzi wa kuchaguana wao wenyewe na kuweka Serikali zilizochaguliwa. Sasa nadhani ni muhimu kwamba, wanapofikia hatua ile na sisi sasa tuungane nao, tuwasaidie katika kuhakikisha kwamba, kanda yetu hii inakuwa na utulivu, amani na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuchagua nchi jirani, nchi hizi zipo kilichopo ni namna ya kuishi nao. Mheshimiwa Dr. Chegeni R. Masunga, wakati anazungumza hapa mchana alikuwa anazungumzia suala la *Amani Forum* na jitihada zao za kusuluhisha migogoro. Kama yeye anavyofahamu na Waheshimiwa Wabunge mnavyofahamu humu ndani kwamba, katika masuala ya menejimenti ya migogoro, masuala ya usuluhishi, kuna jambo ambalo ni muhimu sana linaitwa Upanuaji wa Wigo wa Kutegemeana. Ukiliweka katika Kiingereza hili linaitwa *(Widenning the Area of Interdependence),* yaani unapanua wigo, mnaingiliana *through constructive engagement,* kiasi ambacho kupitia maingiliano ya miundombinu ya biashara na kadhalika, amani inajengeka na ndivyo hata nchi za wenzetu kama vile *Europian Union*, hizi ndizo nchi ambazo karne zilizopita ndiyo vita vyote vimetokea kwao. Kutokana na mwingiliano ule, zimekuwa katika hali ambayo si rahisi sasa nchi moja kuanza vita na nyingine au si rahisi nchi moja kuwa na mgogoro wa ndani bila kupata msaada wa utatuzi na nchi nyingine. Kwa hiyo, nadhani hili ndio jambo ambalo mimi nimeliona na Serikali yetu inaliona kwamba ni muhimu, badala ya kuwaacha hawa waendelee kama walivyo, tukahusiana nao, tukashirikiana nao. Napenda niseme kwamba, ule Mkataba wa kujiunga na Jumuiya una vipengele vinavyozingatia na kusisitiza Utawala Bora, Amani, Demokrasia na Utawala wa Sheria. Kama nilivyosema mwanzo, ndio maana kwa kupitia vigezo hivi, nchi hizi zimeweza kuchukuliwa na kujiunga na Jumuiya hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa suala la Bunge la Afrika Mashariki. Nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba, kuna haja ya kuimarisha Bunge la Afrika Mashariki, kuna haja ya kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kutoa taarifa mara kwa mara Bungeni na kadhalika. Hili halina tatizo. Limezungumzwa lingine juu ya sheria zile, kwamba, je, namna gani sheria zinazotungwa Arusha kwenye Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki, zinatumika? Utaratibu uliopo ni kwamba, sheria zikishatungwa pale, zinapelekwa kwa Wakuu wa Nchi na wakishazitia saini, sheria hizo zinatumika, ndio utaratibu ulioko. Kama sheria haijaanza kutumika, inakuwa kwamba kanuni zake hazijaundwa na taratibu zake nyingine hazijawekwa bayana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nataka nije kwenye jambo moja ambalo limezungumzwa sana hapa na ambalo ni zito. Waheshimiwa Wabunge, wameulizia hatma gani itakuwa baada ya wananchi kusema asilimia 75.9 kwamba wao hawataki Shirikisho liharakishwe, itakuwaje? Nataka nirejee maneno ya Mheshimiwa Rais, wakati anapokea taarifa ya Kamati ya kukusanya maoni ya Profesa Chacha Z. Wangwe. Alisema, Serikali itaifanyia kazi taarifa ile na Serikali itazingatia maoni ya wananchi. Lakini zaidi ya hapo, nataka niseme jambo moja kwamba, hapa pamejengeka

hofu kama vile patatokea hali ambayo kwa njia moja au nyingine, tutashinikizwa kuchukua uamuzi bila ya ridhaa yetu. Nataka nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Tanzania haitashinikizwa na yeyote yule, ama kuingia katika Shirikisho au kuchukua hatua yoyote, ambayo haina maslahi na nchi yetu. Huo ndio msimamo wetu na wenzetu wanaokwenda kwenye majadiliano juu ya Jumuiya, wanajua msimamo huo na wanapata maelekezo wakati hadi wakati. Waheshimiwa Wabunge, hakuna haja ya kuwa na hofu, ipo Serikali makini inayojua inachofanya na tutahakikisha kwamba, maslahi ya wananchi hawa yanalindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, nataka nimalizie kwa kuongeza tu kwamba, hata katika uamuzi unaofanywa katika Jumuiya, uamuzi pale siyo wa kupiga kura, uamuzi pale ni wa maridhiano ya wote *(Consensus)*, sijui Mheshimiwa Mohamed Seif Khatibu, mtaalam wa Kiswahili *Consensus* ataiitaje? Hakuna njia ya kulazimisha kuchukua jambo au kufanya uamuzi ambao wewe mwenyewe hujautaka. Nimeona niliseme hili kama kufunga kufuli tu kwa yale ambayo nimeanza kuyasema kwamba, ndugu zangu hakuna uwezekano wa sisi kushinikizwa kufanya mambo ambayo hatuna maslahi nayo na hatuwezi kuyakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda nimalizie na jambo ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri alililisema kidogo, alilolizungumza Mheshimiwa Pindi H. Chana, juu ya uwezo au nafasi ya Wizara kushauri na kadhalika. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, mambo mengi haya ni mambo ya kisekta na pia katika Mfumo mzima wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kuna Mabaraza ya Kisekta *(Sectoral Councils),* ambayo yanashirikisha Wizara husika na masuala yale na maamuzi yakishafanywa, baadaye ndio yanaletwa kwenye Baraza la Mawaziri la Afrika Mashariki na kupitia Baraza la Mawaziri wa Afrika Mashariki, mambo hayo yanapelekwa kwenye mkutunao wa kilele *(Summit)* au kwenye mkutano wa Viongozi Wakuu wa nchi zetu.

Baada ya kusema haya, napenda nikiri kwamba, hoja zilizotolewa hapa ni nyingi na hasa za maandishi. Wizara yangu itazipitia zote na tutazijibu zote, tutazileta kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi huu wa masuala yale ambayo niliona yalihitaji majibu ya hapa hapa sasa hivi, naomba Waheshimiwa Wabunge, wakubali kupitisha Makadirio ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki ili tuweze kuendelea na kazi ya uratibu katika kulinda na kujenga maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iIiamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 97 – Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kitabu tutakachoshughulika nacho ni kimoja tu ambacho ni *Volume II,* Fungu 97, kuhusiana na Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Lakini kabla sijamruhusu Katibu kuendelea, niwakumbushe tu Waheshimiwa Wabunge, taratibu ambazo zimewekwa na Kanuni zetu na ambazo zimekuwa zikisisitizwa sana na Mheshimiwa Spika, kuhusiana na majadiliano katika hatua hii ambapo Kanuni ya 81 ndiyo inayoongoza suala zima ni kuomba ufafanuzi ama maelezo zaidi. Baada ya utangulizi huo, sasa namwomba Katibu tuendelee.

Kif. 1001 – *Administration and General*…...………..Sh. 1,402,139,400

**MHE. MOHAMED G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 97, Program 10, Suvote 1001, Item 250100* - Mshahara wa Waziri. Nilichangia kwa maandishi, napenda kupata ufafanuzi juu ya swali langu.

Swali langu la msingi lilikuwa *External Harmonization of Tariffs* kati ya nchi hizi tatu. Ilikuwa siyo kwamba, kwa nini *edible oil* ina asilimia 10 na siyo *zero*, *rather* ilikuwa kwamba tulikubaliana miaka mitano iliyopita kwamba, tuwe na *External Harmonized Tariffs*, tuwe na *Tariffs* sawa sawa kwa nchi tatu za nje. Asante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu kwamba ni kweli kwenye *Customs Union,* kuna kitu kinachoitwa *common external tariffs* kwamba, wigo wa kodi za ushuru wa forodha unaofanana kwa bidhaa mbalimbali. Lakini vilevile katika utaratibu huo huo, kila nchi inapewa fursa kulingana na mazingira Fulani, unaweza ukajenga hoja ukapeleka kwenye Jumuiya na ukaruhusiwa kuendelea kwa maslahi ya nchi yako na kwa maslahi ya uchumi wa nchi yako, kama ambavyo nilivyosema tulikubaliana, *common external tariffs on sensitive products* kwa mfano ni asilimia 75, lakini katika hili Kenya walituomba tukawaruhusu wa-*import* mchele kutoka Pakistani kwa asilimia 25.

Kwa hiyo, tume-*harmonize,* lakini kuna mambo ambayo tunalazimika kukaa na kujadiliana, kuweka *flexibility* kulingana na mahitaji. Kwa mfano, inapotokea njaa, basi huwezi ukasema kwa sababu ulishakubaliana na *common external tariffs,* watu wafe usiingize chakula. Itabidi hoja zijengwe mrekebishe iendelee. *Common external tariffs* ipo lakini siyo Msahafu wala siyo Biblia, inabadilishwa kwa majadiliano kulingana na mahitaji.

**MHE. MOHAMED G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *the good answers,* lakini mimi swali langu ni kwamba, kama *external tariffs* haziko-*harmonized;* hizo hizo *goods* au mchele ambao unaingia Kenya utapitiliza uje Tanzania? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed G. Dewji, ume-*declare interest* au bado?

**MHE. MOHAMED DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sina *interest*.

**MWENYEKITI:** Asante sana.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishakubaliana kwamba, jambo fulani ni hivi unaporuhusiwa kwa mfano, ule unaotoka Pakstani, akithubutu tu kuuleta Tanzania, tunamtoza kodi ya asilimia 75, kwa sababu unakuwa hauna sifa ya uasilia wa bidhaa. Hivyo hivyo kwa bidhaa nyingine tulizowaruhusu Waganda na mambo mengine. Kwa hiyo, tukiruhusu tuna-*monitor,* tunajua ni kitu gani, ukithubutu kuuleta Tanzania tunakutoza kodi kama kawaida.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 97, Program 10, sub-vote 1001,* kifungu kidogo 250100, sina haja na mshahara wa Waziri. Naomba ufafanuzi, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri, akieleza kuhusu kahawa hii ambayo sasa inatengeneza *three in one,* naamini alikuwa anazungumzia kuhusu *Africa Cafee*. Mimi nimeiona kahawa hiyo, kuna maandishi madogo sana *made in Indonesia*. Sasa nilitaka ufafanuzi, hii kahawa kweli tunaitengeneza Tanzania ama tunawapelekea wa-Indonesia watutengenezee halafu irudi hapa na kama hivyo ndivyo tunazuia vipi wa-Indonesia wasiuze kahawa yetu chini ya jina letu, lakini faida wakawa wanapata wao? Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ile niliyosema inatengenezwa Tanzania *three in one* na niseme katika utaratibu wa utengenezaji maana wanatengeneza kahawa wanachanganya na maziwa pamoja na sukari; sukari inapatikana Tanzania na maziwa yanapatikana Tanzania. Tuna kiwanda kizuri kinazalisha kahawa ya Tanika na kilipata heshima ya kwanza duniani, kwa kuzalisha kahawa bora kuliko kiwanda chochote kile Duniani. Kwa hiyo, vyote hivyo vinapatikana hapa Tanzania. Labda niseme tu, isingekuwa busara kwa kuwa sasa inatengenezwa hapa na inakwenda Kenya, inaingia bila matatizo, isingekuwa busara sisi wenyewe ndiyo tuanze kuwa na wasiwasi. Hoja ni kwamba, tunatengeneza na tutaendelea kuamini hivyo mpaka hapo baadaye. *(Makofi)*

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali nililouliza ni dogo tu, ipo *Africa Cafee, three in one* ya maziwa, sukari imeandikwa *Tanzania Tea Blenders* lakini kuna maandishi madogo sana *made in Indonesia,* sasa anazungumzia *bland* ipi?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia inayotengenezwa Tanzania lakini kwa kuwa Mheshimiwa ameleta hoja hiyo, basi tutachunguza zaidi tuone kama kuna tofauti na tunavyoelewa sisi ili kama kuna ulazima wa kuchukua hatua, basi tuweze kufanya hivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunatumaini vilevile Wizara ya Viwanda na Biashara, watasaidia katika hilo.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 97, Program* ya 10, *sub-vote* 1001 na *item* 250100. Nilitaka ufafanuzi kutoka kwa

Mheshimiwa Waziri, Tanzania ina ratibu vipi sekta binafsi katika Soko la Afrika Mashariki ili kuondoa matatizo yaliyopo, ambayo ni mengi hivi sasa na kuiletea nchi yetu manufaa? Kwa mfano, sasa hivi wafugaji mipakani, wana matatizo la kupeleka ng'ombe wao katika soko katika miradi ya Kenya, lakini Wakenya wanaingia Tanzania na kununua ng'ombe wetu. Hali kadhalika, wakulima kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge kwamba, wananunua machungwa Tanzania lakini Tanzania hawana nafasi ya kupeleka machungwa Kenya. Nilitaka maelezo ya Mheshimiwa Waziri, hizi sekta binafsi zinaratibiwa vipi ili kuondoa hili zogo?

Lakini la pili, baada ya Zanzibar kukataliwa kuingia katika Shirikisho la Afrika Mashariki, pamoja na maelezo yote yanatolewa kwa faida ambazo zingepatikana, lakini pia imekataliwa. Swali langu ni kuwa; hapo Tanzania itakapoingia katika shirikisho litakapokuja, ikiwa baada ya miaka 50 au 100; je, itaingia katika sura ya Muungano au ni katika hali kama tunavyoona sasa hivi ya kubabaisha tu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, swali la pili nitalipenda ulifafanue vizuri zaidi, kabla sijaliruhusu halijaeleweka.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninasema kwamba, Zanzibar iliomba kuingia katika Shirikisho litakapokuja kama nchi, lakini kwa sababu mbalimbali hilo halitowezekana. Sasa ninachosema ni kwamba, hapo litakapokuja Shirikisho, hatujui lini Tanzania itaingia katika Shirikishoi katika sura ya Muungano halisi, yaani kwa Uwakilishi wa Tanzania Bara na Zanzibar au zinapenyezana kama inavyoonekana baadhi ya sekta sasa hivi kwamba, hizi za Muungano lakini Wazanzibari hawamo?

**MWENYEKITI:** Nadhani inabidi Mheshimiwa Waziri, uweke sawa haya mambo.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kufafanua hili la kwanza. La pili kuhusu bidhaa, Mheshimiwa Naibu Waziri, atalitolea ufafanuzi. Mimi nadhani kunakutokuelewa suala hili, Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Mkataba wa Afrika Mashariki, unazungumzia nchi kamili *(Sovereignty)*. Tanzania, Kenya na Uganda zimo kama *Sovereignty*.

Kwa hiyo, hakuna suala la kusema kwamba, kuna suala la Zanzibar imekataliwa kuingia katika Shirikisho, kwanza hatujafika kwenye Shirikisho, ndiyo haya tulikuwa tunazungumza leo hapa, tunazungumzia Jumuiya kama ilivyo.

Shirikisho ndiyo hili yamekusanywa maoni na kuwataka wananchi waseme kama wanataka kuharakishwa au kutokuharakishwa Shirikisho. Tunachozungumzia sasa hivi ni suala la Jumuiya ya Kiuchumi na hatua zile ambazo zimetajwa. Sasa tunachosema kwanza, mkataba kama ulivyo hivi sasa, unazungumzia nchi na ndivyo mambo yalivyo, hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini la pili, kama unazungumzia miaka 50 ijayo, miaka 60, miaka 30 ni muda ambao ni mbali sana hapo. Mimi sidhani kama tunahitaji kulifikiria hilo kwa wakati huu.

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la mifugo kuuzwa, kuna wakati imekuwa ikipelekwa nchi jirani na wafugaji wetu wamekuwa wakipata tabu kweli kweli. Njia wanazopita, maeneo wanayopita na saa nyingine wanakamatwa, wanatozwa adhabu. Lakini sasa tunaboresha masoko yetu, ufumbuzi ni kuwa na masoko yetu sisi wenyewe na yapo masoko mengine yameanza kufanya kazi, lakini kubwa kuliko yote ni kwamba, lazima tuwe na viwanda vyetu sisi wenyewe vya kusindika mifugo. Tukifanikisha hayo, tutaweza kusindika nyama. Tukifanikisha hilo tutaweza kuondokana na tatizo hili la Watanzania kuhangaika na mifugo kusafiri umbali mrefu na kuishia kupata bei ndogo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hakuna haja ya kutaja vifungu, kwa sababu nyote mnaofuata mko kwenye hili hili.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuturahisishia. Wakati ninachangia, nilikuwa nimeongelea suala la wakulima wetu wa Wilaya ya Karatu kule Tarafa ya Ihasi, nilitaja na vijiji nikazungumzia kwamba, utaratibu unaotumika na wenzetu wa nchi jirani ni kununua vitunguu hivyo, kwa kitu wanachokiitwa *net*. Nikaeleza vilevile jinsi walivyoingia, wanakodisha na wananunua mashamba kwa utaratibu usioeleweka. Vilevile nikaeleza kwamba, katika utaratibu ule wa *net* wanawahujumu wananchi, kwa sababu *net* moja inafanana na magunia mawili au zaidi katika ujazo tuliozoea sisi wa magunia na hivyo, mkulima wa Karatu anahujumiwa. Waheshimiwa Wabunge wengine, walieleza vilevile maeneo mengine kuna matatizo ya aina hiyo hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri, katika majibu yake akasema tutachangamke na siyo kulalamika lalamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda Mheshimiwa Waziri, alihakikishie Bunge hili tunapoleta tatizo la wananchi, tunapotoa kauli ya wananchi waliotutuma kwamba, hapa tunahujumiwa, kuna utaratibu usiofuata sheria, kuna uhujumu uchumi wa nchi na nikaeleza kwamba, kule kulitokea matatizo. Naomba sasa niseme kwamba, kulitokea mapigano kutokana na tatizo hilo la *net*, *OCD* wa Karatu aliwekwa chini ya ulinzi na wananchi katika mapigano hayo mpaka Jeshi la *FFU* likaletwa kutoka Arusha.

Hili ni jambo zito, Waziri anasema kwamba kuna kulalamika; tusipotoa taarifa hizi ndani ya Bunge tuzipeleke wapi? Utoaji wa taarifa hizi zinazokuwa ni hujuma kwa nchi yetu, zisipochukuliwa hatua tuzipeleke wapi? Wizara hii baada ya kuingia kwenye *Customs Union,* ndiyo mratibu kama alivyosema. Tusipopeleka kwa mratibu tupeleke kwa nani? Sisi Karatu tulichukua hatua, Mkoa ukaingilia tukashindwa namna ya kutatua baada ya Mkoa kuingilia, kwa sababu walituambia biashara ni huria na sisi hatukuwa na madaraka tena, wananchi wetu wamepigana, maisha karibu yapotezwe. Tukitoa hili Waziri anasema tabia hii ya Mawaziri kutoa kauli za aina hii, itaisha lini? Naomba tamko la Serikali. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, kwa hili la kwanza sidhani kama Mwenyekiti nimekuelewa vizuri. Nitakupa dakika mbili ili uliweke vizuri zaidi.

Alichokizungumza Naibu Waziri ni kwamba, sisi Watanzania kama tunajua wenzetu Kenya na Mataifa mengine, wanapokwenda kuuza na sisi tufuatilie utaratibu huo tupate masoko yale, badala ya kulalamika. Nakupa fursa ni maelezo gani zaidi unayoyahitaji?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani wewe kwa kuwa si mwuliza swali, huwezi kuelewa nilichosema mimi niliyeuliza, jina langu ndiyo limetajwa wakati anajibu Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, nilitegemea hoja niliyoitoa itapata majibu kwamba, tatizo hili ufumbuzi wake ni huu na si kuambiwa kwamba tusilalamike lalamike, nilitegemea kwamba tutaambiwa utaratibu huu tutaufuata hivi. Ndiyo maelezo ninayoomba kwamba, sasa tuambiwe inapofikia hatua hiyo twende wapi na Serikali inatoa kauli gani?

**MWENYEKITI:** Hatua ipi Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ipi nilieleza labda nirudie mchango kama nilivyochangia kwa dakika kumi na tano kwa sababu wakati ule…

**MWENYEKITI:** Sasa unabishana na Mwenyekiti, ili swali liende upande wa pili upate maelezo zaidi ni vizuri ukawa *brief* na wewe ni *Doctor,* kuwa *brief* ni kitu gani *in particular,* ambacho unataka maelezo zaidi. Najaribu kuweka masuala haya yaeleweke vizuri kwa kila mtu. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nilisema hivi; utaratibu ambao tungependa Serikali itoe kauli, hawa wafanyabiashara wanapoingia nchini kwetu na ndiyo jibu nililotaka; utaratibu huu uweje, kwa sababu hakuna anayejulikana, mwenye mamlaka ambaye sisi tumemchukulia hatua, Mkoa umeingilia. Nilieleza haya nilitegemea kwamba, Waziri atakuwa ameelewa. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, katika mchango pia nilieleza kuhusu wafanyakazi, nashukuru Waziri amesema kwamba, sasa kuna Kamati zimeundwa, lakini bahati nzuri amesema kwamba, Kamati hizi zimeundwa nadhani kama mwezi mmoja au miezi miwili iliyopita. Nilitaka nipate uhakika, taarifa hizi za Kamati zitaisha lini, kwa sababu ndani ya Bunge hili tulikwisha kuwaambia kwamba, watumishi wale ambao wanakuja kutoka nje wasio sifa, Serikali inawaondoa na taarifa hii imeelezwa ndani ya Bunge hili mara nyingi.

Mimi ni Mbunge sasa kwa mwaka wa 12 na muda mrefu tu taarifa hizi zimetolewa. Sasa nimesema kwenye hoteli wale wahudumu, wabeba masanduku, wale wote ambao si zile nafasi tano kama sheria zinavyotaka wanaofanya kazi; je, Kamati hizi Waziri atatuhakikishia itafanya kazi lini ili watu wote wasiohusika waondolewe na Watanzania ambao wanastahili hizi nafasi za kazi, wapate hizi nafasi tusiendelee kupoteza nafasi ya Watanzania wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kuhusiana na utaratibu wa jinsi wafanyabiashara kutoka Kenya kuingia Tanzania na hili la Kamati.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala alilolisema Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa ni suala mahususi. Asema pia kwamba, mpaka ngazi ya Wilaya na Mkoa, wameingilia baada ya wao kuchukua hatua. Nataka niseme kwamba, hizo ngazi alizozitaja ni ngazi za Serikali. Suala hili kalileta hapa sasa hivi, nachelea kulitoa kauli moja kwa moja, bila ya kuwa na taarifa kamili kutoka kwenye upande wa Serikali pia. Nataka nimuahidi Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kwamba, hii ni Serikali ambayo haitaki wananchi wake wadhulumiwe, hii ni Serikali ambayo haitaki wananchi wake wahujumiwe na kama yanayozungumzwa ndivyo, basi Serikali itachukua hatua. Lakini tungependa tupate fursa kupitia sekta husika ili hili suala litazamwe vizuri. Kwa sababu kuna hatari ya kutoa kauli hapa ikawa ni tofauti, wakati mwingine ikawa ni mwenendo wa mambo yalivyokuwa. Lakini tunamheshimu Mheshimiwa Mbunge, kwa kuleta suala hili na tulidhani kwamba, ni suala ambalo lingeweza kwanza kushughulikiwa kule Mkoani, lakini yeye mwenyewe amesema Mkoa umeingilia na ametoa sura kama vile kuna matatizo ya aina fulani. Kwa sababu hiyo, ndiyo maana nasita kutoa majibu ya moja kwa moja kwenye suala hili.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Sijakuita Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nadhani ndiyo aina ya jibu tulilokuwa tunataka kwamba, suala litashughulikiwa hatukutaka kitu zaidi ya pale. Naomba niseme kwamba, ulinikatisha pale nilikuwa naendelea kueleza. Ile ya Mkoa kuingilia ilikuwa ni mapema kama mwaka mmoja uliopita, baada ya Mkoa kuingilia ndiyo watu wetu wakamkamata *OCD* na watu wake na kuwaweka kwenye *siege* kwa zaidi ya siku tatu. Sasa juzi nimepigiwa simu hali hiyo imeanza tena.

Kwa hiyo, nashukuru kama Waziri anasema atalifuatilia kwa taratibu za kawaida, mimi sioni kama kuna tatizo. Kwa hiyo, naridhika kama suala litafanyiwa kazi kwa utaratibu wa kawaida.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru maelezo ya Mheshimiwa Waziri kwamba, watafuatilia suala mahususi kwa Karatu. Lakini bado ningetaka kurudia kauli ile ambayo pengine hukuielewa vizuri. Tunachosema, tusaidiane viongozi wote, Waheshimiwa Wabunge, tusaidie kuwaelimisha watu wetu, wanapokwenda kwenye Soko la Afrika Mashariki wasiwe wanyonge. Wachangamkie shughuli hizi, wapambane kibiashara maana yake ni mapambano ya kibiashara haya.

Tukiwaachia watu kwamba tutakuja kulalamika, hapana lazima watu wetu waende kifua mbele, wachangamkie fursa hizi za kibiashara. Bila kuchangamkia, tutaonekana kila sisi tuko nyuma kuliko Kenya, tuko nyuma kuliko Uganda, kumbe watu wanaweza kama tukiwa-*encourage* na kuwasaidia wachangamkie fursa hizi. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, wakati nachangia nilizungumzia suala la *EPA,* ambalo kwa kweli sijapata ufafanuzi wa kina ambao uko *clear.* *EPA* ni makubaliano ya ubia wa kiuchumi *(Economic Partnership Agreement),* kwa kifupi *EPA,* kwa Kiswahili kifupi (MUK) Makubaliano ya Ubia wa Kiuchumi kati ya nchi za *EU* na *ACP*. Makubaliano haya yanajadiliwa kwenye vikundi vya nchi mbalimbali. Mwaka 2003, Wakuu wa Nchi za Afrika ya Mashariki, walikubaliana kwamba, tujadiliane haya makubaliano kupitia *East African Community,* baadaye wenzetu Kenya na Uganda wakawa wamekiuka haya makubaliano wakaenda kujadiliana kupitia *ESA*.

Nakubaliana na wewe Mheshimiwa Waziri kwamba, *EPA Configurations* siyo umoja wa kikanda ni umoja ambao ulikuwa mahususi kwa ajili ya suala hili. Lakini jambo la msingi ambalo labda Mheshimiwa Waziri, angepaswa kulizingatia ni kwamba, makubaliano ya *EPA* siyo makubaliano tu ni makubaliano ambayo yanapelekea nchi kupoteza mapato kutokana na forodha. Hapa nina matokeo ya *studies* nane, ambazo zimefanywa na watalaamu mbalimbali, ambazo zinaonesha kwamba, asilimia 46 ya mapato yetu yanayotokana na forodha, yatapotea kuanzia tarehe 1 Januari, 2008 mara baada ya kusaini *EPA*. Kwa hiyo, kuchelewa kwetu kuamua *configuration,* kutatuathiri sana Taifa kwa sababu ni lazima tusaini *EPA* na *WTO.* Asilimia 46 ya mapato ya forodha yanayopotea ni sawa na asilimia 6.6 ya *revenue* yote ya Serikali, ambayo ukichukua bajeti ya mwaka huu ni jumla ya shilingi bilioni 250.

Wakuu wa Nchi wakakubaliana tena mwaka huu kwamba, turudi kwenye *East Africa,* wenzetu Kenya kupitia kwa Wizara yao, wakatugeuka kinyumenyume wakaandika barua kwenda *Brussels* kupinga *configuration* ya *EAC.* Waheshimiwa Wabunge kadhaa, wameshauri wakasema kwa kuwa *EPA Configuration* siyo ushirikiano wa kikanda ni suala la majadiliano na nchi za Jumuiya ya Ulaya, tuendelee na majadiliano na Uganda, Ruanda na Burundi na tuombe *DRC* tuachane na Kenya wao waendelee kujadili kupitia *ESA*. Lakini Mheshimiwa Waziri, hujalieleza kabisa hili na unasema tuvute subira, utavutaje subira wakati tunasaini mwezi Desemba, tulikuwa tunaomba maelezo ya kina kuhusiana na hili kwa sababu linahusu maslahi ya taifa na ni lazima tuwe *serious* katika maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilidhani suala hili la *EPA* nililieleza vya kutosha kwamba, sisi kama Serikali, tunakubali kwamba tukiwa katika *EPA* ya Afrika ya Mashariki, maslahi yetu na maslahi ya jumuiya, yatakuwa bora zaidi. Nimetoa maelezo ya awali kwamba, suala hili sasa linashughulikiwa, ni dhahiri kama limeshughulikiwa lazima nitamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira hayo ndiyo mambo yanavyokwenda na akatoa mtiririko wa vikao vinavyofuata akatoa mfano kama kutakuwa na Mkutano wa Mawaziri wa Afrika Mashariki na wa Viwanda na Biashara tarehe 16 Agosti, 2007, Mjini Arusha.

Sasa sijui Mheshimiwa Mbunge, alikuwa hakulisikia hili, lakini ndiyo maelezo niliyoyatoa kwamba, tusubiri uamuzi. Niseme tu kwamba, kama Wakuu wa Nchi zetu watafanya uamuzi watakapokutana, bado tutakuwa hatujachelewa, tumefanya

mawasiliano na *European Union,* bado tutakuwa tuna muda. Lakini ninachosema, suala hili liko katika mchakato, hebu tuliache vikao vinavyohusika vishughulikie.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri, mwenye dhamana ya Afrika Mashariki, ningeomba kutoa nyongeza tu kwa suala la *EPA. Argument* au mgogoro mkubwa uliopo ni kwamba, wenzetu wa *EPA* wanaoshughulikia migogoro hii, kidogo kuna *selective engagement,* kuna upendeleo kwa mfano, South Africa peke yake imeruhusiwa kuingia *EPA Agreement,* nchi moja tu. *Argument* ya pili, *SADC* ile imechukuliwa kwenye *SACU,* ambayo ni *South Africa Customs Union,* ina nchi nne tu na wamekubali kuingia kwenye *EPA*. Swali ambalo Mheshimiwa Rais na wote tulili-*pose* ni kwamba, kama South Africa imeruhusiwa kuingia kwenye mkataba peke yake, kama *SACU* kwa nchi nne za *SADC,* zimeruhusiwa kuingia mkataba na *EPA* peke yao; kwa nini Afrika Mashariki, ambayo kwanza ina nchi zaidi ya tatu, lakini pili *we are the only country* katika Afrika, ambayo tuko kwenye *Customs Union;* kwa nini hatu-*qualify* kuingia kwenye *EPA Agreement*?

Walikuwa na kigugumizi kwa sababu nilikuwa *Brussels* na Mheshimiwa Rais. Wakaingiwa kigugumizi, wakatulazimisha kwamba itabidi sisi tu-*expand,* yaani Afrika Mashariki i-*expand* na *COMESA* na sisi siyo *members* wa *COMESA* au tugawane pale *for the purpose* ya *envelope* kwa sisi Tanzania ama twende *SADC* na wenzetu Kenya, Uganda waende kwenye *COMESA*, lakini *COMESA* siyo *Customs Union* na ndiyo maana kama Waziri anavyosema, sasa *deadline* tarehe 15 Desemba lakini tumeshawasiliana wa *European Union,* wasituburuze. Afrika Mashariki imeingia kwenye *Customs Union* na sisi wenyewe tunaweza tukaingia. Lakini ningependa pia kulisema suala lingine, ingawa *deadline* tarehe 15 na athari zinaweza kupatikana, hii *process* ya *EPA* ni *on going,* sio *incidence* ambayo inakwisha sasa hivi. Ndiyo maana nakubaliana na mawazo ya Mheshimiwa Waziri kwamba, tuvute subira, tubuni mgogoro ambao tusipoangalia, tutakwenda ovyo ovyo lakini kuna ujanja pia hapa wa watu kutaka Tanzania iingie kwenye *COMESA*. Tunavutwa hapa kwa sababu Kenya na Uganda iko kwenye *COMESA, pressure* inayopelekewa hapa ni kwamba, Tanzania tujiunge kwenye *COMESA* ili tu-*qualify* kwenye *EPA*. Tumesema *we are not members of COMESA* na hutuna mpango huo. *East Africa* inaweza yenyewe kuingia kwenye *agreement. (Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika sana kusema kwamba, Waziri wa Jumuiya ya Afrika na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hawaelewi wanachokizungumza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema nasikitika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, kaa chini.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti - Kuhusu Utaratibu.

Kwanza, naomba niseme kwamba, Kanuni ya 51 fasili ya 8; kwanza ni marufuku kwa Mbunge yeyote kutumia lugha ya maudhi, lakini vilevile jambo analosema linahusiana zaidi na kanuni ya 50 fisili ya kwanza, Mheshimiwa anapozungumzia jambo na kuhukumu kitu ambacho hana uhakika nacho. Waheshimiwa Mawaziri, wanazungumzia hapa kwa sababu wamekuwa *involved* katika majadiliano mbalimbali, wanazungumzia jambo kwa *authority*. Kama Mheshimiwa Mbunge, ameshiriki katika vikao kupitia asasi mbalimbali za *NGOs* na kadhalika, hana *authority* katika mazungumzo katika *level* hii. Kwa hiyo, naomba afute usemi wake na kwa kweli siyo jambo zuri na kauli nzuri kurudia kusema. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Sijakuita bado. Sasa nakuita na nakushauri ufute yale maneno.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba niseme rasmi kwamba, mimi ni *consultant* wa mambo ya *EPA* na nimefanya kazi na Serikali kupitia Wizara ya Fedha na ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, kaa chini. Maneno unayozungumza yanavunja heshima na hadhi ya Waheshimiwa Mawaziri, ambao ndiyo wanaotuwakilisha katika mazungumzo yote haya. Ndiyo wenye dhamana hii nzito, pamoja na *qualifications* zote utakazozielezea hapa, bado hazitaku-*qualify* kuweza ku-*caution intelligence* yao *on a personal level.* *(Makofi)*

Kumwambia mtu mzima na ni kiongozi, hajui anachokiongea ni kosa, ni vizuri kuwa muungwana. Nimekushauri kwamba, u-*withdraw* hiyo kitu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nimeeleweka na wenzangu wameona kwamba, nimeongea kitu ambacho kimewaudhi, kwa kweli naomba radhi. *Point* yangu ninayotaka kuizungumza ni kwamba, nina *authority* ya kuzungumzia masuala ya *EPA,* kwa sababu nimekuwa *engaged* na Serikali, nimekuwa *Consultant* wa Wizara ya Fedha, kuhusu suala hili na nimekuwa nikitoa ushauri wa aina mbalimbali toka nimeingia Bungeni na nimesema leo asubuhi kwamba, hii ni mara yangu ya tano naongelea suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, South Africa kwa mfano, haina *EPA Aggrement*, wame-*sign* makubaliano ya kibiashara na nchi za Jumuiya ya Ulaya mwaka 1999, *TDCA* nje ya *EPA Aggrement* na sasa hivi imeomba ku-*re-negotiate* makubaliano yao kupitia *SADC,* kitu ambacho kinaathiri zaidi maslahi ya Taifa. Ninachokizungumza mimi hapa ni kwamba, maslahi ya Taifa hayajazingatiwa katika majibu yote ambayo Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, ameyazungumza. Hakuna suala la maslahi ya Taifa ambalo limezingatiwa na halijazingatiwa, kwa sababu ambazo naomba nizieleze hapa, nina dakika tano kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Summit* iliyopita ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, iliyokutana Kampala ndiyo ambayo ilikuwa ifanye maamuzi kuhusiana na *Confederation* ya *East African Community*. Lakini kufuatia barua ambayo Mkisa Kitui aliituma Brussels kwa *Chief Negotiator* wa *EU on EPA,* Bwana Facon Bag na ambayo naamini Waziri Msabaha alivyoenda juzi Brussels ameonana naye na wamelizungumza hili. Barua ile ikapelekea wenzetu wa Kenya kupitia Kiongozi wao, kushindwa kukubaliana na wengine wanne na hapo ninachokisema maslahi ya Taifa ni vipi, kwa sababu *East African Community as a Secretariat* inaweza ika-*negotiate EPA minus,* kwa sababu *EPA* siyo *Regional Group.* Kwa hiyo, tunachokitaka sisi au ninachokitaka, mimi niweke *very clear* kwa Serikali kwanza, wakubali kwamba Wakenya wamekwenda kinyume na makubaliano na hili ndiyo suala ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameweza kulizungumzia hapa, wanatufanya tuonekane wanyonge, wakati sisi kama Taifa, tuna *potentialities* za kuweza kuhakikisha kwamba tunafaidika na makubaliano ya kiuchumi ambayo yanatokea.

Kwa hiyo, ninachokiomba kwa Mheshimiwa Waziri wa Afrika Mashariki na ninachokiomba kwa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje, licha ya kuwakwaza hapo nyuma kidogo na nimeomba radhi kwa kweli inatoka moyoni kabisa, nimeomba radhi kwa ambayo nilisema. Tunaomba tuweke maslahi ya Taifa letu mbele na twende ku-*negotiate EPA* bila ya Kenya, kwa sababu Kenya wana maslahi zaidi. Asante Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, muda wako umekwisha.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania inajua inachofanya. Hatuko hapa kuelezana sifa zetu, wapo watu wa aina mbalimbali humu ndani. Hatuko hapa kuelezana sifa zetu. Lakini Serikali ya Tanzania inajua inachofanya na hapa kama Bunge, hatuwezi tukakaa ukategemea kwamba, Serikali itakuwa inazungumza au inamzunguka Waziri wa nchi nyingine. Siyo utaratibu. *(Makofi)*

Lakini ninachotaka kusema ni kwamba, sisi tunajua tunachofanya na kwamba, tunazingatia makubaliano ya Wakuu wa Nchi kwamba, suala hili watalizungumza tena na kulifanyia maamuzi watakapokutana tarehe 20 na mimi nataka nirejee kusema kwamba, masuala yote yanayohusu *EPA,* Serikali itachukua uamuzi kwa kuzingatia maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Naomba tena nitoe nyongeza na nashukuru ndugu yangu amefuta usemi. Jambo hili ni rahisi sana. Mimi nazungumzia sasa maslahi ya Taifa. Maslahi ya Taifa ni nini?

Maslahi ya Taifa katika *EPA* ni kwamba, Tanzania, Kenya na Uganda ni ndugu na tuko kwenye *Customs Union.* Tanzania, Burundi, Rwanda, pamoja na hizo nchi tatu ndizo zinazo-*form Customs Union.* Swali ambalo mwenzetu ambaye ni *Consultant* lazima tushirikiane kutetea maslahi ya Taifa ni moja kubwa, kwa nini sisi kama *Customs Union,* tangu mwezi Machi wamekataa watu wa *EPA* tusi-*negotiate* nao. Narudia tena na

kuiruhusu Afrika ya Kusini, kuiruhusu *SACU,* mbona Mheshimiwa haizungumzii *SACU, The South African Customs Union,* ambayo ina nchi nne tu.

Kwa nini nchi zile zimeruhusiwa ku-*negotiate* kwenye *EPA Aggrements* na kwa nini *South Africa as an entity,* nchi moja imeruhusiwa kuzungumza na *EPA*, yaani ku-*negotiate EPA.* Sisi katika Afrika Mashariki, kwa njama za kututaka ku-*join the COMESA,* jambo ambalo hatupo tayari, wanataka kutulazimisha tu-j*oin* ama *SADC* au tu-*join COMESA* na tuiache Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ndiyo maana Kenya haikufanikiwa kwenda *unilaterally.* Lazima nchi zote kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, Marais wakutane, Afrika Mashariki i-*qualify* yenyewe, *on its own,* kuingia kwenye *EPA Aggrements.* Jambo hili halihitaji kusoma, wala mtu hahitaji kuwa *Consultant* kulifahamu. Ni jambo rahisi sana. *(Makofi)*

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, pamoja na mambo mengine, nili-*raise* suala la kwamba, Tanzania kwa lugha ambayo imeandikwa kwenye vitabu, *aggreed to remove suspended duties on firestone imports, firestone tyres imports from Kenya.* Maana yake nini hii kwa uchumi wetu sisi Tanzania na hasa ukizingatia kiwanda chetu cha matairi cha Tanzania.

Kama uelewa wangu ni sahihi, ni kwamba, tunapoteza *duties at the same time* tunapoteza soko la matairi yetu ya *General Tyre* na tatu tutaathiri ajira za wafanyakazi wa kiwanda chetu cha *General Tyre.* Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi juu ya hili. *(Makofi)*

Lakini la pili, nilichangia vilevile pamoja na mengine, lilikuwa ni suala zima la ku-*strengthen East African Development Bank,* kama Benki ya Rasilimali kwa Afrika ya Mashariki. Mambo haya tunayoyazungumza ya maendeleo kwa Afrika Mashariki, hayawezekani bila pesa, tena za muda mrefu. Pesa kwa maana ya mikopo ya muda mrefu, itapatikana kwenye Benki ya Maendeleo.

Kwa bahati nzuri, tunayo Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki, ambayo ili-*survive the collapse of the first East African Community.* Nikatoa rai kwamba, kupitia Wizara hii, changamoto iwe ni kuiunda upya na kuipa nguvu benki hii ili isaidie maendeleo haya ya Afrika Mashariki. Mheshimiwa Waziri, hakuwa ametoa ufafanuzi wa hayo na sasa naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nilitaka nimshukuru Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, kwa mawazo yake mazuri juu ya Benki ya Afrika Mashariki. Mimi nadhani tunakubaliana na ushauri wake na ndivyo inavyopaswa kuwa, tujitahidi katika kuhakikisha kwamba, Benki hii inatoa mchango mkubwa katika ujenzi wa Jumuiya.

Sasa lile la pili alilolizungumzia juu ya kiwanda chetu. Hoja ya msingi mimi nadhani aliizungumza yeye kwamba ni muhimu tufufue kiwanda chetu au tukiboreshe

kiwanda chetu cha kutengeneza Matairi Arusha. Mimi naamini Serikali iko katika mchakato wa kushughulikia suala hili kupitia Wizara husika.

**MHE. SIRAJU J. KABOYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, lakini angenisaidia basi pale *Tanzania agreed to remove suspended duties on imports from Kenya* ina athari gani kwa uchumi wetu?

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninavyofahamu ni kwamba, baada ya *Customs Union* kuanza, suala la *suspended duties* halipo, sasa hii taarifa anayotoa Mheshimiwa Mbunge, nadhani inabidi niifanyie kazi.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nashukuru Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwanza, naomba uniruhusu nitoe maelezo ya utangulizi, kabla ya kuuliza yale masuala ninayotaka ufafanuzi ili niweke sawa *records.* Nilikuandikia kukuambia kwamba, kutokana na ushirikiano wa kiuchumi wa Afrika Mashariki, mimi ninauhitaji. Lakini ushirikiano wa kisiasa, kwa sababu katika ushirikiano wa kiuchumi na sisi Pemba kule ni majirani wa Kenya, kama walivyo majirani wengine waliokubali kama Wabunge sita na yule mwakilishi mmoja, aliyekubali kwamba Shirikisho la Kisiasa lianze mara moja.

Mimi napendelea kiuchumi tuanze mara moja, kwa sababu karafuu zetu sisi hatuna bei kule SMZ. Kule tunapata bei kubwa, kwa maana hiyo kiuchumi nahitaji tuanze hivi sasa, lakini kisiasa itachukua muda. Ndiyo maana hata katika chama chetu tunasema, uchumi ndiyo uongeze siasa na si siasa iongoze uchumi. *(Makofi)*

Baada ya ufafanuzi huo, kwa *record* nilikuwa nahitaji ufafanuzi kuhusu *Customs Union.* Ningeomba Mheshimiwa Waziri atufafanulie, kuna siri gani katika Umoja wa Forodha, ambao ulikuwa ukamilike 2005 tu kwanza tumefikia wapi mpaka hivi sasa? Halafu kuna siri gani kwamba, Kenya wao kuingiza bidhaa nchini wanalipa ushuru. Tanzania tumeruhusiwa tusilipe ushuru kuingiza bidhaa Kenya, kwa kipindi cha miaka mitano na hivi sasa miaka miwili imeshapita. Je, tumelenga wapi Tanzania baada ya hii miaka mitatu na sisi tutakua kiviwanda kama Kenya au pana siri gani hapa na wao kukubali hilo Kenya? Naomba ufafanuzi ahsante.

**MWENYEKITI:** Kabla ya ufafanuzi, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, sijaelewa tatizo ni nini, maana ipo *comperative advantage,* wewe unakuwa na faida zaidi kama Mtanzania. Swali lako hasa unataka ufafanuzi kuhusu nini?

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Miaka mitatu iliyobakia, itabidi na sisi tulipe ushuru kuingiza bidhaa Kenya. Je, uwiano wa kisoko na kiviwanda tutakuwa na sisi tumeshafikia Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Kwa niaba ya Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kwamba, Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki ulianza tarehe 1 Januari, 2005 na tunatarajia mpaka 2010, ndiyo bidhaa zinazotoka Kenya kuja Tanzania zitatozwa ushuru unaoenda unapungua taratibu, ifikapo mwaka 2010 itakuwa *zero.* Lakini tutakapofikia 2010, haimaanishi kwamba, sasa bidhaa zetu zinazoenda Kenya zitaanza kutozwa ushuru, hapana haimahanishi hivyo zitaendelea. 2010 tutafanya tathmini kama Jumuiya, kuangalia ni mambo yapi yametokea katika kipindi hicho, tumejifunza nini na twende vipi katika awamu nyingine ambayo italenga kwa mfano, *Common External Tariff,* hivi sasa ni asilimia 25, lakini hatua ya pili itakuwa asilimia 20, baada ya kufanya tathmini. Lakini si kwamba bidhaa za Tanzania zitaanza kutozwa ushuru kwenda Kenya. Tutafanya tathmini tuone kama itaonekana kuna matatizo, basi tutashauriana kwenye vikao, tuone tufanye nini kuendelea kulinda viwanda vya nchi itakayoonekana inaweza kuathirika.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kuuliza Serikali imeshatoa maelezo. Naomba ni-*withdraw.* *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati*
*ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finace and Accounts* ....... ....... ....... Sh. 205,228,800.00

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. *Vote 97, Sub-Vote 1002, item 250100.* Nilikuwa naomba ufafanuzi kidogo. Nijuavyo mimi, mshahara ni kipato halali anachopata mwajiriwa kwa kufanya kazi na kipato hicho huwa anakipata kila mwezi na ninavyojua pia, mishahara ya wafanyakazi imeongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwenye hiyo *Sub-item* niliyosema ni kwamba, mishahara imepungua kwa shilingi milioni 14. Sasa nilikuwa naomba kuuliza; je, wafanyakazi wamepunguzwa au ni kwa nini hali iko hivi? Asante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ujumla, nadhani amelinganisha mwaka jana na mwaka huu. Ule mshahara ulioko pale ndiyo wa idadi ya wafanyakazi ambao wapo katika Idara inayohusika, mshahara uliopo hapa. Kwa hiyo, ni *level* ya *employment* ambayo imetokana na wafanyakazi kama walivyopatikana, ukilinganisha na ambavyo ilivyotarajiwa iwe mwaka jana.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa na nadhani Waziri pia amenielewa kwamba, nilikuwa nazungumzia kitengo hicho hicho, ndiyo sababu nimeuliza; najua mishahara imeongezeka; je, wafanyakazi wamepungua kwa sababu ukiangalia mshahara wa mwaka jana ni mkubwa zaidi kuliko hivi sasa? Sasa nilikuwa naomba kujua kama wafanyakazi wa kitengo hicho wamepunguzwa.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nimetoa maelezo kwamba, katika kifungu hiki kwanza, kuna suala

kwamba wengine wanalipwa kutokana na suala la mishahara kwa ujumla katika Wizara. Hawa ambao wapo katika kitengo hiki, ndiyo wapo katika *level* ya watakaolipwa kwa pesa hizo. Kwa hiyo, kwa maana nyingine si kwamba, wamepungua hapana. *Comparison* ya mwaka ilitokana na makisio kama wangeweza kuajiriwa wote, lakini walioajiriwa ni pungufu ya ile idadi ambayo ilitarajiwa. Kwa hiyo, hiki kilichopo ndicho kitakachoweza kuwalipa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1003 - *Policy and Planning* .. ..... .... ..... Sh. 5,688,050,600.00
Kif. 1004 - *Trade, Finance and Investment* ... .... Sh. 290,285,000.00
Kif. 1005 - *Economic and Social Infrastructure* . ...... Sh. 320,159,300.00
Kif. 1006 - *Political, Defence and Security* .... .... Sh. 101,416,900.00

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu hadi kifungu na kupitisha vifungu hivi bila mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Bajeti ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kama tulivyoomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2007/2008 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo tumefikia mwisho wa shughuli zilizokuwa zimepangwa kwenye *Order Paper* ya leo. Nawashukuru sana kwa ushirikiano mlioutoa. Niseme tu kwamba, katika Kanuni zetu mpya tutakazokuwa nazo baada ya muda si mrefu, moja ya matatizo ambayo yatakuwa yamepatiwa ufumbuzi ni kumwezesha Spika, kuweza kutoa adhabu ndogo ndogo, bila kusubiri kwa wale ambao wanakiuka viwango kabisa nje ya utaratibu uliowekwa. Kwa hiyo, tunatumaini Kanuni hizo zitasaidia kuweka mazingira na taratibu za uendeshaji wa Bunge letu vizuri zaidi kwa Spika, kutokusubiri kushtaki kwenye Kamati inayohusika, badala yake anakuwa na mamlaka ya kuweza kutoa adhabu ndogo ndogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, shughuli za leo zimekwisha. Kwa hiyo, naahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.22 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Agosti, 2007 Saa Tatu Asubuhi)*